ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 3 Julai, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuweka mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 43

Jitihada za Kupinga Vitendo Viovu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Jumuiya ya kinamama ya *FISABILIH MARKAZ* ya Fuoni ilikutana katika Semina iliyojadili tatizo la kuporomoka mila na silka na tamaduni hasa kujitokeza tatizo la ULAWITI ambalo huja kwenda hata na kinyume na misingi ya dini na maadili.

a) Wizara kupitia Ofisi ya Mufti imechukua juhudi gani za kupambana na tatizo hili kupitia viongozi wa dini na kukemea matatizo hayo.

b) Serikali inasaidia vipi Jumuiya zinazojitokeza na kutoa elimu ya kupiga vita vitendo hivyo kama inavyofanya jumuiya ya *Fisabilillah Markaz*.

c) Ofisi ya Mufti imeshatumia kiasi gani cha fedha katika mwaka uliyopita katika kuzisaidia Jumuiya za dini zilizosajiliwa ambazo zinatoa elimu kwa maisha bora yanayopata kuzingatiwa na kila binaadamu kulingana na matakwa ya dini.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kupitia Ofisi ya Mufti imekua ikishirikiana na jumuiya mbali mbali za kiraia katika kupiga vita mporomoko wa mila, silka na tamaduni zetu za Zanzibar, ikiwemo Jumuiya ya *Fisabalillah Markaz* ya Fuoni.

Kwa kushirikiana na taasisi hizo, Ofisi ya Mufti imekua ikichukua hatua mbali mbali katika kupambana na tatizo la ulawiti ikiwemo kutoa elimu juu ya ubaya wa jambo hili, kupitia ziara, vipindi vya redio na televisheni, semina na makongamano mbali mbali. Jumla ya vipindi 12 vya televisheni na redio kuhusiana na tatizo hili vimeandaliwa na kurushwa hewani. Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wananchi wa Zanzibar kuendelea kushirikiana na taasisi zetu za dini ili kupiga vita vitendo hivi ambavyo vinapelekea kuharibu mila, silka na utamaduni wetu wa Kiislamu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kupitia serikali kupitia Afisi ya Mufti inachukua hatua mbali mbali za kuzisaidia jumuiya zinazojitokeza katika katoa elimu ya kupiga vita vitendo vya ulawiti, ikiwemo kushirikiana nazo katika kutoa elimu, kuzijengea uwezo pamoja na kuwapa fikra na miongozo inayostahiki ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa misingi ya kiislamu.

(c) Mhe. Mwenyekiti, serikali haina utaratibu wa kuzipatia fedha Jumuiya za Kiraia katika kutekeleza majukumu yake, ingawa inashirikiana nazo katika kuzipatia misaada ya kitaalamu katika kutoa elimu kwa jamii, kulingana na matakwa ya ya dini. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza Jumuiya ya *Markaz* ya Fuoni kwa kazi kubwa wanayoifanya kuelimisha jamii.

(a) Je, wizara yako imechukua hatua gani ya haraka haraka kuelimisha au kukuza kuwasaidia katika elimu hii kubwa ambayo wanayoitoa jumuiya hiyo.

(b) Ofisi ya Mufti katika mwaka uliopita imepokea kesi ngapi za migogoro ya wanandoa wanaume wanaodai unyumba kinyume na maumbile.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, wizara kupitia ofisi hii ya Mufti imekuwa ikifanya jutihada za kutosha kuhakikisha kwamba inashirikiana na jumuiya mbali mbali zinazohusiana na masuala ya kidini ikiwemo hii Jumuiya ya *Fisabilillah Markaz.*

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni ofisi hii ilielekeza nguvu zake Pemba na ilikuwa ikishirikiana na Mashekhe pamoja na jumuiya hizi zinazohusiana na masuala haya ya Kiislamu ili kuhakikisha kwamba inatoa elimu ili jamii wetu iweze kuishi vizuri na kuwa na maadili mema ya Kiislamu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine la Mhe. Mwakilishi, ni kwamba anataka suala la takwimu, ofisi hii ya Mufti imepokea kesi ngapi za ulawiti. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hili suala kitakwimu na linahusu zaidi kufanya uchunguzi wa kina kuangalia kesi ngapi tumepokea za ulawiti, Mhe. Mwenyekiti uniruhusu nimuombe Mhe. Jaku, suala hili niweze kumletea kwa maandishi kama zipo, narejea kusema zipo na kama hazipo pia nitakujuulisha Mhe. Mwakilishi, kwamba hizi kesi hazipo. Ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri au bahati mbaya huwa tunapokea taarifa mbali mbali baadhi ya walimu wetu katika madrasa mbali mbali kuwafanyia udhalilishaji wanafunzi wao. Na kwa kuwa wenzetu hawa wanajitahidi *Fisabilillah Markaz* kutoa elimu na kuelimisha jamii juu ya adha hii wanayoipata watoto wetu. Je, wizara ina mpango gani wa kuwasaidia kama wizara ili suala hili lipigwe vita lisitokee tena katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa kumekuwa kukitokezea matatizo mbali mbali ambayo yanahusiana na masuala ya kuvuka maadili yetu ya Kizanzibari na hata maadili ya Kiislamu. Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama ni kwamba, serikali

kupitia ofisi hii ya Mufti imekuwa ikifanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba elimu inatolewa katika jumuiya mbali mbali ili jamii yetu iweze kuepukana na haya matatizo ambayo yanatokezea ambayo yanaenda kinyume na maadili ya Kizanzibar halikadhalika yanaenda kinyume na maadili ya Kiislamu.

Kwa hivyo, wizara kupitia ofisi hii imekuwa inafanya jitihada za kutosha pamoja na hayo kutoa elimu hata jumuiya wakati mwengine zinapakwama kifedha ni ofisi yetu hii ya Mufti imechukua jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba hutoa barua kwa zile jumuiya ambazo zinahitaji msaada ule kwenda kwa zile taasisi husika au watu husika ambao wangeweza kuzisaidia jumuiya hizi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana marefu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa Zanzibar *University* ina Kitengo cha *Islamic* Sheria na kwa kuwa inafanya tafiti mbali mbali katika *unit* ya Kiislamu ikiwemo ndoa, talaka pamoja na jinsia ya udhalilishaji. Je, serikali ina mashirikiano gani kuzipata tafiti zile na kuzifanyia kazi ili kuona mila, silka za Kizanzibari pamoja na Uislamu zinaendelea vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba, Chuo Kikuu cha Zanzibar kimekuwa kikifanya tafiti mbali mbali kwa wanafunzi wake ambapo pale wanapotaka kumaliza masomo yao ikiwemo utafiti huo wa masuala hayo ya Kiislamu.

Mhe. Mwenyekiti, nimwambie tu Mhe. Mwakilishi, tutafanya utaratibu kufuatilia zile *research* ambazo zinahusiana na masuala ya Kiislamu ili ziweze kutusaidia au kusaidia ofisi hii ya Mufti ili kufikia lile lengo husika. Nina maana ya kwamba tutachukua zile *research* za Kiislamu tu kwa sababu kama tunavyojua tafiti nyengine ambazo zinafanywa pale sio za Kiislamu. Kwa hivyo, tutachukua zile za Kiislamu ambazo nahisi kwamba zitatusaidia katika mustakabal mzima wa kuhakikisha kwamba tunapata elimu, Maafisa wetu wa Ofisi ya Mufti wanapata elimu zaidi ya zile *research* ambazo zimefanywa pale chuoni na baadae tutazitumia kuwapelekea wana jamii popote pale walipo hapa Zanzibar.

Nam. 80

Kudorora kwa Tamasha la Elimu Bila Malipo

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Tamasha la Elimu Bila ya Malipo ambayo ilishamiri sana katika miaka ya 1980 - 1990 na ilichangia kwa kiasi kikubwa kuibua vipaji vya vijana wetu ikiwemo michezo mbali mbali na usanii. Aidha, tamasha hilo lilisaidia sana kukuza udugu, Umoja na Mshikamano kati ya wanafunzi na walimu kutoka pande zote za Unguja na Pemba.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea tamasha hilo hivi sasa kudorora na kupoteza haiba yake kama vile zamani.

(b) Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba tamasha hilo la Elimu Bila ya Malipo linarudi hadhi yake kama pale lilipoanzishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nitatoa maelezo marefu kidogo ambayo yatafafanua mambo mengi pamoja na jibu linalohusiana na suala hili.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein mwaka 2015 aliamua kwa makusudi kabisa kuunda Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu, kwa lengo la kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo na utamaduni kwa wanafunzi na hatimae kurejesha hamasa na vuguvugu kama ilivyokua katika miaka iliyopita.Tayari idara imekamilisha muundo wake pamoja na kuandaa mpango wa miaka mitano wa kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo na utamaduni, mpango ambao umeandaliwa kwa mashirikiano na Maafisa wa Elimu Mkoa na Wilaya zote, Walimu Wakuu wa msingi na sekondari Unguja na Pemba, walimu wa michezo na utamaduni, vyama vya michezo, Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar, wachezaji wa zamani, pamoja na wadau wengine muhimu na tayari shughuli hizi zimeanza kutekelezwa katika skuli zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuwepo kwa mpango huu kutasaidia kutatua changamoto zinazokabili sekta hizi hasa katika kupata wataalamu wa kusimamia michezo na utamaduni, upatikanaji wa vifaa na viwanja vya michezo, kuimarika kwa mashindano ya Tamasha la Elimu bila Malipo, *UMISSETA*, *FEASSA* na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, *WEMA* kupitia Idara ya Michezo na Utamaduni imefanya mapitio ya muongozo wa kazi nambari nne unaohusika na usimamizi na uendeshaji wa michezo na utamaduni katika skuli pamoja na kanuni zake ili kuongeza nguvu na ufanisi wa shughuli za michezo katika skuli. Muongozo huu unaelekeza wajibu wa wasimamizi na waendeshaji wote wa michezo na utamaduni wakiwemo walimu wakuu ambao ndio wasimamizi wakuu wa michezo na utamaduni katika skuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Mabaraza ya Utamaduni na Michezo katika elimu (*BUME*) katika Wilaya zote za Zanzibar yameimarishwa na yamejengewa uwezo na tayari yanafanya kazi zake vizuri kwa kusimamia vyema mashindano katika ngazi ya Kanda na Wilaya zao ambayo yanaendelea kwa sasa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuleta hamasa na vuguvugu la michezo, tayari Tamasha la Elimu Bila Malipo mwaka wa 2016 limezinduliwa rasmi katika Mkoa wa Kusini Pemba tarehe 13/02 ambapo Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake, Mhe. Hanuna Ibrahim Masoud kwa niaba ya Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba alilizindua na kuwaomba wahusika wote watoe mashirikiano kutimiza azma ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kurejesha hamasa na vuguvugu la Michezo katika skuli zetu. Aidha, uzinduzi katika Wilaya mbali mbali umefanyika kwa ufanisi mkubwa. *WEMA* imedhamiria kwa dhati kabisa kurejesha ule utamaduni wa asili wa kusherehekea kilele cha Tamasha la Elimu Bila Malipo katika muundo wa kubadilishana kati ya Unguja na Pemba ambao kwa kiasi kikubwa sana ulijenga heshima na hamasa ya Tamasha la Elimu Bila Malipo katika miaka iliyopita.

Mhe. Mwenyekiti, *WEMA* kupitia Idara ya Michezo na Utamaduni kwa kushirikiana na Kamati la *Olympic* Tanzania imetoa mafunzo ya Utawala na Usimamizi wa Michezo kwa viongozi/wasimaizi 100 wa ngazi ya Taifa na Wilaya ya Unguja na Pemba ili kuwajengea uwezo na kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa usimamizi wa michezo, aidha, walimu wakuu, walimu wa

michezo na utamaduni Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kukabiliana na changamoto zinazokwaza maendeleo ya michezo na utamaduni katika skuli. Mafunzo hayo yameongeza hamasa na ari kwa wasimamizi wa michezo na utamaduni na tayari jitihada hizi zimeanza kuleta matokeo mazuri ambapo vijana wetu wameanza kushajihika kushiriki michezo wakiwa skuli.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Tamasha la Elimu bila Malipo liliimarika sana na kuwa na hamasa na vuguvugu kubwa katika miaka ya 70 na 80 na hadi kufikia miaka ya 90, wanafunzi na walimu walishajihika sana kushiriki michezo na shughuli za sanaa, kulikua na ushindani mkubwa na wananchi walifurahia kuwepo kwa Tamasha hili, ila katika miaka ya 2000 haiba na vuguvugu la Tamasha imepotea kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha tamasha la Elimu Bila ya Malipo linarudi katika hadhi yake kama pale lilipoanzishwa. Wizara imejiandaa kukabiliana na changamoto zote zilizozorotesha kwa kuhakikisha yafuatayo:-

i. Kuwepo kwa usimamizi na uendeshaji wa michezo na utamaduni unaokidhi mahitaji ya sasa.
ii. Kutafuta wataalamu/walimu wa michezo na sanaa katika skuli zetu.
iii. Kuhamasisha wazazi na jamii kuunga mkono masuala ya michezo na utamaduni kama ilivyokuwa katika miaka iliyopita.
iv. Kutafuta vifaa na viwanja vya michezo jambo ambalo linachangiwa kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa maeneo ambayo yalitumika kwa shughuli za michezo.
v. Kuzijengea uwezo skuli zetu katika kukabiliana na changamoto za uendeshaji na usimamizi wa michezo, hasa gharama za maandalizi ya timu na mashindano.
vi. Kuongeza ushiriki katika michezo ya nje kama vile *UMISSETA, UMITASHUMTA NA FEASSA*.
vii. Kurejesha utamaduni wa kuendesha Tamasha la Elimu Bila Malipo kwa utaratibu wa kubadilishana kati ya Unguja na Pemba mwaka huu Pemba mwaka mwengine Unguja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu cha 37 Mhe. Mwenyekiti, mimi siwezi kusema msahafu kama wenzangu waliowahi kusema msahafu, msahafu hauwezi kubadilika, maneno yake yanakuwa yale yale mpaka leo hayajabadilika, lakini kanuni zinaweza kubadilika, kinasema;

"Waziri wa Wizara hiyo hiyo anayeulizwa suali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu suali hilo kwa kikamilifu, kwa

usahihi na kwa ufupi, isipokuwa kwamba Waziri au Mwanasheria mwengine".

Mhe. Mwenyekiti, suala alilojibu Mhe. Naibu Waziri, ni refu na limechukuwa muda, kanuni zetu hazituruhusu, nataka maelekezo ya kiti chako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimamia Kanuni ya 37, naomba ninukuu;

> "Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa suali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu suali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi na kwa ufupi isipokuwa kwamba suali akiulizwa Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine".

Mhe. Mwenyekiti, suali alilojibu Mhe. Naibu Waziri, ni refu sana na limechukuwa muda, nataka maelekezo ya kiti chako.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, naona alijieka hivyo kwa sababu ya kuongeza ufahamu wa hili suali lenyewe.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi nimshukuru sana Naibu Waziri, kwa majibu yake ya kina ambayo ameyatoa mpaka kunifilisi katika majibu yangu ya nyongeza, hilo kwanza nimsifu sana ni Naibu Waziri. niliyekuwa nampigia *salute* ametafuta vina vya nguvu amenifurahisha sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nikizungumza kihistoria kidogo tu kwa upande wa Tanzania Bara, Jumuiya ya Wazazi ambayo ndiyo ilikuwa kama ndiyo Wizara ya Elimu kwa upande wa miaka hiyo ndiyo iliyoleta uhuru katika kutafuta Uhuru wa Tanganyika. Elimu kwetu sisi ni changamoto kubwa...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, naomba uulize swala moja kwa moja.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninakuja Mheshimiwa, bila ya maelekezo nitakuwa kama siulizi vizuri, sawa nakubaliana na wewe. Dhamira ya elimu bila ya malipo ilikuwa ndio msingi mkubwa wa watu na kutokea kwa ufasaha wa kuletwa elimu bila ya malipo pamoja na changamoto zake. Kulitokea kasoro gani mpaka kudhorota kwa sherehe ambazo kwa Mheshimiwa. alivyozungumzwa silikuwa zinaleta tija kwa Serikali hii. Kulitokea kasoro gani ambazo zilifikia mpaka kudorora kwa elimu bila ya malipo. Hilo swala langu la kwanza lenye (a).

Mhe. Mwenyekiti, lakini (b) kama hakuna dhamira mbaya, sherehe zile zilileta mafanikio makubwa sana na kwa upande mmoja zinaleta kila haiba, maana yake zilileta michezo kwa afya, zilileta watu kuelewana, zilileta kila aina ya shamira. Mhe. Naibu Waziri, ananihakikishiaje kwamba sherehe zile zitarudi kama zamani, wakati ambapo hivi sasa Wizara ya Elimu hata magari ya kuchukulia watu haina. Kipindi kile ilikuwa sherehe zinaanza wakati Wizara ya Elimu ina ma-*ISUZU* na ina magari mengine, nakumbuka enzi zetu, yanaanza sherehe kutoka shule na shule mpaka wanapata watu ambao wana-*combine* kuja kuleta Zanzibar. Je, Serikali imejipangaje kuhusu suala hili kurudisha kama zamani katika mafanikio kama yale. Nashukuru Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe.Mwenyekiti, kwa ridhaa yako na kwa ruhusa ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan, Muwakilishi wa Jimbo la Chake Chake, masuala yake ya nyongeza (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la (a) ambalo linaulizia sababu zilizofanya kudhorota kwa mashindano haya tumejibu vyema katika masuala haya katika jibu la msingi, lakini ningependa kumuhakikishia kwamba au ningependa kumfafanulia zaidi kwamba, kulikuwa na sababu ambazo zilikuwa zinakwaza katika miaka hiyo. Sababu moja kubwa kabisa ilikuwa ni upungufu wa fedha za kuendeshea mashindano haya; na tuelewe kwamba kuendesha mashindano ni gharama kubwa sana, kwa hivyo, mashindano haya yalikuwa yanachangiwa na walimu, wanafunzi na tukaona kwamba tumewabebesha mizigo mingi; walimu, wanafunzi na wazazi wachangie masuala mengine, wachangie na masuala mengine ya elimu na kadhalika, kwa hivyo, hii ni sababu moja tu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna sababu nyengine ni kwamba kupunguwa kwa ari ya michezo kwa Zanzibar nzima pia kuliathiri kupunguwa ari ya michezo katika maskuli yetu. La tatu au sababu nyengine ya tatu, ni kwamba walimu katika maskuli walitia mkazo zaidi *curriculum* na wakapuuza masuala *extra curriculum activities* ambayo yote kwa pamoja ndiyo yanajenga mitaala ya skuli, yaani tulitilia mkazo zaidi masomo na tukapuuza shughuli za nje ya masomo ambayo kimtaala zote zimo katika skuli na zote ni muhimu. Hizo ni baadhi ya sababu.

Mhe. Mwenyekiti, (b) Katika suala ambalo Serikali itahakikisha vipi kwamba shughuli hizi zinarejea katika hadhi yake, tumeeleza kwamba Mhe.Rais ili kuona kwamba michezo inarejea katika skuli, ameunda Idara Maalum katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Na Idara hii pamoja na mambo mengine kazi yake ni kuibua vipaji, lakini huwezi kuibua vipaji bila ya

michezo, kwa hivyo, tunamuhakikishia Mhe. Muwakilishi na tunaihakikishia jamii kwamba Wizara ya Elimu itahakikisha kwamba Sherehe za Elimu Bila ya Malipo zinafanywa wakati wote na kwa upeo wa juu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Nchi katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais juzi alisema kwamba, katika sherehe ambayo moja haitosahaulika ni Sherehe ya Mapinduzi, basi ya pili itakuwa Elimu Bila ya Malipo. Ahsante.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza suali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri, yaliyokwenda shule na kwa kweli leo amethibitisha kwamba Mhe. Naibu Waziri, ni mwalimu. Lakini mbali na majibu yake ambayo ameeleza kuna shangamoto nyingi ambazo amezitaja takriban saba, akaongeza pia ari ya michezo ambayo imesababisha kutokuendelea matamasha haya ya michezo. Lakini suala langu ni kwamba, je, Wizara imejipanga vipi ili kutenda fedha na kutafuta wadhamini ili kuweza kuyaendesha matamasha haya, (b) je, Wizara inahitaji fedha kiasi gani ili kuweza kuyaendesha matamasha haya Elimu Bila ya Malipo kila mwaka?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Jazira, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni katika masuala yake kama yafuatayo (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Michezo na Utamaduni katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejipanga vyema kuona kwamba wanaendesha shughuli zake kwa ufanisi na kwa matarajio ambayo nchi imewekea. Katika kufanya hivyo, Idara hii imejipangia mbinu mbali mbali za kutafuta fedha kutoka vyanzo mbali mbali, kwa wahisani na taasisi nyengine ambazo zina maslahi ya kuendeleza michezo, na katika kufanya hivyo fedha za kuendeshea haya mafunzo ambayo tumeyasema, fedha hizo zimetoka kwa wahisani.

Mhe. Mwenyekiti, suala la (b), suala la fedha kiasi gani ambazo Wizara imejipanga kwa ajili ya kuendesha Tamasha la Elimu Bila ya Malipo hili namuomba nimuwakilishie kwa maandishi hapo baadae.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana. Mheshimiwa naomba baada ya kumshukuru Mhe.Naibu Waziri, kwa majibu mazuri sana, lakini naomba Mhe. Naibu Waziri, akumbuke kwamba huko kulikotoka Zanzibar vipaji vya michezo vilikuwa vikionekana kupitia Wizara ya Elimu na kipindi kifupi kwa

sababu yalikuwa yale mambo hayapo vipaji vilikufa. Sasa unavyotuambia fedha zinatoka kwa wahisani, wahisani wanaweza wakakupeni au wanaweza wasikupeni, ina maana kama hamjapata fedha kutoka kwa Wahisani hivi vipaji ndio havipo. Sasa tuambie kama mmekosa fedha kutoka kwa Wahisani, kutakuwaje, hii michezo au programu nzima katika Idara zenu ndio ziwe hazipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe.Hassan Khamis Hafidh wa Jimbo la Welezo katika swala lake kama hivi ifuatavyo: Ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pia imetenga fungu la fedha za kuendeshea michezo endapo hawa wahisani hawakupatikana.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kiasi gani mmetenga?

(*Hapa Mjumbe hakujibiwa swali lake kwa sababu aliuliza swali bila ya kuruhusiwa kisheria*)

Nam. 62

Kutokushuka Bei ya Umeme Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Ahsante sana Mhe. mwenyekiti, niko tayari hivi sasa kusubiri jawabu ya swali nam. 62

Karibuni kumekuwa na taarifa za uhakika kupitia vyombo vya habari kuwa *TANESCO* wameshusha bei za umeme karibu mara mbili, ambapo kwa hapa Zanzibar hatujasikia *ZECO* kushusha umeme ingawa wao wanaunga kutoka *TANESCO*.

Je, sababu gani za msingi zilizofanya *ZECO* kutoshusha bei ya umeme wakati huko *TANESCO* wanako nunua bei imeshushwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 kama ifuatavyo:-

Mhe. spika, ni kweli Shirika la Umeme *TANESCO* wameshusha bei ya umeme kuanzia tarehe 01 Aprili, 2016 kwa wastani wa asilimia mbili (2%). Hata hivyo, naomba ieleweke kwamba mnamo tarehe 01 Januari, 2014 *TANESCO* ilipandisha bei ya umeme kwa *ZECO* kwa wastani wa asilimia thalathini na nane (38%) ambapo kwa upande wa *ZECO* haikuweza kupandisha bei ya kuuzia umeme kwa wateja wake tokea wakati huo hadi sasa. Pamoja na punguzo hilo bei ya kuuzia umeme hapa Zanzibar ipo chini ikilinganishwa na Tanzania Bara, ambapo *ZECO* ina nunua umeme. Mtumiaji wa kawaida wa Zanzibar analipa Sh. 222 kwa *unit* wakati Tanzania Bara mtumiaji wa kawaida analipa TSZ 295 kwa *unit*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa kukiri kuwa gharama imeshuka sana Tanzania Bara, nakupongeza Mhe. Naibu Waziri na huu ndio ukweli, mtu haki yake mpe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa umeme kutoka Tanzania Bara gharama yake imekuwa kubwa na wanaoumia ni wananchi. Lini Serikali itasikiliza kilio hichi cha wananchi bila ya kutegemea umeme kutoka Tanzania Bara, umeme huo tunanunua *unit* moja shilingi ngapi kutoka Tanzania Bara? Hilo (a).

Mhe. Mwenyekiti, na (b) Serikali itakuwa tayari kupokea muwekezaji kwa sekta ya nishati ya kuzalisha umeme kwa kutumia umeme kwa mawimbi ya bahari ili wananchi wapate umeme huo kwa bei nafuu, mtakuwa kukuleteeni muwekezaji wa sekta ya umeme kwa kutumia umeme huu wa mawimbi ya bahari.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, naomba kumjibu Mwakilishi Jaku Hashim Ayoub, swala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe.Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nilisema kwamba mtumiaji wa umeme Zanzibar ananunuwa kwa *unit* moja ni shilingi 222, tofauti na wenzentu ambako sisi tunachukuwa umeme, wao wananunuwa shilingi 299 kwa *unit* moja. Bado tunapendelea unafuu wa watu wetu na ukiona hapo kwa nini hawa wa kwetu wanalipa bei hii ni jitihada ya Serikali kuhakikisha kwamba raia wake au watu wake wanapata unafuu zaidi inavyowezekana.

Sasa hao watu ambao watataka kuwezesha au kuja kufanya namna ya kupata umeme wa kwetu mbadala, mimi nikwambie kwamba wakaribishe, tuone ni namna gani, isije ikawa kwamba tunahisi huku kukawa kuna nafuu ikaja ikawa

ndio kikwazo zaidi. Lakini kama wapo basi tuwakaribishe na tuonane tutajuwa nini cha kufanya.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nataka muongozo wako wa kiti. Kanuni ya 37, nilichomuuliza Mhe. Naibu Waziri, *unit* moja kutoka Tanzania Bara nyie kama *ZECCO* mnanunuwa shilingi ngapi, sio wa kununuwa wananchi, kama nyie kutoka Tanzania Bara mnanunuwa *unit* moja shilingi ngapi, wananchi wanataka kufahamu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Jaku, Mwakilishi wa Jimbo la Paje suala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo. *Unit* moja kwa Zanzibar tunanunuwa shilingi 275 lakini sisi tuna-*subsidies* ndio tunauza shilingi 222.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi nina swala dogo la nyongeza. Katika suala la kawaida la kununua umeme kutoka *ZECO* wananchi huwa wanapewa *charged VAT,* wanaponunua *units* za shilingi 10 basi watalipa tozo ambayo inatakiwa ilipwe ya hiyo *VAT*. Lakini pia wawekezaji wanaponunua umeme huo huo wanalipa hiyo tozo hiyo ya *VAT* ambayo ni %18, lakini wao wanapata fursa ya mwisho wa mwezi kwenye *input* na *output* ya *returns* zao kuweza kurudisha na kuomba zile fedha waweze kurudishiwa.

(a) Swali, ni kwa nini wizara husika inayosimamiwa na taasisi ya *ZECO* haifikirii kuondosha hii tozo ya *VAT* kwa wananchi masikini wa kawaida ili waweze kupata unafuu wa hiyo %18.

(b) Pia, tunajua sisi sasa tunaelekea katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na matumizi ya wananchi yataongezeka, basi kwa nini serikali isifikirie kuondosha hiyo tozo ya *VAT* katika Mwezi Mtukufu huu wa Ramadhani ili ikawa ni kianzio kizuri na kuonesha kwamba wanawajali wananchi wao. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, suala la kuondoa *VAT* kwa ajili ya wananchi wetu. Kama nilivyosema mwanzo serikali imebeba jukumu la kupunguza gharama za umeme kwa mtumiaji. Lakini suala la kuondosha *VAT* ni suala la utaratibu wa serikali kwa sababu kodi mbali mbali zipo za serikali, lakini ninachotaka kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza hili sisi sasa hivi bado tunaendelea ku-*negotiate* na watu wa

TANESCO kuhusu suala la *VAT* kwa sababu ni muda mrefu na sisi tunatozwa *VAT* na kodi zote za serikali katika kununua umeme.

Tumejaribu kwa sababu sisi ni watumizi na tunatumia umeme ule kwa sababu ya kuuza kwa wananchi wetu na *VAT* inachukua asilimia kubwa asilimia 18 na wanatuletea hivyo hivyo. Bado tutaendelea ku-*negotiate* nao na ni juzi tu wizara yangu kupitia Shirika imekwenda kukaa na wenzake, lakini bado kwa sababu ya utaratibu wa mfumo wenyewe bado mambo hayajakaa sawa, lakini bidii na juhudi mbali mbali tunazichukua kuhakikisha kwamba hata sisi tunabeba mzigo mkubwa kama Shirika kwa sababu ya hizi kodi.

Swali la pili ambalo amelizungumza kwamba tunamuangaliaje mwananchi wa kawaida katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambapo matumizi yanaongezeka. Kama nilivyosema mwanzo serikali ina nia njema kwa wananchi wake ndio maana imekubali kubeba hizi gharama nyengine za ziada. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi umeme ambao tunauuza tunauza kwa bei rahisi sana, lakini serikali bado inaendelea kubeba mzigo kugharamia hizo gharama za ziada. Ahsante.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya swali la msingi la Mhe. Waziri, mimi nina swali dogo la nyongeza. Wizara haifikirii kuwapunguzia gharama zaidi wananchi kwa kuwawekea nguzo za umeme bure na wananchi hao kulipia umeme tu. Ukizingatia umeme ni muhimu katika maisha ya binadamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimwambie kwamba shirika linajitahidi kadri ya uwezo kuhakikisha kwamba huduma ya umeme inafika. Lakini tatizo ni kwamba inapojitokeza kijiji au mtu anahitaji umeme wa ghafla nje ya utaratibu wa *ZECO*, ndio lile jibu la jana kwamba lazima achangie, lakini lilifahamika vibaya. Sasa namna ya kubeba kwa utaratibu ni kwamba *ZECO* inapeleka nguzo na umeme katika kijiji husika mwananchi mwenyewe ndio anatia kwa utaratibu na vijiji vingi tumefanya hivyo na hata baada ya muda mfupi *Inshaallah* Fundo utafika umeme kwa misingi hiyo.

Nam. 21

***ZIPA* kuwa chini ya Wizara ya Fedha**

Mhe. Simai Mohammed Said - Aliuliza:-

Ni vipimo gani vinavyotumika kuifanyia *ZIPA* iwe chini ya Wizara ya Fedha wakati asilimia zaidi ya 80% ya Wawekezaji wapo chini ya Wizara ya Utalii.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Kifungu cha 53(a), Mamlaka ya kuanzisha au kufuta Afisi/Taasisi ya Serikali hapa Zanzibar yamo mikononi mwa Mhe. Rais. Wakati wa kuanzisha anaelekeza pia afisi au taasisi hiyo iwepo chini ya wizara gani. Lakini Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 44(1) katika utoaji wa hati ya majukumu kwa maana ya *instrument* hiyo kwa Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili au mawaziri majukumu ya kazi zao pia na hati hiyo ni mamlaka ya Mhe. Rais. Hivyo, ni muhimu kwa Waheshimiwa Wajumbe, kwanza tukaelewa msingi huu mkuu wa Kikatiba na kuepuka pia kuhoji utekelezaji wa mamlaka ya Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na *ZIPA* kuwa chini ya Wizara ya Fedha na Mipango badala ya wizara inayosimamia utalii, ni vigumu sana kumsemea Mhe. Rais juu ya vigezo alivotumia zaidi ya uwezo wake aliopewa Kikatiba. Hata hivyo, dhana ya kuwa *ZIPA* inapaswa kuwa chini ya wizara yoyote ile kwa sababu tu miradi mingi ya uwekezaji ipo chini ya wizara hiyo itakuwa haina mashiko stahiki.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu pia inawezekana kwamba leo miradi mingi tunaiona kwenye sekta moja, lakini kadri uchumi wetu unavyokua sekta nyengine zinaweza zikatokezea zikawa na miradi mingi zaidi kuliko sekta ya utalii. Lakini vile vile tukumbuke kwamba suala la *ZIPA* la uwekezaji ni suala mtambuka linagusa sekta nyingi; Uvuvi wa Bahari Kuu, uwekezaji kwenye viwanda ukiachilia mbali uwekezaji kwenye kilimo, uwekezaji kwenye mifugo. Kwa hivyo, hili ni suala mtambuka Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, jukumu kuu la *ZIPA* ni kushajiisha fedha kutoka sekta binafsi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu kupitia uwekezaji. Kwamba kwa sasa mafanikio yamepatikana zaidi katika Sekta ndogo ya Utalii haibadilishi jukumu la msingi la *ZIPA* la kusimamia maendeleo ya Sekta ya Utalii. Bado jukumu lake limebaki kuwa ni ushajiishaji na upatikanaji wa fedha kutoka kwa wawekezaji binafsi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Dhana ya kutafuta fedha (iwe za ndani au nje, kodi, mikopo au uwekezaji) ni la wizara inayosimamia fedha. Pamoja na kwamba imewahi kutokea huko nyuma *ZIPA* kuwa chini ya wizara inayosimamia utalii, tunaamini kuwa kwa sasa, wakati wa kuiweka *ZIPA* chini ya wizara inayosimamia masuala ya fedha Mhe.

Rais amezingatia upana wa majukumu ya taasisi hii ya *ZIPA*. Badala yake usimamizi wa maendeleo ya utalii unaosimamiwa na Kamisheni ya Utalii akauweka chini ya wizara inayosimamia utalii.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya kujitosheleza na ya kunifurahisha, lakini pia nina maswali ya nyongeza mawili.

(a) Katika mkakati uliotajwa na serikali *MKUZA* wametaja kwamba utalii, biashara na huduma, lakini pia serikali imekiri kwamba mapato wanayopata katika fedha za kigeni ni zaidi ya asilimia 80.

Je, Mhe. Waziri, haoni umuhimu wa kuwepo watu ambao katika Wizara yake ya Fedha na Mipango ambao wataweza kufanya kazi kwa ukaribu kabisa na hao wawekezaji ambao wapo nje katika utalii. Kwa sababu hisia iliyokuwepo ni kwamba baada ya wao kutoka *ZIPA* wameshapata leseni zao wanabakia hawajui wapi pa kwenda. Sasa mimi ningepata ushauri au majibu mazuri juu ya maelezo yangu pamoja na hilo swali nililouliza. Ikiwa *ZIPA* zamani ilikuwa chini ya utalii, biashara na uwekezaji...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, nenda kwenye swali moja kwa moja.

Mhe. Simai Mohammed Said: Swali langu ni kwamba Mhe. Waziri, haoni umuhimu wa kuwepo maafisa wanaohusika watakaoweza kuwa karibu na wawekezaj hususan katika eneo la utalii kwenye wizara yako.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba *ZIPA* iko chini ya Wizara ya Fedha na moja ya jukumu la msingi kabisa la *ZIPA* ni kusaidia katika masuala ya *coordination*, kuunganisha sekta, lakini vile vile kuunganisha wawekezaji, wizara kwa maana ya serikali na taasisi nyengine. Hilo ndio jukumu la msingi, ukiacha majukumu mengine ya kupokea maombi, ya kuchambua maombi, ya kutoa leseni, jukumu la msingi ni ku-*forge linkages*, kusaidia kuweka utaratibu mzuri wa kuunganisha taasisi mbali mbali za kusaidia uwekezaji katika nchi yetu.*(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi lakini ningekuomba kidogo hicho kiti chako ungekuwa unazungusha ili uangalie huku na huku. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na majibu ya Mhe. Waziri kwamba, mamlaka ya Rais si vyema kuhojiwa wala kuingiliwa, lakini pia nakubaliana na

majibu ya Mhe. Waziri kwamba, muundo wa taasisi mamlaka hayo yapo katika uwezo wa mwenyewe Mhe. Rais. Katika majibu yake Mhe Waziri amesema kwamba, si vyema kuhoji utekelezaji wa Mhe. Rais.

Swali langu ni kwamba, ni nini maana ya kuwa na Baraza kuisimamia serikali.

Pili, Mhe. Waziri, anazungumziaje suala la dhana nzima ya *checks and balance* katika mfumo wa vyombo vya dola.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, hapa tunazungumzia suala la katiba na katiba ni katiba ya nchi. Mhe. Rais, Makamu wa Pili, Mawaziri, Manaibu Mawaziri wote walioteuliwa na Mhe. Rais, tumekula kiapo kuilinda katiba iliyopo. Sasa katiba hii ndiyo iliyotoa mamlaka kwa Mhe. Rais ya kuanzisha taasisi au afisi, lakini pia na kuteuwa wale watakaoshikilia ofisi hizi na kuwapa majukumu yao. Sasa suala la kwamba kama mamlaka haya ya Rais tunayaona makubwa ni suala ambalo lina *process* yake refu kidogo ya kubadilisha hiyo katiba yenyewe. Lakini kwa sasa hivi hatuwezi kwenda kinyume na katiba ambayo sisi wenyewe tumeipitisha. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri, kwa umakini wake na pengine huko mbele anaweza akachukua nafasi kubwa kuliko hii aliyokuwanayo penye majaaliwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimeshukuru kuwa hii wizara iko kwake na najua haina mjadala, lakini vile vile nitakuwa sijatenda haki kama sijawashukuru watendaji wake hasa Wakurugenzi wa *ZIPA* kwa umakini wao na jitihada wanazozichukua kwa uwekezaji. Je, unatoa kauli gani lakini kwa baadhi ya taasisi nyengine kurudisha nyuma maendeleo ya wawekezaji hapa nchini.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, samahani sijasikia lile swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Waziri baada ya kumpongeza, nilikuwa nina swali dogo sana la nyongeza. Wizara yake, yaani *ZIPA* imekuwa ikifanya kazi kwa hali na mali, mvua, jua na wawekezaji wengi wanaokwenda pale hawapati matatizo. Lakini kuna baadhi ya taasisi zinarudisha nyuma maendeleo ya wawekezaji. Je, unatoa kauli gani ikiwa wewe ni Waziri wa Fedha wakati unahitaji mapato.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napokea pongezi ya kwamba taasisi yetu ya *ZIPA* inafanya kazi vizuri na kwa umakini. Vile vile, nimhakikishie kwamba taasisi nyengine zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha, lakini naamini pia na taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitafanya kazi kwa umakini na kwa umadhubuti kwa mujibu wa sheria na katiba. Suala hilo Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mawaziri, Manaibu Mawaziri na wote Makatibu Wakuu, watendaji wana majukumu maalum ya kusimamia masuala haya. Sasa Mwakilishi wala asiwe na wasiwasi taasisi zote zitafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa na mkazo mkubwa kuleta ufanisi katika nchi yetu.

Nam. 23

Kuanzishwa Mfuko Maalum wa Ununuzi wa Dawa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kwa kuwa bajeti ya matibabu ni muhimu sana kwa wananchi.
Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mfuko maalumu wa manunuzi ya dawa na kukaribisha wananchi wazalendo kusaidia Mfuko huo wakiwemo wafanyabiashara wa ndani na nje kama wanvyosaidia katika harakati nyengine mbali mbali.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kukabiliana na suala la ununuzi wa dawa Wizara imeanzisha akaunti na orodha maalum ya dawa (*Essential Medicine Account and Drug List*) ambapo mfadhili au mwananchi yeyote mwenye nia ya kuchangia katika ununuzi wa dawa anaweza kuingiza fedha katika akaunti hii iliyopo Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) akaunti namba 021103000679. Hivyo, napenda kuchukuwa fursa hii kuwaomba wananchi, wafanya biashara wa nje na wa ndani pamoja na Wajumbe wa Baraza hili wenye nia ya kuchangia ununuzi wa dawa watumie akaunti hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inatoa fursa ya kuandaa mkataba wa makubaliano ambao utahakikisha kwamba fedha zitakazochangiwa katika mfuko huo zinatumika kwa ajili ya manunuzi ya dawa tu na sio kwa matumizi mengine yoyote.

Hadi sasa kuna akaunti ya dawa ambayo tunaitumia pamoja na wafadhili mbali mbali na wahisani wa maendeleo. Ahsante.

Mhe. Jaku Hasim Ayoub:

(a) Mhe. Mwenyekiti, tangu kuanzia kwa akaunti hiyo kiasi gani cha fedha kimepatikana ili wananchi wa Zanzibar wapate kufahamu.

(b) Serikali imechukuwa hatua gani za kutangaza mpango huo kwa kuchangia kwa wananchi wa Zanzibar na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya:

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kiasi gani cha fedha siwezi kumjibu kwa ukamilifu kwa sababu ni fedha ambazo zinaingia na kutumika na hazikai kwenye akaunti, zinatumika kwa ajili ya manunuzi ya dawa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub, aniongeze kidogo swali la (b) sikulielewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, serikali imechukuwa hatua gani kwa kutangaza mpango huo kwa wananchi wa Zanzibar na wananchi wanaoishi nje ya nchi kuitangaza sera hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Serikali kupitia Wizara ya Afya imechukuwa hatua ya kutangaza kwa wahisani kwa wananchi walio ndani na nje ya nchi kuchangia akaunti hii kwa kuitangaza na kuitoa akaunti naomba hii ambayo nairudia 021103000679, tuna mpango wa kuitoa hata katika vyombo vya Habari ili wananchi walio ndani ya nchi na nje ya nchi waweze kuisikia na kuichangia.

Tunashukuru kwamba hadi sasa michango tunaipata kidogo. Lakini tunaomba mashirikiano yenu Waheshimiwa Wawakilishi, mliomo humu sasa hivi ili muhamasishe katika majimbo yetu waweze kuichangia zaidi akaunti hii pamoja na nyie tunahitaji michango yenu. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongze Mhe. Naibu Waziri, kwa kuweza kujibu maswali yake kwa ufanisi na ufasa zaidi.

Mhe. Naibu Waziri, je, wizara yako inamahitaji gani na mpango gani ili kuondosha tatizo la madawa kwenye vituo vya Afya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Samahani Mhe. Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa, arudie swali lake kidogo sikumsikia.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Je, wizara yako ina mpango gani na ina malengo gani ili kuondosha tatizo la madawa kwenye vituo vya Afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Wizara yangu ina mpango madhubuti wa kuondosha tatizo la mapungufu ya dawa katika vituo na hospitali vilivyopo Unguja na Pemba, sio Pemba tu. Mhe. Mwenyekiti, wizara imejipanga na mahitaji inayohitaji ni makubwa ili kuondosha kabisa tatizo hili.

Kwa hiyo, imejipanga kupunguza kwa asilimia kubwa kwa kupitia michango hii ambayo tumeitangaza ichangiwe na tunawaomba sana Waheshimiwa mchangie lakini kwa kupitia kuwahamasisha wafadhili mbali mbali wa ndani na nje ya nchi ili waweze kutuchangia na hatimae tuweze kumaliza tatizo hili.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa anajibu majibu wa ufasaha sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu umekiri kuwa kuna mfuko huu wa serikali au wa wizara ambao unaingia na kutoka pesa wa Wizara ya Afya. Lakini kutokana na sababu hizo hizo kwa kipindi sasa cha mwezi wote kutoka mwezi wa 5 mpaka mwezi huu wa 6 ulipofikia dawa za chanjo za watoto wanaozaliwa mwanzo mpaka sasa hazijapatikana hospitali zote pamoja na Hospitali ya Mpendae. Je, ni nini tamko la serikali juu ya chanjo hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, chanjo za watoto zipo na kama hazipo katika kituo chako inawezekana ni ucheleweshaji wa wahusika katika kituo cha afya hicho kwenda kuchukuwa katika sehemu inayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimthibitishe Mheshimiwa kwamba, karibuni tarehe imenitoka lakini mimi mwenyewe nilifungua uwekaji wa chanjo kwa watoto katika kituo cha Hospitali ya Jimbo la Mhe. Balozi Seif Ali Idd.

Kwa hiyo, chanjo zilitolewa na kuanzia hapo chanjo zilikuwa zinatolewa. Sasa kama kuna udhaifu kidogo wa upatikanaji wa chanjo, naomba tuwasiliane ili tuone kwamba ni tatizo gani ambalo limetokea katika kituo cha afya ambacho

umekisemea ili tuweze kuwasaidia. Lakini tunawahakikishia kwamba chanjo zipo.

Utaratibu

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nimeinuka kwa Kanuni ya 62, lakini vile vile nikilia mkazo Kanuni ya 37.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri, alipokuwa akinijibu yeye nadhani alifungua chanjo ya *Vitamin* 'A' ambayo ndiyo iliyokuwa ikifunguliwa na ndio ikitoka.

Nilichokuwa nikizungumza mimi hapa ni ile chanjo ya watoto wadogo wanaozaliwa siku moja mpaka miezi mitatu, chanjo hiyo hakuna na hakuna kwenye mahospitali mengi. Naomba tu Mhe. Naibu Waziri, nimtanabahishe hilo, lakini tuonane ili tuzungumze tuweze kuweka hali ya wananchi sawa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohamed Said Mohamed, kwa maelezo yako, yeye alitaka muonane, kwa hivyo, mtaonana ili muweze kuweka sawa.

Nam. 73

Matengenezo ya Barabara ya Msingini – Chachani

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Barabara ya Msingini – Chachani hadi Kilimatinde ni muhimu na imekua ikisaidia sana hasa wakati wa dharura, na Serikali kwa kipindi kirefu imeisahau barabara hiyo na hivi sasa ni mbovu na imechafuka kabisa.

a) Kwa nini barabara hiyo haijafanyiwa matengenezo ya aina yoyote kwa kipindi kirefu sasa.
b) Ni lini barabara hiyo itafanyiwa matengenezo na kuwafanya watumiaji wa barabara hiyo kufaidi matunda ya serikali yao tukufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake Nam. 73 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli barabara ya Msingini – Chachani hadi Kilimatinde ni muhimu na imekuwa ikisaidia sana hasa wakati wa mvua.

Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Msingini – Chachani iko katika Baraza la Mji la Chake-Chake chini ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.Hata hivyo, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji mara zote huwa inatoa mashirikiano makubwa na ushauri pale Wizara husika zinapokuwa na shughuli zake za kazi katika kuhakikisha barabara hizo zinapitika vizuri na muda wote.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme anaielewa vizuri barabara ya Msingini, ni kweli barabara ya Msingi inaweza kuingia katika Serikali za Mitaa. Lakini barabara hii kwa asili yake ni barabara iliyojengwa toka enzi za Ukoloni ambayo ina mikiki mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, barabara hii si ya kutia kifusi, barabara hii ina msingi kuanzia mwanzo mpaka mwisho kiasi inakaribia nusu kilomita au kilomita moja ina daraja, ina milima sifikirii kama Serikali za Mitaa inaweza ikaijenga barabara hii iliyoko katikati ya mji. Mji namba mbili kwa Zanzibar ambao una haiba zake...

Mhe. Mwenyekiti: Mweshimiwa, uliza swali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said:

(a) Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba kwa Mhe. Naibu wa Ujenzi, atasaidia kiasi gani kusaidia Serikali za Mitaa kumaliza kadhia hii ya mji ule.

(b) Ni lini barabara hii itajengwa kwa sababu imekuwa kama wimbo wa taifa na iko katikati ya mji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, nataka kwanza nimtoe shaka kwamba hizi barabara zilioko katika Halmashauri wao si kwamba wanajenga moja kwa moja. Wao kupitia mfuko wa barabara wametengewa fungu lao maalum kama tulivyotengewa sisi Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Jambo linalofanyika hapa ni kwamba kama unavyofanyika sasa hivi ujenzi unaoendelea wa barabara katika jimbo langu la Malindi barabara inayopita Miti Ulaya wametangaza Zabuni na baadae ikampa mzabuni ambaye ni *MECO* ndie

alietengeneza barabara ile pamoja na barabara ya Mhe. Nassor Salum Jazira wa jimbo la Kikwajuni.

Utaratibu ule tunaotumia kujenga barabara hizi ndio utaratibu tutakaotumia kujenga barabara yako na nakupa ahadi kwamba ni jana tu wamekaa watu wa mfuko wa barabara, watu wa Idara yetu wa barabara ya utengenezaji *UUB* na Halmashauri. Nataka kuahidi tu kwamba karibuni tu baada ya kumaliza bajeti wataanza maandalizi ya kutangaza zabuni pamoja na barabara yako nyengine inayoitwa *Qatar* nafahamu pia unaijua.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Naibu Waziri, roho ya Pemba iko Ndagoni ni kutokana na umeme uliotoka Tanga, mpaka hivi sasa Ndagoni hakuna barabara tangu ilipoumbwa dunia. Walinzi wetu wanaolinda umeme ndani ya mwaka 2013 walikuwa wakipita baharini kule wakazama na hivi sasa barabara ile imetiwa fusi lakini kwa mvua zile zilizopita imechimbuka.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mpango gani wa kuitengeza barabara ya Ndagoni ili kuwaondoshea usumbufu wananchi wa Shehia ya Ndagoni na walinzi wetu wanaokwenda kulinda umeme.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ile barabara ya Ndagoni ni kweli, ni barabara mimi nimepita wa sababu gari zinapita mpaka kwenda chini kule kulikuwa na mabwawa. Isipokuwa tu nataka kumwambia kwamba tuna kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba barabara zote hizi hata zile zilizokueko kwenye Halimashauri tunataka kuzitengeneza ili wananchi wazipitie kirahisi na bila ya tatizo lolote.

Namuhakikishia kwamba tutakwenda kuiangalia barabara hiyo tena na iwapo uwezekano wa kuifanyia marekebisho katika zile sehemu korofi tutazifanyia. Lakini nataka kumwambia tu ilani yetu ya uchaguzi ya 2015 mpaka 2020 inafahamu fika kwamba kuna matatizo ya barabara ndio maana ikatoa kipaumbele katika kuzijenga barabara hizo kwa lami na njia za kifusi na nyengine changarawe. (*Makofi*)

Mhe. Abdalla Maulidi Diwani: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa pongezi kwamba serikali yetu sikivu katika siku niliopita niliuliza barabara juu ya uondoshaji wa vumbi katika barabara ya Mwanakwerekwe - Fuoni lile suala limefanyika na sasa hivi inamwagiwa maji, nashukuru sana kwa usikivu wake Mhe. Naibu Waziri.

Kutokana na kucheleweshwa kumalizika barabara ile na tayari inasadikika kwamba miundombinu ya umeme na maji ndio kikwazo cha kumalizika barabara ile, sijui serikali inatwambia nini au kuna tatizo gani baina ya miundombinu na maji mpaka dakika hizi kushindwa kuondoa miundombinu yao ya maji na barabara ile ili kuweza kuendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli barabara ile tumeitanua na kwa hiyo, miundombinu ya maji imeathirika na vile vile taa za barabarani. Tumeshakaa sisi kamati yetu pamoja na Wizara ya Ardhi kuhakikisha kwamba ile miundombinu tunaiondoa kwa haraka na tunashukuru sana Wizara ya Fedha imeshatenga pesa kwa ajili ya kuondosha ile miundombinu na kuhakikisha kwamba inawekwa mingine kwa haraka ili barabara ile baadae tuendelee na utaratibu na tuhakikishe kwamba tunaimaliza ndani ya kipindi chake ambacho ni Disemba 2016.

Namtoa shaka kwamba karibuni tutatangaza zabuni au tenda ili kumpata mkandarasi sasa hivi wa kutia lami na nina imani mkandarasi huyo atafanya kazi kwa haraka ili kuwaondolea wananchi kero ambazo na sisi pia zinatuumiza, tukisikia kila siku katika mawio au vyombo vya habari kwamba wanaathirika sana na barabara ile. Ahsante.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (0R) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha hotuba yangu naomba niwaombe Waheshimiwa Wajumbe watakaotaka kuchangia watakapokuwa wanafuatilia michango yao, taarifa zote zipo katika vitabu viwili.

Kitabu cha kwanza kinaeleza mambo ya jumla na kitabu cha pili kinazungumzia shughuli za Serikali za Mitaa. Kwa hivyo, wanaweza wakenda kwenye vitabu vyote viwili ili kupata *reference* ya kile ambacho kimezungumzwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya

Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo katika Baraza hili Tukufu tukiwa salama katika hali ya amani na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, naomba kutumia nafasi hii kupitia Baraza lako Tukufu kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Zanzibar kwa miaka mitano ijayo. Aidha, nampongeza kwa uadilifu na uongozi wake wenye busara na hekima ambao umemuwezesha kuchaguliwa tena kwa kishindo na kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani na utulivu ambayo itaendelea kuchochea kasi ya maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.Uongozi wake imara na makini umeiwezesha Serikali kutekeleza kwa kiwango kikubwa Sera ya Chama Tawala cha CCM kama zilizovyoainishwa katika Ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2010 hadi 2015 na kuonyesha muelekeo wa kuifikia Dira ya Maendeleo ya mwaka 2020. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa tena kuendelea na nafasi ya Makamo wa Pili wa Rais ili kumshauri Mheshimiwa Rais wa Zanzibar. Kuteuliwa kwake kumetokana na hekima na uadilifu wake katika kumshauri na kumsaidia kwa karibu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuteuliwa kwake kumetokana na hekma na uadilifu wake katika kumshauri na kumsaidia kwa karibu Mhe. Rais wa Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli na Makamo wake Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuchaguliwa kwao kuiongoza nchi yetu. Aidha, nampongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu. Nawaombea Mwenyezi Mungu awape nguvu waweze kukutumikia Watanzania wote.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii adhimu kukupongeza wewe binafsi Mhe. Spika na Mhe. Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwenu

kuliongoza Baraza lako Tukufu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Naomba niwapongeze Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi kwa kuchaguliwa kwenu pamoja na viongozi wengine mbali mbali wa Baraza katika kipindi hiki cha miaka mitano. Nawaombea wote Mungu awajaalie uwezo na uongozi mahiri, wenye hekima, busara na uadilifu wa kutimiza majukumu yenu hapa Barazani. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba vile vile kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza waliochaguliwa na wakuteuliwa kwa kupata fursa hii adhimu ya kuwatumikia wananchi. Aidha, naomba niwapongeze Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa na kuwa wasaidizi wa Mhe. Rais katika kuziongoza Wizara za Serikali. Namuomba Mwenyezi Mungu atupe uwezo, busara na uadilifu ili tuweze kuendesha vyema shughuli za Serikali katika dhamana tulizopewa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuipongeza Kamati mpya ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya uwenyekiti wake Mhe. Machano Othman Said, ambayo tumeanza nayo kazi hivi karibuni ambapo miongozo yao ya awali imetupa matumaini ya kuisaidia Ofisi yangu katika siku zinazofuata.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tumbatu kwa imani waliyonipa ya kunichagua kwa mara nyengine tena kuwa Mwakilishi wao. Naamini imani yao kwangu ni deni ambalo siku zote nitakuwa namuomba Mwenyezi Mungu aniongoze katika kutimiza matarajio yao. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa wananchi wote waliopata maafa katika kipindi cha mvua za masika na kusababisha baadhi ya familia kukosa makaazi baada ya maji kuvamia nyumba zao. Pia, nawapa pole waathirika wa matukio yote yaliyojitokeza katika kipindi hiki yakiwemo maradhi ya Kipindupindu. Nawahakikishia kwamba Ofisi yangu iko pamoja nao katika kipindi hiki kigumu. Naomba pia kupitia Baraza lako tukufu kuwashukuru wale wote waliojitolea kwa hali na mali kuungana na Serikali katika kukabiliana na maradhi ya Kipindupindu na mafuriko yaliyotokea wakati wa mvua kubwa za masika. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, aidha, natumia nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wote wa Zanzibar kwa kudumusha amani na utulivu hasa katika kipindi chote cha uchaguzi. Utulivu na uzalendo wao umewezesha

kuendelea kuimarika kwa shughuli zote za kiuchumi na kijamii nchini mwetu. (*Makofi*)

MAJUKUMU MAKUU YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ yamefafanuliwa katika ***Kiambatanisho Namba 1***.

Mhe. Mwenyekiti, kimuundo Ofisi imegawika katika kuu tatu kama zinavyoonekana katika ***Kiambatanisho Namba 2.***

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi naomba sasa nichukue nafasi hii kutoa maelezo juu ya mapato, matumizi na utekelezaji wa programu kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2015/2016.

MUUNDO WA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR.

Mhe. Mwenyekiti, kimuundo Ofisi imegawika katika sehemu kuu 3 ambazo ni; Taasisi za Ofisi Kuu ambapo pia ina Ofisi inayojitegemea ya Ofisi ya Usajili, Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho; Mamlaka za Mikoa na Serikali za Mitaa; na Idara Maalum za SMZ. Mchanganuo wa Ofisi kimuundo ***Angalia Kiambatanisho Namba 2.***

Mhe. Mwenyekiti, Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nichukue nafasi hii nitoe maelezo juu ya mapato, matumizi na utekelezaji wa programu kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakusanya mapato ya Serikali Kuu yanayoingia mfuko mkuu wa Serikali na mapato ya Serikali za Mitaa

ambayo hutumiwa na Serikali hizo. Kwa upande wa mapato ya Serikali Kuu, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 195,586,000/= kupitia vianzio mbali mbali na hadi kufikia mwezi Machi 2016, Shilingi 75,539,000/= zimekusanywa sawa na asilimia 39 ya lengo la mwaka. ***(Tafadhali angalia Kiambatisho Namba 3).*** Kwa upande wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2015/16 zilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi 7,227,861,000/= na hadi kufikia Machi 2016, zimekusanywa jumla ya Shilingi 4,114,533,657/ = sawa na asilimia 56 ya makadirio ya mwaka ***(Angalia Kiambatisho Namba 4a na 4b).*** *Na Makadirio kwa Mamlaka hizo* ***(Angalia kimabatanisho namba 4(c))***

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi inasimamia mafungu 12 ya kibajeti na kwa mwaka wa fedha 2015/2016, mafungu hayo yalitengewa jumla ya Shilingi 66,772,700,000/= kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya hizo Shilingi 56,072,700,000/= ni kwa ajili ya mishahara, ruzuku ya Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji na matumizi mengineyo. Shilingi 10,700,000,000/= zilitengwa kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2016, mafungu hayo yameingiziwa jumla ya Shilingi 48,449,021,574/= sawa na asilimia 73 ya lengo la mwaka. Kati ya hizo Shilingi 43,984,816,574/= sawa na asilimia 65 ya lengo la mwaka ni kwa ajili ya kazi za kawaida na Shilingi 4,464,205,000/= sawa na asilimia 42 ya lengo la mwaka ni kwa kazi za maendeleo. ***(Angalia Kiambatisho Namba 5).***

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo ambayo imeunganishwa na Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Kwa mwaka wa fedha 2015/16 programu ya Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo imeidhinishiwa jumla ya shilingi 501,641,600/=. Kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo.Hadi kufikia Machi Ofisi imeingiziwa jumla ya Shilingi 276,157,275/= sawa na asilimia 55. Ofisi pia, ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 245,000,000/= ikiwa ni mapato ya Serikali. Hadi kufikia Machi imekusanya jumla ya shilingi 109,241,500/= sawa na asilimia 45 ya makadirio.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imetekeleza majukumu yake kupitia Programu kubwa 28 na programu ndogo 7.

TAASISI ZA OFISI KUU (D01)

Programu kuu nne (4) zinazotekelezwa na Taasisi za Ofisi Kuu ni kama zifuatazo;

1) Programu ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
2) Programu ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ;
3) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Utumishi katika Idara Maalum na;
4) Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ina jukumu la kutoa na kusimamia huduma za Uendeshaji na Utumishi katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, zikiwemo kusimamia Sheria na Kanuni zinazosimamia utumishi na uendeshaji wa Ofisi, kwa kuwaendeleza wafanyakazi kielimu pamoja na kusimamia upatikanaji wa vitendea kazi na pia kuendelea kusimamia utunzaji kumbukumbu.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa fedha 2015/2016, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilitekeleza programu ya Usimamizi wa Shughuli za Utumishi na Utawala, ambapo programu ilijipangia kutoa huduma mbili nazo ni; Huduma za kiutumishi na utawala na Huduma ya ukaguzi wa hesabu za Ndani. Katika kutekeleza huduma hizo imenunua vitendea kazi na kulipia huduma nyingine za lazima. Idara imeratibu vikao vitatu vya Kamati ya Uongozi. Kitengo cha Manunuzi kimefanya vikao vinane vya Bodi ya Zabuni kwa ajili ya matumizi mbali mbali. Aidha, Idara imeratibu vikao vitatu vya kamati ya ukaguzi ambapo ripoti za vipindi vitatu zimeshawasilishwa katika kamati ya Ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 1,219,546,000/= na kwa kipindi cha miezi tisa ilikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 978,456,500/= kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi Machi 2016, Idara iliingiziwa jumla ya Shilingi 630,713,513/= sawa na asilimia 64.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la kupanga, kuratibu na kusimamia Sera, Mipango na Programu za Ofisi na kufanya kazi kwa mujibu wa maelekezo ya mipango ya Kitaifa ikiwemo Dira ya 2020, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Sera na MKUZA. Aidha, inatoa huduma za uandaaji wa mipango ya maendeleo, bajeti, ufuatiliaji na tathmini wa programu na miradi, kusimamia uandaaji na mapitio ya sera, sheria, pamoja na tafiti.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Idara inatekeleza Programu ya Uratibu wa Kazi za Mipango, Sera na Utafiti, chini ya programu hiyo, Idara inatekeleza huduma ndogo mbili ambazo ni; Kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mipango ya Ofisi na huduma ya uwekaji wa kamera za ulinzi (*CCTV*) katika maeneo ya Mji Mkongwe, bandarini na uwanja wa ndege na baadhi ya njia kuu za maeneo ya Wilaya ya Mjini kupitia Mradi wa Mji Salama.

Mhe.Mwenyekiti, katika kutoa huduma ndogo ya kwanza Idara iliandaa maandiko matano ya miradi kati ya maandiko hayo miradi mitatu imekubaliwa kupatiwa fedha za utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha, Miradi ya maendeleo 35 imefanyiwa ufuatiliaji na ukaguzi angalia ***Kiambatanisho Namba 6.***

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza huduma ndogo ya pili ya uwekaji wa kamera na vifaa vya ulinzi, kazi mbali mbali zimeanza kutekelezwa, ikiwemo uwekaji wa nguzo na ufungaji wa kamera za ulinzi katika maeneo ya mji wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya Serikali kuamua usimamizi na ukarabati wa barabara za ndani mijini na vijijini ufanywe na Mamlaka za SerikaIi za Mitaa, katika mwaka 2015/2016, Ofisi imefanya matengenezo ya barabara ya Muembekisonge kwa gharama ya Shilingi 101,016,850/=. Aidha, matengenezo ya barabara za Kikwajuni, Mitiulaya, na Kilimani zenye urefu wa kilomita 1.23 yanaendelea kwa gharama ya shillingi 585,646,055.88/=. Pia, matengenezo ya barabara itokayo Chake Chake Hospitali-Barabara ya Tibirinzi Pemba na barabara ya Misufini - Kwabiziredi Unguja yataanza hivi karibuni. Barabara za ndani za vijijini 30 zenye urefu wa kilomita 134.69 zimefanyiwa tathmini (75.9*km* Unguja na 58.7*km* Pemba). ***Angalia Kiambatanisho Namba 7.***

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 295,511,000/= kwa kutekeleza huduma ndogo ya kwanza na kwa kipindi cha miezi tisa ilikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 238,762,000/= ikiwa ni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi Machi 2016, iliingiziwa jumla ya Shilingi 97,352,300/= sawa na asilimia 41.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, katika kutekeleza huduma ndogo ya pili ya uwekaji wa Kamera za Ulinzi (*CCTV*) na vifaa vya ulinzi, Idara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 10,000,000,000/=. Hadi kufikia Machi 2016 Idara imeingiziwa jumla ya Shilingi 4,124,205,000/= sawa na asilimia 41.

OFISI YA AFISA MDHAMINI – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Afisa Mdhamini ni kiungo kati ya taasisi za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ zilizopo Pemba ikiwa na jukumu la kuratibu na kusimamia kazi zote za Ofisi kwa upande wa Pemba.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi imetekeleza programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Pemba. Kupitia programu hii, Ofisi inatoa huduma za kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Ofisi kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi imefanya ukaguzi katika miradi ya Mabaraza ya Miji Pemba na miradi midogo midogo inayotekelezwa na Halmashauri za Wilaya. Miradi ya Mabaraza ya Miji inayofadhiliwa na Benki ya Dunia chini ya *ZUSP* ambapo hadi sasa miradi hii inaendelea vizuri na iko hatua za mwisho kukamilika.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa masuala mtambuka, Ofisi kuu Pemba, imeendesha semina kwa watendaji wa Wizara juu ya mapambano ya UKIMWI, dawa za kulevya, mazingira na masuala ya jinsia na idadi ya watu. Aidha, Ofisi imeendesha mafunzo ya siku moja kwa Masheha wa Mkoa wa Kusini Pemba na wananchi juu ya maambukizi ya *VVU* na UKIMWI, huduma zinazotolewa na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi pamoja na Masuala ya Mazingira. Aidha, Ofisi imefanikisha upatikanaji wa vifaa vya Ofisi na kulipia huduma muhimu za uendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Ofisi iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 542,557,000 na kwa kipindi cha miezi tisa ilikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 388,646,000/= kwa matumizi ya kawaida. Hadi Machi 2016, iliingiziwa jumla ya Shilingi 355,084,500/= sawa na asilimia 91.

IDARA YA URATIBU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetekeleza programu ya uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambapo programu hiyo imegawika katika programu ndogo mbili; nazo ni Uratibu wa Tawala za Mikoa na Uratibu wa Serikali za Mitaa. Idara hii ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kutoa miongozo kwa Taasisi za Mamlaka ya Mikoa na Serikali za Mitaa. Katika kufanikisha majukumu yake, inasimamia utekelezaji wa maagizo ya mipango mikuu ya Serikali, Sera za Serikali na kusimamia utekelezaji wa Sheria Nam. saba (7) ya Serikali za Mitaa ya 2014 na Sheria Nam. nane (8) ya Tawala za Mikoa ya 2014.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, kwa Mwaka wa fedha 2015/2016 Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilijipangia kutoa huduma mbili kuu nazo ni kuratibu na kusimamia Mamlaka ya Mikoa na Wilaya; na huduma ya pili ni kuwapatia wananchi elimu ya Utawala wa Kidemokrasia na ugatuzi wa madaraka katika kuimarisha mfumo wa mageuzi ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imeratibu mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani na watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mikoa na Wilaya ambao ndio wasimamizi wakuu wa shughuli za Serikali za Mitaa. Aidha, rasimu ya Kanuni ya Sheria mpya ya Serikali za Mitaa imejadiliwa na kufikishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa mapitio ya mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha elimu ya watumishi wa Serikali za Mitaa, Idara kwa kushirikiana na uongozi wa Chuo cha Serikali za Mitaa kilichopo Hombolo - Dodoma kimekubali kuandaa mafunzo katika fani mbali mbali za uendeshaji na usimamizi wa fedha katika Serikali za Mitaa. Mafunzo hayo yatakuwa yanatolewa kutegemeana na haja ya Sekta husika.

Mhe.Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 2,340,703,000/= kati ya fedha hizo Shilingi 840,703,000/= ni kwa ajili ya kazi

za kawaida za Idara na Shilingi 1,500,000,000 ikiwa ni ruzuku kwa Baraza la Manispaa. Kwa kipindi cha miezi tisa Idara ilikadiria kutumia Shilingi 1,823,063,970/=. Hadi kufikia Machi 2016, Idara iliingiziwa jumla ya Shilingi 1,786,241,300/= sawa na asilimia 98.

IDARA YA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Mwenyekiti, Idara inatekeleza Programu ya Uratibu wa Idara Maalum za SMZ, kupitia programu hii Idara inaratibu utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za Idara Maalum na kusimamia vikao vya Mahakama ya Rufaa vya Idara Maalum za SMZ. Aidha, Idara ina jukumu la kusimamia mwenendo wa kiutumishi, maslahi ya maafisa na wapiganaji na kuwajengea uwezo wa kiutendaji na kuratibu masuala ya michezo ya pamoja kati ya SMZ na SMT.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016.

Mhe.Mwenyekiti, Idara imefanya kikao kimoja cha Mahakama ya Rufaa na kusikiliza na kutolea hukumu mashauri mawili ya rufaa. Idara iliendelea na hatua za kuanzisha Wakala wa Ulinzi wa JKU ambapo baada ya kupitishwa kwa sheria husika, Rasimu ya awali ya kanuni ya sheria hiyo imekamilika kwa kufikishwa katika vikao stahiki kwa hatua zinazofuata. Mkufunzi kwa kazi hizi amepatikana na vijana 50 wametayarishwa kwa kupatiwa mafunzo ambapo vijana hao watakuwa walimu wa kutoa mafunzo kwa wengine watakaochaguliwa kutekeleza huduma hiyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Idara ya Uratibu wa Idara Maalum iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 53,883,000/=. Kwa kipindi cha miezi tisa ilikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 44,854,000/= ikiwa ni kwa matumizi ya kawaida na hadi Machi 2016, iliingiziwa Shilingi 3,595,000/= sawa na asilimia 8.

TUME YA UTUMISHI YA IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ inatekeleza Programu ya Usimamizi wa Utumishi katika Idara Maalum. Tume ina jukumu la kusimamia shughuli za utumishi na maslahi ya maafisa na wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ. Malengo makuu ya Tume ya Utumishi ni kuhakikisha misingi ya Utumishi na Utawala bora inazingatiwa na Idara hizo.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ iliendelea kuimarisha misingi ya utawala bora katika Idara Maalum na kusimamia utekelezaji wa miundo ya utumishi *(Scheme of Service).* Tume imetoa mafunzo ya sheria zinazoongoza Idara Maalum pamoja na Sheria ya Utumishi wa umma namba 2 ya mwaka 2011 kwa wapiganaji wapatao 1200.

Mhe. Mwenyekiti, katika kusimamia utumishi wa Idara Maalum, Tume imefanya vikao 5 vya kawaida vilivyojadili utendaji kazi wa Idara Maalum za SMZ ambapo miongozo ya kiutumishi imetolewa, katika vikao hivyo Maofisa 6 wameongezewa muda wa Utumishi na 4 wamepewa mikataba ya Utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Tume ya Utumishi Idara Maalum iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 138,000,000/= na kwa kipindi cha miezi tisa ilikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 122,112,500/= ikiwa ni kwa matumizi ya kawaida na hadi Machi 2016, iliingiziwa jumla ya Shilingi 7,040,000/= sawa na asilimia 6.

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU) – (D02)

Mhe. Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) lina jukumu la kutoa mafunzo kwa vijana katika nyanja za uzalishaji wa kilimo, mifugo na uvuvi. Vile vile, kuwafunza vijana ufundi, kazi za amali na uzalendo ili kuwafanya vijana hao waweze kujitegemea na kuwa raia wema wa nchi yao.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 lilitekeleza Programu Kuu mbili (2); Programu ya Mafunzo ya Amali, Uzalishaji, Uzalendo na Michezo kwa Vijana, na Programu ya Ulinzi, Mipango na Uendeshaji wa JKU. Jeshi la kujenga Uchumi limesajili vijana 1,550 na kuwapatia mafunzo ya uzalendo na uzalishaji wa kilimo na mifugo, 104 katika michezo mbali mbali, 710 kwa mafunzo ya ufundi na 520 kwa elimu ya sekondari.

Mhe. Mwenyekiti, Jeshi la Kujenga Uchumi limeweza kuwajengea uwezo wa kitaaluma maofisa na wapiganaji 12 katika fani na ngazi mbali mbali, kuwapatia mafunzo ya kijeshi maofisa na wapiganaji 491 na kufanya vikao

viwili vya kamati ya Mashirikiano kati ya JKU na JKT ili kuimarisha ushirikiano.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Jeshi la Kujenga Uchumi liliidhinishiwa jumla ya Shilingi 10,804,500,000/= na kwa kipindi cha miezi tisa limekadiria kutumia kiasi cha Shilingi 9,190,234,726/= ikiwa ni kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi Machi 2016, liliingiziwa jumla ya Shilingi 9,166,346,726/= sawa na asilimia 99.7.

CHUO CHA MAFUNZO (MF) (D03)

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Chuo cha Mafunzo ina jukumu la kuwapokea wale wote wanaopelekwa Chuo cha Mafunzo kwa mujibu wa sheria. Kuwalinda na kuwarekebisha ili wanaporejea katika jamii wawe raia wema waliorekebishika. Urekebishaji unajumuisha mafunzo katika fani za ujenzi, kilimo, ushoni, ufundi magari, useremala, ujasiriamali pamoja na huduma za ushauri nasaha.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu ya huduma za Urekebishaji Wanafunzi, Chuo kimeandaa mpango wa urekebishaji wanafunzi ambapo pia huduma za ushauri nasaha zimeanza kutolewa. Aidha wanafunzi 290 wamepatiwa elimu ya watu wazima, mafunzo ya lugha na mafunzo ya amali.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Uongozi na Utawala wa Chuo cha Mafunzo imetekelezwa kwa kufanya vikao viwili vya kamati tendaji na ziara 8 ambazo zimejumuisha viongozi wakuu na watendaji kwa kambi za Unguja na Pemba. Pia imekamilisha ujenzi wa bweni kwa hatua ya kuezeka na kukarabati nyumba mbili za walimu. Idara pia imepanda miti 6,000 ya mivinje na miarubaini eneo la Hanyegwa mchana.

Mhe. Mwenyekiti, idara hadi kufikia mwezi Machi 2016, imeweza kushona jumla ya sare 425 kwa wanafunzi, na sare 1,100, kofia 300, na viatu pea 250 kwa maafisa na wapiganaji Unguja na Pemba. Aidha ekari 110 za mazao mbali mbali zimelimwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Idara imeidhinishiwa kiasi cha Shilingi 7,975,300,000/= na kwa kipindi cha miezi tisa imejipangia kutumia kiasi cha Shilingi 6,001,267,819/=. Hadi kufikia mwezi wa Machi imeingiziwa jumla ya Shilingi 6,811,080,140/= sawa na asilimia 113.

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) – D04

Mhe. Mwenyekiti, kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kina majukumu ya kulinda usalama wa bahari ya Zanzibar, kuzuia njia zote zinazoweza kutumika kupitisha magendo, kusaidia usalama wa baharini ikiwemo abiria, mizigo na watumiaji wengine wa bahari pamoja na uokozi baharini na kuongoza misafara ya viongozi katika shughuli maalum wanapotumia usafiri wa bahari.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimetekeleza Programu ya Usimamizi na Uzuiaji wa Magendo na Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Huduma za KMKM. Kupitia Programu ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo, Kikosi kimekamata magendo ya karafuu kavu kilo 1,725, Makonyo kilo 1,875 na Sukari kilo 500 ambazo zina thamani ya shilingi 627,523,200/=.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi kimefanya ukarabati wa majengo ya kambi za Kibweni Makao Makuu na kujenga mtaro wa kupitisha maji ya mvua. Aidha Kikosi kimejenga ukuta kwa ajili ya kuzuia mmong'onyoko eneo la ufukwe, kukarabati majengo Kambi ya Kama, na umaliziaji wa ujenzi wa nyumba ya Kamanda wa KMKM Wete Pemba. Kikosi kimekamilisha ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uzamiaji na Uokozi Kibweni KMKM na kuanza kwa ujenzi wa Kituo kama hicho Mkoani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, katika Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Huduma za KMKM, Kikosi kimenunua vifaa kamilifu vya uzamiaji kwa wazamiaji 28. Aidha vifaa mbali mbali vya mawasiliano vimenunuliwa kwa gharama ya Shilingi 257,815,000/=. Kikosi pia kimeendelea kuboresha huduma zinazotolewa kwa wagonjwa wanaofika katika hospitali ya Kikosi.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi kimewapatia wapiganaji wake 28 mafunzo ya Uzamiaji na Uokozi kutoka kwa wataalamu wa Kampuni ya L&W ya Uingereza. Sambamba na hilo Kikosi kimeanza kutoa mafunzo kwa wahusika wa maeneo ya vituo vya Uokozi vinavyoendelea kujengwa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Kikosi kimeidhinishiwa kiasi cha Shilingi 12,953,000,000/= kwa kazi za kawaida na kwa kipindi cha miezi tisa kilikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 10,787,975,040/=. Hadi kufikia mwezi Machi 2016 kimeingiziwa Shilingi 10,687,975,040/= sawa na asilimia

99 ya makadirio. Aidha, Kikosi kiliidhinishiwa Shilingi 700,000,000/= kwa kazi za maendeleo na kwa kipindi cha miezi tisa kilikadiria kupata shilingi 440,000,000/=. Hadi kufikia Machi 2016 Kikosi kimeingiziwa Shilingi 340,000,000/= sawa na asilimia 77.

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU) – (D05)

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kina majukumu ya kusimamia shughuli zote za uzimaji moto na uokozi wa maisha na mali za watu wakati wa majanga. Kikosi pia kinasimamia huduma za Zimamoto kwenye viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba. Vile vile, Kikosi kinatoa huduma za kibinaadamu, ushauri na mafunzo ya kujikinga na moto kwa wananchi, taasisi za Serikali na za watu binafsi pamoja na vyombo vya usafiri baharini na nchi kavu.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kilitekeleza kazi zake katika programu kuu mbili za utoaji wa huduma za Zimamoto na Uokozi, na Kukuza Huduma za Kiutawala na Uongozi kwa wafanyakazi wa Kikosi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi 2016 chini ya programu ya utoaji wa huduma za zimamoto na uokozi, jumla ya matukio 482 yameripotiwa katika vituo vya Zimamoto na Uokozi Unguja na Pemba ambapo matukio 165 yameweza kupatiwa huduma kwa wakati na matukio yaliyobakia yalishindwa kufikiwa kutokana na sababu mbali mbali .Matukio haya yote yamesababisha vifo vya watu 17 na hasara inayokadiriwa kufikia Shilingi bilioni 3.1. Inakadiriwa pia Shilingi bilioni 7.2 zimeokolewa wakati wa kukabiliana na matukio ya ajali hizo na kuokoa maisha ya watu 32 na wanyama 56. ***Angalia kiambatanisho namba 8.***

Mhe. Mwenyekiti, katika programu ya kukuza huduma za kiutawala, mafunzo, uwajibikaji na ushirikiano kwa wafanyakazi wa Kikosi cha Zimamoto. Kikosi kimetoa mafunzo kwa wapiganaji 20 katika fani na ngazi tofauti ndani na nje ya nchi. Aidha kikosi kimewapa mafunzo wafanyakazi 111 katika ngazi ya uongozi mdogo na uongozi mkubwa. Vilevile Kikosi kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Ujerumani kimewapatia wapiganaji 90 mafunzo ya uokozi.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi kimeendelea kutoa elimu ya kujikinga na majanga ya moto kwa jamii kwa kurusha vipindi 12 kwa njia ya redio na vipindi vinne kwa

njia ya televisheni. Aidha kikosi kimetoa mafunzo kwa taasisi 45 za Serikali na 75 za watu binafsi juu ya kuchukua hadhari ya kinga dhidi ya moto.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi kimeshiriki vikao viwili vya Jumuiya ya Afrika Mashariki juu ya masuala ya majanga na usalama. Aidha kimepatiwa msaada wa magari matatu, moja kwa ajili ya kubebea wagonjwa, moja la kuzimia moto na moja la usafiri kutoka Serikali ya Japan. Pia kikosi kimepokea vifaa mbali mbali vya kuzimia moto vyenye thamani ya Shilingi 858,550,000/= kutoka jiji la Hamburg Ujerumani.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kiliidhinishiwa kutumia Shilingi 4,313,300,000/= na kwa kipindi cha miezi tisa kilikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 3,224,848,665/= kwa kazi za kawaida, na hadi kufikia mwezi Machi 2016 Kikosi kimeingiziwa jumla ya Shilingi 3,815,620,000/= sawa na asilimia 118.

KIKOSI CHA VALANTIA (KVZ) – (D06)

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Valantia (KVZ) kina jukumu la kutoa ulinzi kwa kushirikiana na vikosi vya ulinzi na usalama vya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kulinda raia na mali zao na kutekeleza shughuli za kijeshi kwa wakati wa dharura kwa ajili ya kuimarisha usalama wa nchi.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Kikosi cha Valantia kinatekeleza Programu kuu mbili ambazo ni; Programu ya Amani na Utulivu kwa Raia, Taifa na mali zao na Programu ya Usimamizi na Utawala wa Kikosi Cha Valantia. Lengo kuu la programu ya kwanza ni kuhakikisha amani na utulivu kwa raia, taifa na mali zao inaimarika na Programu ya pili ina lengo la kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi kimefanya doria na kudumisha ulinzi katika vituo mbali mbali ikiwa ni pamoja na Ofisi za Serikali, taasisi binafsi na nyumba za viongozi wakuu wa Serikali. Kikosi kimewajengea uwezo wa kijeshi wapiganaji 25 kwa ngazi ya uongozi mkubwa na wapiganaji 178 kwa ngazi ya uongozi mdogo. Aidha kikosi kimeimarisha utoaji wa huduma na mahitaji muhimu kwa Maofisa na Wapiganaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Valantia kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kiliidhinishiwa jumla ya Shilingi 6,003,600,000/= na kwa kipindi cha miezi tisa kilikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 5,049,339,998/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2016 Kikosi kimeingiziwa jumla ya Shilingi 4,978,539,494/= sawa na asilimia 99.

MKOA WA MJINI MAGHARIBI – (D07)

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Mjini Magharibi unajukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango na Miongozo ya Serikali ndani ya Mkoa. Aidha, kuhakikisha ulinzi na usalama unaimarika pamoja na kutatua matatizo mbali mbali ya wananchi wa Mkoa huo.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Mkoa ulitekeleza majukumu yake kwa kupitia mfumo wa pragramu kuu mbili ambazo ni Uratibu wa shughuli/Miradi ya maendeleo na Programu ya Usimamizi na Utawala wa Mkoa. Kupitia programu hizi Mkoa ulilenga kuwahudumia wananchi kupitia huduma ya kuratibu shughuli za maendeleo ya Mkoa, kuratibu shughuli za Ulinzi na Usalama, kutoa misaada ya kijamii na kiuchumi, kuwasaidia wazee wasiojiweza na kutoa huduma za kiutumishi na kiuendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi 2016 Mkoa wa Mjini Magharibi ulitoa huduma za kuratibu mitihani ya majaribio na ya kitaifa ya ngazi mbali mbali na kuhamasisha uandikishaji wa watoto katika skuli za maandalizi na msingi ambapo watoto 4,842 maandalizi, na watoto 16,769 darasa la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa pia umefanya ufuatiliaji wa udhalilishaji wa watoto ambapo jumla ya matukio 56 yakiwemo ya utelekezwaji, kubakwa na kukashifiwa yameripotiwa na kufuatiliwa ambapo matukio 20 ya utelekezaji yamepatiwa ufumbuzi baada ya kufanyika majadiliano baina ya wazee na uongozi wa Wilaya. Watoto 14 wamepelekwa katika kituo cha kubadilishwa tabia, wakiwemo wanawake 4 na wanaume 10.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa kwa kushirikiana na Idara ya Kinga uliratibu utoaji wa taaluma ya kujikinga na maradhi ya mripuko wa kipindupindu na athari za mvua za vuli na masika ambapo vikao vya kamati ya maafa vilifanyika. Aidha maombi 46 ya usajili wa vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa (*SACCOSS)* yamepokelewa.

Mhe. Mwenyekiti, katika huduma ya uratibu wa shughuli za Usalama, Mkoa umefanya vikao 27 vya kawaida na vya dharura kujadili masuala ya usalama wa wananchi na mali zao yakiwemo ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015 na ule wa Machi 2016 . Aidha, Mkoa umeratibu na kufuatilia shughuli za ulinzi katika vipindi vya sikukuu za kitaifa pamoja na matukio ya kihalifu na maeneo hatarishi kiusalama.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa misaada ya kijamii na kiuchumi, Mkoa umewasaidia wananchi 52 kwa mahitaji mbali mbali. Aidha, wazee 2,071 wamepatiwa msaada wa Shilingi 93,195,000/= kwa kipindi cha miezi tisa. Katika kutoa huduma za kiutumishi na kiuendeshaji Mkoa umeimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi wake ikiwemo ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kutendea kazi na upatikanaji wa mahitaji mengine muhimu ya Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mradi wa jengo la Ofisi ya Mkoa wa Mjini Magharibi liliopo Amani ambao ni mradi wa ubia kati ya Serikali na Muwekezaji, ujenzi wake ulichelewa kutokana na sababu mbali mbali. Hata hivyo, juhudi za kuanza upya mradi huu zinaendelewa kuchukuliwa na mradi unategewa kuanza wakati wowote kuanzia sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Mkoa wa Mjini Magharibi, uliidhinishiwa Shilingi 1,521,800,000/= na kwa kipindi cha miezi tisa Mkoa ulikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 1,146,285,755/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2016 Mkoa umeingiziwa jumla ya Shilingi 929,008,050/= sawa na asilimia 81.

MKOA WA KUSINI UNGUJA – (D08)

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Unguja una majukumu ya kufuatilia, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kuhakikisha kuwa sera, mipango na miongozo ya Serikali inatekelezwa. Aidha, Mkoa una jukumu la kusimamia shughuli za Ulinzi na Usalama.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Unguja umetekeleza programmu kuu mbili za Kuratibu Maendeleo ya Mkoa na Kuratibu shughuli za Uendeshaji na Utawala. Hadi kufikia mwezi Machi 2016, Mkoa umefanya vikao vya Baraza la usalama 27 vya kawaida na 13 vya dharura kwa kujadili mambo muhimu yakiwemo uchaguzi mkuu, kuimarisha doria na kupunguza matukio ya uhalifu.

Mkoa kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama umeweza kuadhimisha siku ya Uhuru wa Tanganyika kwa kufanya usafi maeneo ya huduma za jamii yakiwemo maeneo ya Ofisi za Serikali, skuli, vituo vya afya na barabara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuweka mazingira bora ya kazi, ujenzi wa Ofisi ya Wilaya ya Kati unaendelea na hatua iliyofikiwa ni uwekaji wa jamvi la zege ya juu. Aidha katika kuratibu shughuli za Maendeleo, Mkoa umefanya ukaguzi wa ujenzi wa barabara zilizojengwa kwa kiwango cha kifusi kupitia Mradi wa "Kuimarisha Miundombinu ya Masoko (*MIVARF*) ambapo ujenzi wa barabara hizo umekamilika.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umefanya ukaguzi katika skuli tano na pia kukutana na kamati za Wazee za Skuli na Bodi za Elimu za Wilaya. Aidha Ukaguzi wa Walimu juu ya ufundishaji umefanyika katika skuli 16. Mkoa pia uliratibu shughuli za mitihani ya Taifa katika ngazi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umeratibu na kusimamia kilimo ambapo ekari 2,746 zimelimwa sawa na asilimia 69 ya lengo kwa kilimo cha mpunga. Jumla ya tani 50.5 za mbegu ya mpunga, mbolea ya kupandia paketi 294 na paketi 1,742 za mbolea ya kukuzia zimegaiwa. Pia juhudi za kusaidia wakulima wa kilimo cha mboga mboga zimefanyika ambapo visima vitatu vya umwagiliaji maji vimechimbwa katika shehia za Uzini na Kiboje Mkwajuni kwa kushirikiana na jumuiya ya UWAMWIMA kupitia washirika wa Maendeleo *Africa Development Fund (ADF)*.

Mhe. Mwenyekiti, mafunzo kwa wakulima wa migomba na viazi katika shehia za Pagali, Bambi, Kijibwemtu na Kiboje Muembe Shauri yametolewa. Mkoa umeratibu usambazaji wa mabomba ya maji kutoka Kibuteni - Makunduchi kilomita nne, Pango la maji Mnywambiji - Kibuteni kilomita moja na nusu na ukamilishaji wa ujenzi wa tangi la maji Chwaka.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuadhimisha siku ya UKIMWI Mkoa umeshiriki katika kuwapa msaada wa vyakula jumuiya ya watu wanaoishi na VVU wakiwemo vijana, wazee na watoto Wilaya ya Kati. Jumla ya wanachama 50 wa Jumuiya hiyo wamepatiwa msaada wa mahitaji muhimu uliogharimu jumla ya shilingi 16,200,000/= Aidha, wagonjwa watano wenye maambukizi wameorodheshwa Wilaya ya Kusini na kuingizwa kwenye mpango wa kupatiwa msaada huo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Mkoa wa Kusini Unguja, uliidhinishiwa Shilingi 1,336,600,000/= na kwa kipindi cha miezi tisa Mkoa ulikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 1,026,904,147/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2016 Mkoa umeingiziwa jumla ya Shilingi 867,429,450/= sawa na asilimia 84.

MKOA WA KASKAZINI UNGUJA (D09)

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja ina jukumu la kuratibu, kufuatilia, kusimamia na kutekeleza kazi za Serikali pamoja na shughuli za maendeleo katika Mkoa. Aidha Mkoa unajukumu la kuhakikisha kuwa Sera, Mipango na Maelekezo ya Serikali yanatekelezwa, kusimamia na kuendeleza shughuli za ulinzi na usalama katika Mkoa.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Unguja ulitekeleza Programu mbili kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Programu hizo ni programu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo ndani ya Mkoa na programu ya Utawala na Uendeshaji. Programu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo ndani ya Mkoa ina lengo la kuboresha huduma za jamii na Programu ya Utawala na Uendeshaji ina lengo la kuiwezesha Ofisi kutekeleza kazi zake kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umetoa elimu ya kupinga udhalilishaji pamoja na kufanya mikutano ya kampeni ya kupinga vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia ambapo wananchi pamoja na skuli kumi na tatu na madrasa mbali mbali wamepatiwa elimu hiyo. Kwa upande wa misaada, Mkoa umewapatia wazee 2,170 msaada wa Shilingi 97,650,000/= kwa kipindi cha miezi tisa.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi 2016, Mkoa umefanya vikao 20 vya kamati ya ulinzi na usalama ambavyo vimejadili mambo mbali mbali ya Mkoa. Aidha mikutano 13 ya uhamasishaji wa wananchi juu ya umuhimu wa kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo imefanyika ambapo Mkoa kwa kushirikiana na mradi wa *MIVARF* ulisimamia utekelezaji wa miradi mbali mbali ya wananchi, ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa barabara za ndani zenye jumla ya kilomita 18.5.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umeratibu na kusimamia ujenzi wa madarasa 11 ya awali katika maeneo ya Mahonda, Mkataleni, Mbiji, Kinduni kwa Gube na Mkadini. Kwa upande wa Elimu ya Msingi kuna madarasa 21 ambayo tayari yamekwisha jengwa katika skuli za Pangatupu, Zingwezingwe, Pale, Potoa na

Kandwi. Kwa upande wa Sekondari madarasa 8 yamejengwa katika Skuli za Potoa na Mkwajuni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Mkoa wa Kaskazini Unguja, uliidhinishiwa Shilingi 1,373,900,000/= na kwa kipindi cha miezi tisa Mkoa ulikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 1,043,689,318/= kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2016 Mkoa umeingiziwa jumla ya Shilingi 882,768,600/= sawa na asilimia 85.

MKOA WA KUSINI PEMBA – (D10)

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Pemba una jukumu la kusimamia Sheria, taratibu na miongozo iliyowekwa kwa kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama. Kuhakikisha sera, mipango na maelekezo ya serikali yanatekelezwa ipasavyo na rasilimali zote zinatumika kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Mkoa ulitekeleza majukumu yake kwa kupitia pragramu kuu mbili ambazo ni Uratibu wa shughuli za miradi ya maendeleo na Programu ya usimamizi na Utawala wa Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umefanikisha kuimarisha amani na utulivu katika kipindi chote na hasa kipindi cha uchaguzi pamoja na kupunguza vitendo vya kihalifu vya wizi wa mazao, mifugo na magendo ya karafuu. Vilevile Mkoa umesimamia ujenzi wa barabara za vijijini kupitia mradi wa *MIVARF* kwa kiwango cha kifusi zenye jumla ya kilomita 41.3 na tayari zimeshakamilika.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umeratibu ujenzi wa madarasa mapya 15 ya kusomea katika Skuli za Kilindi, Pujini, Matale na Vitongoji pia ukumbi mmoja na vyoo vinane vimejengwa katika Skuli ya Vitongoji. Ofisi pia imesimamia ukarabati wa majengo katika Skuli ya Kwale, Makoongwe, Kiwani Msingi, Chambani na Ngwachani yenye jumla ya madarasa 40, Ofisi za walimu, ghala na ukarabati wa paa katika skuli ya Kwale. Hadi kufikia mwezi Januari 2016, jumla ya wanafunzi 2,932 wanawake ni 1,514 na wanaume 1,418 wameandikishwa kuanza maandalizi na jumla ya wanafunzi 7,693 wanawake 3,763 na wanaume 3,930 wameandikishwa kwa ajili ya kuanza darasa la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi hichi wazee waliendelea kupatiwa msaada wa kuwawezesha kupata mahitaji yao ya kawaida, kwa kipindi cha miezi tisa Mkoa umelipa jumla ya Shilingi 101,880,000 kwa wazee 2,264. Aidha Mkoa umevijengea uwezo vikundi vya ushirika na wajasiriamali. Jumla ya vikundi 32 vimekaguliwa na kupatiwa elimu inayohusiana na shughuli zao wanazozifanya ili kuwaongezea kiwango cha uzalishaji na kuongeza kipato chao.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kusimamia zao la karafuu pamoja na kudhibiti magendo ya karafuu, Mkoa umeendelea na juhudi za kuzuia magendo pamoja na kuwahamasisha wananchi kuuza karafuu zao katika vituo vya Serikali (*ZSTC*) kwa maendeleo ya kiuchumi ya Taifa letu. Hadi kufikia Machi 2016, jumla ya tani 3,067 za karafuu zimenunuliwa kwa Shilingi 42,910,000,000/=sawa na asilimia 105 ya lengo la kununua tani 2,933.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa upande wa kilimo jumla ya ekari 3,607 zimelimwa kwa jembe la mkono ambayo ni sawa na asilimia 48.7 ya lengo la kulima ekari 7,400 na ekari 1,023 zimelimwa kwa trekta sawa na asilimia 31.9 ya lengo la kulima ekari 3,200. Jumla ya tani 214 za mbolea aina ya TSP na UREA, mbegu za mpunga tani 37 na dawa ya kuulia magugu lita 2,500 zimegaiwa kwa wakulima. Aidha Mkoa umeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama, ambapo visima virefu 20 vimechimbwa katika Shehia 19. Kati ya hivyo, visima 7 vimekamilika na kuanza kutoa huduma katika maeneo ya Matangini, Mahuduthi, Mtambile, Kwapopo-Chambani, Kwamabata–Mkanyageni, Changaweni na Mfikiwa.

Mhe. Mwenyekiti,Katika kutekeleza kampeni ya kupambana na vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, hadi kufikia Machi 2016, jumla ya kesi 27 za matukio mbalimbali ya udhalilishaji yameripotiwa ikiwemo ubakaji na ulawiti, shambulio, kutorosha na mimba za utotoni. Kati ya kesi hizo, kesi 17 zipo Polisi kwa hatua za upelelezi. Kesi 5 zipo Ofisi ya Muendesha Mashitaka (*DPP*) na Kesi 5 zipo Mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa umeendelea kuimarisha mazingira bora ya kazi kwa kufanya ukarabati mkubwa wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kuendelea na ujenzi wa Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani. Kwa upande wa masuala mtambuka, Mkoa umetoa mafunzo kwa kamati za Ukimwi za Shehia tano juu ya harakati za mapambano dhidi ya UKIMWI. Elimu juu ya uhifadhi wa mazingira pia imetolewa kwa vikundi 16 vya wanawake na vijana katika maeneo ya bahari na maeneo yaliyoathirika na uharibifu wa mazingira katika Shehia za Mwambe, Vitongoji, Wesha na Kisiwapanza.

Mhe. Mwenyekiti,Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Mkoa wa Kusini Pemba uliidhinishiwa Shilingi 1,772,000,000/= kati ya fedha hizo Shilingi 1,150,900,000/= ni kwa ajili ya kazi za kawaida za Mkoa na Shilingi 621,100,000/= ni ruzuku ya Baraza la mji Chake Chake na Baraza la Mji Mkoani, kwa kipindi cha miezi tisa Mkoa ulikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 1,471,572,409/=. Hadi kufikia mwezi Machi 2016 Mkoa umeingiziwa jumla ya Shilingi 1,321,198,471/= sawa na asilimia 90.

MKOA WA KASKAZINI PEMBA – (D11)

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Pemba una jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na kanuni kwa lengo la kustawisha hali za maisha ya wananchi wa Mkoa, kudumisha amani, ulinzi na usalama na kusaidia utekelezaji wa kazi za Serikali pamoja na shughuli za Maendeleo.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Pemba katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 ulijipangia kutekeleza Programu kuu tatu (3); Kuratibu Shughuli za Maendeleo katika Mkoa, Kuratibu Shughuli za Ulinzi na Usalama katika Mkoa na Programu ya Kuratibu shughuli za Mipango na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, Katika utekelezaji wa Programu ya kuratibu shughuli za maendeleo ndani ya Mkoa hadi kufikia Machi 2016, Mkoa umefuatilia miradi 26 inayotekelezwa na sekta mbali mbali. Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa barabara, ujenzi wa madarasa mapya ya skuli, Ujenzi wa Vituo vya afya na mradi wa maji safi na salama. Vile vile, Mkoa uliratibu na kushiriki sherehe mbali mbali za kitaifa katika kipindi hicho. Aidha, kazi za usafi wa mazingira kwa taasisi za Serikali na binafsi zilifanyika.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya pili ya kuratibu shughuli za ulinzi na usalama ina jukumu la kuhakikisha amani na utulivu na usalama wa raia na mali zao unaimarika. Hadi kufikia mwezi Machi, 2016 jumla ya vikao 20 vya Kamati ya Ulinzi na Usalama vilifanyika kujadili maswali ya usalama wa wananchi na mali zao.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya tatu ya kuimarisha shughuli za Uongozi na Utawala imesimamia upatikanaji wa vitendea kazi mbali mbali, huduma muhimu za uendeshaji na kufanya matengenezo ya Ofisi na nyumba za viongozi wa Mkoa na Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Mkoa wa Kaskazini Pemba, uliidhinishiwa Shilingi 1,659,600,000/= kati ya fedha hizo Shilingi 1,331,400,00/= ni kwa ajili ya kazi za kawaida za Mkoa na Shilingi 328,200,000/= ni ruzuku ya Baraza la Mji Wete, na kwa kipindi cha miezi tisa Mkoa ulikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 1,264,507,650/=. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya Shilingi 1,044,397,490/= zimepatikana sawa na asilimia 83.

OFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO (D12)

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho, ina wajibu wa kuwasajili na kuwapatia vitambulisho Wazanzibari Wakaazi na wasiokuwa wakaazi wanaoishi kisheria wenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

Utekelezaji wa Programu kwa Mwaka 2015/2016

Mhe. Mwenyekiti, Kupitia programu ya usajili hadi kufikia Machi 2016, Ofisi imesajili Wazanzibari wakaazi 8,691 na kupatiwa vitambulisho vyao. Aidha kupitia programu ya Utumishi na Uendeshaji, Ofisi imewapatia mafunzo wafanyakazi katika fani na ngazi tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2015/2016 Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho imeidhinishiwa Shilingi 1,768,900,000/= na kwa kipindi cha miezi tisa ilikadiria kutumia kiasi cha Shilingi 1,396,512,000/= kwa kazi za kawaida, na hadi kufikia mwezi Machi 2016 imeingiziwa jumla ya Shilingi 600,426,500/= sawa na asilimia 43.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Programu mbali mbali ya kuendeleza wafanyakazi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imesomesha wafanyakazi 229 Wanawake 97 Wanaume 132. Angalia kiambatanisho namba 9.

OFISI YA MRAJIS WA VIZAZI NA VIFO

Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii imehamishiwa katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ hivi karibuni ikitokea iliyokuwa Wizara ya Katiba na Sheria. Majukumu ya ofisi ni kusajili matukio ya kijamii, kutunza kumbukumbu na kutoa vyeti vya kuzaliwa, vifo, ndoa na talaka. Ofisi imetekeleza Program ndogo ya Usajili wa Matukio ya kijamii ambapo hadi kufikia Machi 2016 imesajili jumla ya Vizazi 39,353, vifo 2,286 ndoa 125 na talaka 16 kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo kwa mwaka 2015/16 imeanza rasmi kusajili Vizazi na kutoa vyeti kwa kutumia mfumo wa elektroniki. Kuanza kutumika kwa mfumo huu kutapunguza uchelewaji wa upatikanaji wa vyeti. Hata hivyo utaratibu huu umeanza katika Makao Makuu ya Ofisi ambayo inatoa huduma za usajili kwa Wilaya tatu za Unguja nazo ni Wilaya ya Mjini na Wilaya za Magharibi 'A' na 'B'

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2015/16 Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo imeidhinishiwa jumla ya shilingi 501,641,600/= kwa kipindi cha miezi tisa ilikadiria kiasi cha Shilingi 383,552,988/= kwa kazi za kawaida na hadi kufikia mwezi Machi 2016 imeingiziwa jumla ya Shilingi 276,157,275/= sawa na asilimia 72 ya makadirio.

SEHEMU YA PILI

MWELEKEO WA MATUMIZI YA BAJETI INAYOTUMIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha utekelezaji wa program za Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2015/16, naomba sasa uniruhusu niwasilishe mpango ya bajeti ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Mpango huu umezingatia pia vipaumbele viwili vya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambavyo ni Kutekeleza Sera ya Serikali za Mitaa kwa kugatua baadhi ya majukumu ya Serikali Kuu na kuyapeleka Serikali za Mitaa na kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina jumla ya Programu kubwa 28 na program ndogo 7 zitakazotekelezwa kupitia taasisi zake zinazojumuisha Taasisi za Ofisi kuu, Idara Maalum za SMZ, Mamlaka za Tawala za Mikoa na Ofisi ya Msajili wa Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho.

FUNGU (D01) TAASISI ZA OFISI KUU

Mhe. Mwenyekiti, Fungu hili la Taasisi za Ofisi Kuu limepanga kutekeleza programu kuu nne zifuatazo katika mwaka wa fedha 2016/2017.

i. Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
ii. Uratibu wa Idara Maalum za SMZ;

iii. Usimamizi wa Masuala ya Utumishi katika Idara Maalum za SMZ; na
iv. Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina program ndogo tatu za

(i) Usimamizi wa Shughuli za Utumishi na Utawala
(ii) Uratibu wa Kazi za Mipango, Sera na Utafiti na
(iii) Uratibu wa Kazi za *OR-TMSMIM* Pemba zinatekelezwa kwa pamoja na Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mipango Sera na Utafiti na Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti,Programu ndogo ya Usimamizi wa Shughuli za Utumishi na Utawala ina lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa kazi za ofisi. Programu itaendelea kusimamia majukumu ya kiutumishi ikiwemo kuendelea kuwahudumia wafanyakazi waliopo masomoni na upatikanaji wa huduma muhimu za kiutawala na nyenzo za kufanyia kazi. Programu itatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na imepangiwa jumla ya shilingi 1,111,016,542/=.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti,Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Mipango, Sera na Utafiti imepanga kusimamia, kuratibu na kufuatilia, utekelezaji wa mipango, Sera na tafiti mbali mbali za ofisi. Katika kufanikisha hilo,programu itaendelea kuandaa miongozo ya kisera na kisheria, kuimarisha kitengo cha utafiti, kuibua miradi na kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Programu imepangiwa jumla ya shilingi 286,501,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya uwekaji wa vifaa vya ulinzi (*CCTV*) inaendelea kuratibu kazi za kuendeleza Mradi wa Mji Salama ambapo kwa mwaka ujao wa fedha umepanga kukamilisha uwekaji wa kamera za ulinzi, ununuzi wa magari manne ya kuzimia moto, gari na pikipiki kwa ajili ya ufuatiliaji pamoja na boti na vifaa maalum kwa ajili ya doria. Programu imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 18,000,000,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, kazi nyengine zilizopangwa chini ya programu hii ni kuzifanyia matengenezo barabara tano za ndani zenye urefu wa kilomita 5.1

ambazo ni Msumbiji - Mwanakwerekwe Makaburini, Kidongo Chekundu na Tomondo njia panda hadi Mombasa Changu kwa upande wa Unguja. Kwa upande wa barabara za Pemba, Soko kongwe kupitia Uwanja wa Tibirinzi - Skuli ya Ng'ombeni na barabara ya Kitutia -Mitiulaya.

OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya tatu ya Uratibu wa Kazi za OR-TMSMIM za SMZ inalenga kuongeza ufanisi katika upangaji na uratibu wa kazi za Ofisi kwa upande wa Pemba. Huduma zitakazotolewa na Programu hii ni kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera, Sheria na mipango kwa upande wa Pemba. Programu itatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba na imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 511,917,500/=.

IDARA YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inatekeleza Programu Kuu ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Chini ya programu hii Idara itatekeleza Programu ndogo mbili (2) ambazo ni (i) Uratibu wa Tawala za Mikoa na (ii) Uratibu wa Serikali za Mitaa. Programu ndogo ya Uratibu wa Tawala za Mikoa ina lengo la kuwawezesha wananchi kushiriki katika mipango ya maendeleo ya maeneo yao kwa kusimamia utekelezaji wa Sera ya Serikali za Mitaa kupitia kamati za maendeleo za Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Uratibu wa Serikali za Mitaa inalenga kuimarisha uratibu kwa kutoa miongozo itakayosaidia utekelezaji wa Ugatuzi wa Madaraka kwa Wananchi, katika kufanikisha adhma hii Ofisi itazingatia utekelezaji wa Sera ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2012 ambapo kwa kuanzia itajikita katika maeneo makuu yafuatayo; kufanya mapitio ya muundo wa kitaasisi ya serikali za mitaa, kuimarisha usimamiazi wa rasilimali watu, kuandaa mifumo ya ukusanyaji na matumizi ya fedha na kukuza usimamizi wa utawala bora na elimu kwa umma katika utekelezaji wa sera. Programu itatekelezwa na Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na imepangiwa kutumia jumla ya shillingi 2,391,639,508/=.

IDARA YA URATIBU WA IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Mwenyekiti, Lengo kuu la programu ni kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa Idara Maalum kwa kuimarisha mfumo, uwezo na upatikanaji wa huduma. Aidha kukuza ushirikiano na vyombo vya ulinzi na usalama vya ndani na nje ya nchi. Matarajio makubwa ni kujenga uwezo wa Idara Maalum katika kutimiza majukumu yake. Programu itatekelezwa na Idara ya Uratibu wa Idara Maalum na imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi. 44,993,000/=.

TUME YA UTUMISHI YA IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Mwenyekiti, Kupitia programu ya Usimamizi wa Masuala ya Utumishi katika Idara Maalum za SMZ, Tume ina lengo la Kuimarisha misingi ya utawala bora na Sheria katika Idara Maalum. Programu itatekelezwa na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum na imepangiwa kutumia Shilingi 115,233,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, Fungu nambari D01 lenye jumla ya Programu Kuu Nne na programu ndogo 5 linasimamiwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambalo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 limepangiwa matumizi ya jumla ya Shilingi 22,461,300,000/=. Hivyo naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya shilingi 600,000/= kama mchango katika mfuko mkuu wa Serikali.

IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

FUNGU (DO2) JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa Fedha 2016/2017 fungu hili limepanga kutekeleza Programu Kuu mbili; Programu ya Mafunzo ya Amali, Uzalishaji, Uzalendo na Michezo kwa Vijana na Programu ya Ulinzi, Mipango na Uendeshaji wa JKU.

Programu ya Mafunzo ya Amali, Uzalishaji, Uzalendo na Michezo kwa Vijana

Mhe. Mwenyekiti**, j**ukumu la program ni kupunguza kiwango cha ukosefu wa ajira, kukuza michezo na kuongeza uzalishaji wa chakula. Programu hii inazo programu ndogo mbili ambazo ni Uzalendo, Uzalishaji na Michezo na programu ya Ufundi na Kazi za Amali.

Programu ndogo ya Uzalendo, Uzalishaji na Michezo ina lengo la kuongeza uelewa wa kutumia mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo, kuibua na kukuza vipaji vya michezo na kuimarisha utaifa. Programu itatekelezwa na Idara ya Utawala ya JKU na imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 32,000,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ndogo ya Ufundi na Kazi za Amali ina lengo la kuwaongezea uwezo vijana 1,450 waweze kuajirika, kujiajiri, na kuchangia kuinua kiwango cha ufaulu kwa vijana. Huduma zinazotarajiwa kutolewa na programu hii ni mafunzo ya ufundi kwa vijana na kuwaendeleza vijana ngazi ya sekondari. Programu itatekelezwa na Idara ya Utawala ya JKU na imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 17,000,000/=.

Programu ya Ulinzi, Mipango na Uendeshaji wa JKU

Mhe. Mwenyekiti, Programu ina jukumu la kuwaandaa vijana kuwa raia wema katika jamii. Matarajio ya programu ni kuwepo kwa chombo imara cha kuwajenga vijana kimaadili na kimaendeleo. Huduma zinazotarajiwa kutolewa na programu ni kujenga uwezo wa kitaasisi ili kusimamia utekelezaji wa majukumu. Programu itatekelezwa na Idara ya Utawala ya JKU na imepangiwa kutumia jumla ya shilingi. 11,407,400,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, Fungu nambari D02 lenye jumla ya Programu Kuu 2 na program ndogo 2 linalosimamiwa na Mkuu wa Kikosi cha JKU kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 limepangiwa matumizi ya jumla ya Shilingi 11,456,400,000/= kwa kazi za kawaida. Hivyo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya Shilingi 44,400,000/= kupitia programu hizi.

D03 - CHUO CHA MAFUNZO (MF)

Mhe. Mwenyekiti, Fungu hili kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 limepanga kutekeleza Programu kuu mbili; Programu ya urekebishaji wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo na Programu ya Uongozi na Utawala wa Chuo cha Mafunzo.

Program ya Huduma za Urekebishaji Wanafunzi wa Chuo Cha Mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Huduma za Urekebishaji Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo ina jukumu la kuimarisha huduma za urekebishaji wanafunzi.

Huduma zinazotarajiwa kutolewa na programu hii ni urekebishaji wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo ikiwemo mradi wa ujenzi wa jengo la urekebishaji tabia kwa watoto. Programu itatekelezwa na Idara ya Sheria na Urekebishaji na imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi. 1,218,895,000/=.

Programu ya Uongozi na Utawala wa Chuo cha Mafunzo

Mhe. Mwenyekiti, Programu ina jukumu la kutoa huduma za kiutawala na uendeshaji. Matarajio ya Programu hii ni kupatikana mazingira wezeshi ya kazi, ustawi wa watumishi na usimamizi mzuri wa fedha. Programu itatekelezwa na Idara ya Utawala na Fedha na imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 8,001,105,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, Fungu nambari D03 lenye jumla ya Programu Kuu 2 linalosimamiwa na Kamishna wa Chuo cha Mafunzo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 limepangiwa matumizi ya jumla ya shilingi. 9,220,000,000/=. Hivyo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya shilingi. 60,578,000/= kupitia programu hizi na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

FUNGU DO4 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 fungu hili limepanga kutekeleza Programu kuu mbili; Programu ya Usimamizi na Uzuiaji wa Magendo na Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Huduma za Watumishi,

Programu ya Usimamizi na Uzuiaji wa Magendo

Mhe. Mwenyekiti, Programu ina jukumu la kuimarisha ulinzi wa bahari ya Zanzibar, kudhibiti usafirishaji wa magendo baharini na nchi kavu, uchafuzi wa mazingira, uhamiaji haramu pamoja na uokozi. Matarajio ya programu ni kuimarika kwa ulinzi na kupungua kwa magendo. Huduma zinazotarajiwa kutolewa na Programu hii ni kuzuia Usafirishaji wa Magendo Baharini, Ulinzi na Uokozi. Programu itatekelezwa na Idara ya Utawala na Fedha na Idara ya Mipango ya Ulinzi na imepangiwa kutumia jumla ya shilingi. 964,700,000/=.

Programu ya Utawala na Uendeshaji wa Huduma za KMKM

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la programu hii ni kutoa huduma za kiutawala na uendeshaji wa huduma za Kikosi na huduma bora na endelevu za afya kwa

wapiganaji na raia. Matarajio ya Programu ni kuongezeka kwa huduma na kuimarika kwa Mazingira ya Ofisi. Programu inatarajiwa kutoa huduma za afya kwa wapiganaji na raia, huduma za kiutawala na uendeshaji na ujenzi wa vituo vya uzamiaji na uokozi Unguja na Pemba pamoja na miradi ya maendeleo. Programu itatekelezwa na Idara ya Utawala na Fedha na imepangiwa kutumia jumla ya shilingi. 15,411,800,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, Fungu nambari D04 lenye jumla ya Programu Kuu 2 linalosimamiwa na Kamanda Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 limepangiwa matumizi ya jumla ya Shilingi 16,376,500,000/= kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Hivyo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya Shilingi 31,005,000/= kupitia programu hizi na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

FUNGU DO5 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI (KZU)

Mhe. Mwenyekiti, Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Fungu limejipangia kutekeleza program kuu mbili; Programu ya Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi na Programu ya Kukuza Huduma za Kiutawala na Kiuongozi kwa wapiganaji wa Kikosi.

Programu ya Utoaji wa Huduma za Zimamoto na Uokozi

Mhe. Mwenyekiti, Programu ina jukumu la kutoa huduma za zimamoto zenye ufanisi. Matarajio ya Programu ni kutoa huduma za zimamoto na uokozi kwa haraka na kwa ufanisi, pia kutoa huduma katika vituo maalum vya bandarini na viwanja vya ndege. Programu itatekelezwa na Kitengo cha Operesheni chini ya Idara ya Utawala na Fedha na imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 268,404,000/=

Programu ya Kukuza Huduma za Kiutawala, Maafisa na Wapiganaji wa Kikosi

Mhe. Mwenyekiti**,** Programu ina jukumu la kuimarisha mazingira ya kazi ili kuongeza uwajibikaji kwa Maafisa na Wapiganaji. Programu inatarajia kutoa huduma za kiutawala na kuwajengea uwezo Maafisa na Wapiganaji kwa kwa kutoa mafunzo na kukuza mashirikiano na taasisi mbali mbali. Programu itatekelezwa na Idara ya Utawala na Fedha na imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 4,642,696,000/=

Mhe. Mwenyekiti**,** Fungu nambari D05 lenye jumla ya Programu Kuu 2 linalosimamiwa na Kamishna wa Zimamoto na Uokozi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 limepangiwa matumizi ya jumla ya Shilingi 4,911,100,000/= kwa kazi za kawaida. Hivyo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya shilingi. 21,084,000/= kupitia Programu hizi na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

FUNGU DO6 - KIKOSI CHA VALANTIA (KVZ)

Mhe. Mwenyekiti, Kikosi cha Valantia katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kimepanga kutekeleza program kuu mbili; Programu ya Kutunza Amani na Utulivu kwa Raia, Taifa na mali zao na Programu ya Usimamizi na Utawala wa Kikosi Cha Valantia.

Program ya Kutunza Amani na Utulivu kwa Raia, Taifa na mali zao

Mhe. Mwenyekiti, Programu ina jukumu la kuhakikisha kuwa amani na utulivu kwa raia, Taifa na mali zao inaimarika. Matarajio ya programu ni kuwepo kwa amani na utulivu kwa jamii. Programu inatarajia kutoa huduma za ulinzi katika taasisi za Serikali, taasisi binafsi na jamii kwa ujumla. Programu itatekelezwa na Idara ya Utawala na na imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 358,000,000/=

Programu ya Usimamizi na Utawala wa Kikosi Cha Valantia

Mhe. Mwenyekiti, Program ina jukumu la kutoa huduma za kiutawala na uendeshaji wa huduma za kikosi cha Valantia na kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi. Matarajio ya Programu hii ni kuimarika kwa mazingira ya kufanyia kazi. Huduma zitakazotolewa ni za kiutumishi. Programu itatekelezwa na Idara ya Utawala na imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 7,169,100,000/=.

Mhe. Mwenyekiti**,** Fungu nambari D06 lenye jumla ya Programu Kuu 2 linalosimamiwa na Kamanda Mkuu wa Kikosi cha Valantia kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 limepangiwa matumizi ya jumla ya shilingi 7,527,100,000/= kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Hivyo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya Shilingi 21,084,000/= kupitia Programu hizi na kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

MAMLAKA ZA MIKOA

FUNGU - DO7 MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi katika mwaka wa Fedha 2016/2017 imepanga kutekeleza Programu kuu mbili (2); Programu ya Kwanza ni ya Uratibu wa Shughuli na Miradi ya Maendeleo ya Mkoa na Programu ya pili ni ya Usimamizi na Utawala.

Programu ya Uratibu wa Shughuli na Miradi ya Maendeleo ya Mkoa
Mhe. Mwenyekiti, Programu ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma za kijamii. Matarajio ya Programu ni kuwepo ufanisi na ubora wa utekelezaji wa shughuli na miradi ya maendeleo. Huduma zinazotarajiwa kutolewa na Programu ni kuratibu shughuli za maendeleo na shughuli za ulinzi na usalama ndani ya Mkoa. Programu imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 240,387,800/=.

Programu ya Usimamizi na Utawala

Mhe. Mwenyekiti, Programu ina jukumu la kuimarisha mazingira ya kazi, kusimamia stahiki na kuwajengea wafanyakazi uwezo wa kitaaluma. Matarajio ya Programu ni ufanisi wa kazi na upatikanaji wa huduma bora. Huduma zitakazotolewa na Programu ni za kiutumishi na uendeshaji. Programu imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 1,396,812,200/=.

Mhe. Mwenyekiti, Fungu nambari D07 lenye jumla ya Programu Kuu 2 linalosimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 limepangiwa jumla ya shilingi 1,637,200,000/= kwa kazi za kawaida. Hivyo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya shilingi 35,989,000/= na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

FUNGU – D08. MKOA WA KUSINI UNGUJA

Mhe. Spika, Mkoa wa Kusini Unguja katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 imepanga kutekeleza Programu kuu mbili (2) Programu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo ya Mkoa na Programu ya Uendeshaji na Utawala.

Programu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo ya Mkoa

Mhe. Mwenyekiti**,** Programu ina jukumu la kuimarisha uratibu wa shughuli za sekta za kijamii. Matarajio ya programu ni kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma bora za maendeleo kwa jamii. Huduma zinazotarajiwa kutolewa na Progamu ni kuratibu maendeleo ya jamii na kuratibu shughuli za ulinzi na usalama ndani ya Mkoa. Programu imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 193,727,200/=.

Programu ya Uendeshaji na Utawala

Mhe. Mwenyekiti, Program ina jukumu la kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanawajibika ipasavyo katika utoaji wa huduma. Matarajio ya Programu hii ni kuimarika kwa mazingira ya utendaji kazi na kuongeza ufanisi. Programu imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 1,069,872,800/=

Mhe. Mwenyekiti, Fungu nambari D08 lenye jumla ya Programu Kuu 2 linalosimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 limepangiwa jumla ya Shilingi 1,263,600,000/= kwa kazi za kawaida. Hivyo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya shilingi 4,790,000/= na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

FUNGU – DO9. MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kaskazini Unguja katika mwaka wa fedha 2016/2017 imepanga kutekeleza Programu kuu mbili; Programu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo ya Mkoa na Programu ya Utawala na Uendeshaji.

Programu ya Uratibu wa Shughuli za Maendeleo ya Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, Programu ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za kijamii. Matarajio ya Programu ni kupatikana kwa huduma bora za maendeleo. Programu imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 401,000,000/=.

Programu ya Utawala na Uendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, programu ina jukumu la kuwajengea uwezo wafanyakazi ili waweze kumudu kazi zao kwa ufanisi pamoja na kuwapatia stahiki zao.

Matarajio ya programu ni kuongeza kiwango cha utoaji huduma. Huduma zinazotarajiwa kutolewa na programu hii ni za kitumishi na uendeshaji wa Mkoa. Programu imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 872,400,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, fungu nambari D09 lenye jumla ya Programu Kuu mbili linalosimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 limepanga kutumia jumla ya shilingi. 1,273,400,000/= kwa kazi za kawaida. Hivyo, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya shilingi 4,790,000/= na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

FUNGU - D10. MKOA WA KUSINI PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini Pemba katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 umepanga kutekeleza programu kuu mbili; Programu ya Kuratibu Shughuli za Maendeleo na Programu ya Mipango na Utawala katika Mkoa.

Programu ya Kuratibu Shughuli za Maendeleo katika Mkoa

Mhe. Mwenyekiti, programu ina jukumu la kufuatilia miradi ya maendeleo ya wananchi. Matarajio ya Programu ni kuwa na maendeleo endelevu ndani ya Mkoa. Programu imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 50,938,000/=.

Programu ya Mipango na Utawala

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Mipango na Utawala katika Mkoa ina jukumu la kutoa huduma endelevu za kiutumishi na kiutawala. Matarajio ya Programu ni kuimarika kwa upatikanaji wa huduma. Programu imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 1,867,462,000/=

Mhe. Mwenyekiti, fungu D10 lenye Programu Kuu mbili limepangiwa matumizi ya jumla ya Shilingi 1,918,400,000/=, kati ya hizo shilingi 782,000,000/= ni ruzuku kwa Baraza la Mji Mkoani na Baraza la Mji la Chake Chake. Hivyo, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa.

FUNGU – D011. MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa mwaka wa fedha 2016/2017 imepanga kutekeleza Programu kuu mbili; Programu ya

Kuratibu Kazi za Maendeleo katika Mkoa na Programu ya kuratibu Kazi za Mipango na Utawala.

Programu ya Kuratibu Kazi za Maendeleo katika Mkoa

Mhe. Mwenyekiti, programu ina jukumu la kufuatilia kazi za maendeleo ndani ya Mkoa. Matarajio ya Programu hii ni kuwa na maendeleo endelevu. Huduma zinazotarajiwa kutolewa na programu ni kuratibu miradi ya maendeleo katika Mkoa. Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 86,792,000/=.

Programu ya kuratibu Kazi za Mipango na Utawala

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Kuratibu Kazi za Mipango na Utawala ina jukumu la kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanawajibika ipasavyo katika kazi zao. Matarajio ya Programu ni kuimarika kwa upatikanaji wa huduma na kuwa na mazingira bora ya kazi. Programu inatarajia kutoa huduma za mipango na utawala na kusimamia na kutoa huduma za usafi wa mji wa Wete. Programu imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 1,487,508,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, fungu nambari D11 lenye Programu Kuu mbili limepanga kutumia jumla ya Shilingi 1,574,300,000/=. Kati ya fedha hizo shilingi 330,500,000/= ni ruzuku ya Baraza la Mji Wete. Hivyo, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa.

FUNGU – D12. OFISI YA USAJILI VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Usajili Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho katika mwaka wa fedha 2016/2017 imepanga kutekeleza Program Kuu tatu (3); Programu ya Kusajili na Kutoa Vitambulisho kwa Wazanzibari na wasio Wazanzibari wanaoishi kisheria, Programu ya Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Usajili wa Vizazi Vifo na Kadi za Utambulisho na Programu ya Kusajili Matukio ya Kijamii.

Programu ya Kusajili na Kutoa Vitambulisho kwa Wazanzibari na wasio Wazanzibari wanaoishi kisheria

Mhe. Mwenyekiti, programu ina lengo la kuwatambua Wazanzibari na wasio Wazanzibari wanaoishi Zanzibar. Programu imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 75,000,000/=.

Programu ya Utumishi na Uendeshaji Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho

Mhe. Mwenyekiti, programu ina jukumu la kutoa huduma endelevu za kiutawala kwa ofisi katika kutekeleza majukumu yake. Matarajio ya programu ni kuwa na mazingira mazuri ya kazi. Programu itatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji na imepangiwa kutumia jumla ya shilingi 1,486,100,000/=.

Programu ya Kusajili Matukio ya Kijamii

Mhe. Mwenyekiti, programu ya kusajili matukio ya kijamii ina jukumu la kusajili, kutunza kumbukumbu na kutoa vyeti vya vizazi, vifo, ndoa na talaka na uasili wa mtoto na kuendeleza usajili wa vizazi kwa mfumo wa kielektroniki. Programu imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 528,800,000/= na itatekelezwa na Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo.

Mhe. Mwenyekiti, fungu namba D12 lenye jumla ya Programu Kuu linalosimamiwa na Mkurugenzi wa Usajili, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 limepangiwa jumla ya Shilingi. 2,089,900,000/= kwa kazi za kawaida. Hivyo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe fedha hizo kwa matumizi yaliyopangwa. Aidha naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ukusanyaji wa mapato ya shilingi 275,430,000/= kupitia Programu hizi na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

SHUKURANI

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwashukuru watendaji Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi hii ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, napenda kuwashukuru Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Makamanda wote wa Idara Maalum za SMZ na wafanyakazi wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Radhiya Rashid Haroub na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Kai Bashir Mbarouk kwa mashirikiano waliyonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, navishukuru vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Idara Maalum za SMZ katika kudumisha amani na utulivu nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nawashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Tumbatu, kwa mashirikiano makubwa waliyonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kiofisi pamoja na Jimboni. Pia naishukuru familia yangu kwa uvumilivu wao kwa muda wote niliokuwa mbali nao wakati

nikitekeleza majukumu ya Kitaifa. Uvumilivu wao na moyo walonipa umeniongezea nguvu na ari katika kutekeleza majukumu yangu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha naomba nizishukuru Taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi zilizoshirikiana na ofisi yangu katika kutimiza majukumu yake. Napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo na nchi rafiki ambazo zinaendelea kuchangia katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi yangu kwa misaada na ushirikiano wao katika mwaka wa fedha 2015/2016. Miongoni mwao ni; Jamhuri ya Watu wa China, India, Jamhuri ya Watu wa Korea ya Kusini, Ujerumani, Uingereza, Romania, Israel, Afrika ya Kusini, Misri, Benki ya Dunia, *UNICEF*, na wengine wote waliofanikisha kuchangia maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inasimamia jumla ya mafungu 12 ya Bajeti yanayoanzia D01 – D12. Makadirio ya matumizi ya Programu kupitia mafungu hayo ni kama yanavyoonekana katika *Kiambatanisho namba 10*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 81,709,200,000/=, ambapo kati ya fedha hizo shilingi 61,390,000,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 20,319,200,000/= ni kwa kazi za Maendeleo. Kati ya shilingi 61,390,000,000/= shilingi 48,380,600,000/= ni kwa matumizi ya mishahara na maposho, shilingi 10,396,900,000/= kwa matumizi ya kazi nyenginezo (*OC*) na shilingi 2,612,500,000/= ni ruzuku ya Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji ya Wete, Chake Chake na Mkoani. Aidha naliomba pia Baraza lako Tukufu liidhinishe makusanyo ya mapato ya shilingi 499,750,000/= yatakayoingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri hoja imeungwa mkono.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Machano Othman Said (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kutoa hotuba ya maoni

ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia kukutana hapa tukiwa wazima asubuhi yetu hii ya leo. Aidha kwa rehma zake Mwenyezi Mungu atujaalie kheri ili tuweze kuendelea na Baraza letu tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia uniruhusu nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kuchaguliwa kwa mara nyengine tena na Mhe Rais, hii inaonesha wazi kuwa Mhe Waziri ni mchapakazi mzuri na kamati yangu inamuombea kheri na mafanikio katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoipa kamati yangu katika kutekeleza majukumu yetu ya kazi. Vile vile, napenda kuishukuru Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kuwasilisha mbele ya kamati yetu pamoja na Baraza lako Tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2016/2017 ili yapate Baraka za Wajumbe wako na baadae yapitishwe kwa maslahi ya wananchi na serikali kwa ujumla. Napenda pia kumpongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Mikoa wapya na Wakuu wa Wilaya ambao wameteuliwa hivi karibuni kwa kuwatakia mafanikio mema.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukuwa fursa hii kwa dhati kabisa kuwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Mfenesini kwa kuniamini na kuweza kunichagua kuwa mwakilishi wao kwa kipindi cha miaka mitano. Sina cha kuwalipa ila niwaahidi kuwa tutakuwa pamoja katika mambo yote yanayohusiana na Jimbo la Mfenesini na inshaallah, Mwenyezi Mungu atatufanyia wepesi katika kutekeleza majukumu hayo kama ambavyo tumepanga.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kuwashukuru kwa kazi kubwa walioifanya Wajumbe wa Kamati yangu wakati tulipokua tukipitia bajeti hii kwa kunionesha mashirikiano yao makubwa katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu ambayo yanaiwezesha kamati hii kufanya kazi zake kwa ufanisi. Hivyo, kwa ridhaa yako naomba niwataje Waheshimiwa Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Machano Othman Said - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
5. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Mjumbe
6. Mhe. Shamata Shaame Khamis - Mjumbe
7. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf - Mjumbe
8. Mhe. Ali Khamis Bakar - Mjumbe
9. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
10. Ndg. Ali Alawy Ali - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza kutoa maoni ya kamati yangu ni vyema tukajua kwamba kwa kipindi hiki kamati ilikosa muda wa kufanya kazi zake mapema kutokana na kuchelewa kwa kuanza kwa shughuli za Baraza, na kupelekea kutoweza kutembelea wizara na idara ziliopo chini yake ambazo zingeweza kuieleza kamati na sisi tukaweza kushauri, kuagiza na kupendekeza mambo mbali mbali ambayo yangeleta faida kwa serikali na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa kwa niaba ya kamati yangu naomba uniruhusu niwasilishe maoni yetu juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

IDARA ZA MAKAO MAKUU

Mhe. Mwenyekiti, katika fungu hili kamati imeridhishwa na malengo waliojipangia kupitia kwenye *programme* zake kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo kamati inaendelea kuisisitiza serikali iweze kuwaingizia fedha kwa wakati na ipasavyo kwa ajili ya kufikia malengo yao waliokusudia kuyafanya.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, mbali na majukumu iliyopangiwa idara hii ikiwemo kusimamia sera, mipango na programu za wizara lakini pia ina jukumu la ufatiliaji wa tathmini za programu na miradi. Na kwa mwaka wa fedha 2015/2016 idara hii nayo ilikabiliwa na tatizo la uingizwaji wa fedha usioridhisha kitu ambacho kimeweza kukwamisha utekelezaji wa malengo yake. Hivyo, kamati inaendelea kuisistiza tena serikali kwa mwaka wa fedha ujao wa 2016/2017 uingizwaji wa fedha uwe mzuri ili wizara iweze kukamilisha malengo waliojipangia.

OFISI YA AFISA MDHAMINI – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba tunashukuru imeweza kuingiziwa fedha vizuri zaidi ya nusu ya kile walichopangiwa, kitu ambacho kimeipa faraja kamati kwani wao ni kiungo muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya kazi za wizara kwa upande wa Pemba.

IDARA MAALUM ZA SMZ

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Idara Maalum za SMZ napenda kuwashukuru kwa dhati kabisa kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuhakikisha usalama wa nchi na raia kwa kipindi chote kabla na baada ya uchaguzi.

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeridhishwa na uingizwaji wa fedha kwa upande wa Jeshi la Kujenga Uchumi kwa mwaka 2015/2016, ambapo wamepatiwa asilimia 88 ya kile walichoidhinishiwa kukipata. Hivyo, kamati inapenda kusisitiza utendaji mzuri katika fedha zinazoingizwa kupitia mafungu yao ili yale yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa ndani ya mwaka ujao wa fedha.

CHUO CHA MAFUNZO

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Chuo cha Mafunzo kamati yangu inawapongeza kwa kutekeleza majukumu yao ya kila siku, lakini pia kamati inawataka waendelee kutoa huduma vizuri kwa wanafunzi wa chuo na vile vile waendelee kujiiimarisha katika shughuli za uzalishaji mali pamoja na kutoa elimu ya ujasiri amali kwa wanafunzi wa chuo ili wanapotoka waweze kujitegemea.

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Mhe. Mwenyekiti, kikosi kimeendelea na majuku yake ya kawaida ya kuzuia magendo pamoja na kuhakikisha usalama katika maeneo ya baharini ikiwemo abiria na mali zao.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na jitihada hizo ambazo zinafanywa na KMKM lakini pia kamati inaishauri serikali kukipatia kikosi vifaa vya kutosha pamoja na mafuta kwa ajili ya kufanyia doria katika maeneo ya baharini na kuweza kuisaidia serikali katika kuzuia uingizwaji wa bidhaa kinyume na sheria kupitia bandari bubu ambazo zina changamoto za kupitisha magendo ya bidhaa pamoja na madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, aidha kamati inakipongeza Kikosi cha KMKM kwa kutoa huduma za afya vizuri katika hospitali yao ya Kibweni, kwani hospitali hiyo imekuwa kimbilio la wananchi wengi wa Wilaya ya Magharibi "A"

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Kikosi cha Zimamoto mbali na kutekeleza majukumu yake ya uokozi wa maisha na mali za watu, kamati imeona kuna ukosefu wa kituo cha zima moto katika Wilaya ya Micheweni Pemba hali ambayo kwa sasa ni changamoto kubwa kwa wakaazi wa eneo hilo, kwani wanakabiliwa na matukio ya moto ya mara kwa mara ambayo yanaathiri raia na mali zao. Hivyo basi, kamati inaona ni busara kuwekwa kituo cha Zima moto ili kupunguza athari zinazojitokeza kila siku kutokana na majanga ya moto.

Mhe. Mwenyekiti: aidha kamati inaiomba Serikali kuharakisha upatikanaji wa magari mapya ya zima moto katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Aman Karume kwa lengo la kujiimarisha zaidi kiusalama.

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Mhe. Mwenyekiti, Awali ya yote napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Ayoub Moh'd Mahmoud kwa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib ambapo wananchi wa Mkoa huo wana mategemeo makubwa na uongozi wake, pamoja na Wakuu wake wa Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Mjini Magharibi umeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo la utekelezaji wa sera, sheria, mipango na miongozo ya Serikali ndani ya Mkoa huo.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na utekelezaji huo Mkoa unakabiliwa na tatizo la ukosefu wa ofisi hali ambayo inapelekea usumbufu katika utendaji kazi wake, kwani inawalazimu kuhama hama kwa afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini katika majengo tofauti na kukodi kitu ambacho kamati imeona ni hasara kwa Serikali kulipia kodi ya jengo na badala yake kamati inaishauri Serikali kujitahidi kujenga majengo yake wenyewe ya Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya za Mkoa huo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inatoa ushauri kwa uongozi wa Mkoa wa Mjini Magharibi kujipanga vizuri katika kukabiliana na maradhi ya miripuko kama kipindupindu na mafuriko ya mara kwa mara hali ambayo kwa kiasi kikubwa inasababishwa na ujenzi holela katika mkoa huo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Baraza la Manispaa kamati yangu inatoa pongezi kwa Baraza la Manispaa kwa kusafisha mji zaidi katika kipindi hichi cha mripuko wa maradhi ya kipindu pindu. Vile vile kamati yangu inashauri Baraza la Manispaa kuweka utaratibu maalum wa kutoa maegesho ya magari *parking* kwa watu binafsi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Mwenyekiti, pia kamati inashauri Serikali kuwapatia ruhusa ya kuajiri wafanyakazi wataalamu kwa ajili ya kuongoza vitengo muhimu vya manispaa hiyo.

Mhe Mwenyekiti, kamati inatoa shukrani kwa Mkurugenzi na Watendaji wa Halmashauri ya Magharib kwa kuweza kutumia vizuri rasilimali zao kwa wakaazi wa Wilaya ya Magharib. Aidha, kamati inaipongeza Serikali kwa kuipandisha hadhi Halmashauri hiyo kwa kuwa na Manispaa mbili ambazo ni Manispaa ya Magharib “A” na Manispaa ya Magharib “B”. Kamati inaona wakati umefika kwa manispaa hizo kuanza kazi mara moja hasa kwa vile madiwani tayari wameshachaguliwa tangu machi 20 ni mwezi wa tatu sasa waheshimiwa madiwani walipochaguliwa na wapo bila ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, kwa upande wa halmashauri, kamati yangu inaishauri wizara kuwaajiri wafanyakazi wa halmashauri zote ambao hawajaajiriwa na wametumikia halmashauri hizo zaidi ya miaka mitano (5) kwani wao wameshakua wazoefu na wanajua mambo mengi ya kazi tofauti na

mtu atakaeajiriwa akiwa mpya. Hivi sasa wafanyakazi wengi wa halmashauri hizo kwenye vitengo muhimu hawana ajira ya kudumu, hali ambayo inaweza kushusha ufanisi wa kazi na kudhorotesha mapato halmashauri hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Aidha, kamati yangu inazishauri halmashauri zote kuweka utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kupitia masoko ya samaki ambayo yanafanya minada, kwani kupitia minada hiyo masoko hukusanya mapato ambayo hayaifaidishi serikali kwa vile hadi sasa mapato hayo hubaki kwa wananchi wenyewe na hali hii imejitokeza kutokana na wahisani wanaojenga masoko hayo baada ya kumalizika kuwakabidhi kwa wananchi wenyewe na sio Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kamati inashauri kuangaliwa upya maslahi ya wakurugenzi wa Halmashauri kwani kwa sasa ni madogo ukilinganisha na maslahi wanayopata wakurugenzi wengine Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, pia kamati inaishauri Serikali kupitia wizara ya ardhi kuweka mipango miji vizuri ili kuweza kuepuka hasara zitokanazo na ujenzi holela ambao haufuati utaratibu na ujenzi unaofanywa katika maeneo ya mabondeni kwenye vianzio vya maji ambapo hupelekea athari wakati wa mvua pamoja na mradhi ya miripuko. Kamati inaiomba Serikali kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanasababisha athari hizo kwa makusudi.

MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla kamati haikuridhishwa na ukusanyaji wa mapato kwa upande wa Pemba katika kipindi cha bajeti cha mwaka 2015/2016 ukilinganisha na Unguja jambo ambalo limezorotesha ufanisi katika utendaji kazi kupitia makusanyo hayo kwa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kamati imesikitishwa kwa ushukaji wa mapato kwa Halmashauri na Baraza la Mji Wete kutokana na baadhi ya wanasiasa kuwashawishi wananchi wasilipe kodi kitu ambacho si kizuri na kamati yangu imeona si busara kufanya hivyo kwani maendeleo yatokanayo na mapato hayo ni faida kwa wananchi wote.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa upande wa mikoa ya Pemba haikuwekewa malengo katika ukusanyaji wa mapato kitu ambacho kitarejesha nyuma maendeleo yanayopatikana kwa ukusanyaji wa mapato hayo, kwa upande wa Unguja Mikoa yote imepangiwa mapato kukusanya. Hivyo basi kamati inaishauri wizara ya fedha kuliangalia

upya suala hili na kulitafutia ufumbuzi unaofaa, kwani kwa mwaka ujao wa fedha kwa upande wa Pemba tutakua tumeikosesha Serikali Mapato yake na tukizingatia kuwa vyanzo vya mapato vipo na wahusika wataendelea kukusanya mapato hayo bila ya kuwasilisha Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kamati yangu inaishauri serikali kuweka nguvu kubwa katika uanzishwaji wa serikali za mitaa na ikiwezekana kuwe na kurugenzi mbili, moja ni kwa ajili ya uratibu wa Tawala za Mikoa na nyengine kwa ajili ya Serikali za Mitaa.

AFISI YA USAJILI WA VIZAZI, VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na mabadiliko mapya yaliyofanywa na Serikali kwa kuwekwa pamoja afisi ya usajili wa vizazi,vifo na kadi za utambulisho wa Mzanzibari kwa ajili ya kuleta ufanisi katika majukumu yao kwa vile yanalingana kiutendaji, Lakini pia kukamilisha azma ya Serikali kuwa na rikodi ya taarifa za mtu tokea anazaliwa hadi anafariki.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo kwa mwaka 2015 kwa kuanza rasmi kusajili vizazi na kutoa vyeti kwa kutumia mfumo wa elektroniki kwa Wilaya tatu za Unguja, hali ambayo kamati imeona ni vyema kuendelea kutumika kwa Wilaya nyengine za Unguja na Pemba, kwani mfumo huu utasaidia kupatikana kwa huduma hii kiurahisi kwa Wananchi na kuondokana na mfumo wa zamani ambao ulikuwa na changamoto ya kukaa kwa muda mrefu bila ya kupatikana vyeti kwa wahusika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza ofisi ya usajili na kadi za utambulisho kuendelea kuwasajili na kuwapatia vitambulisho Wazanzibari wakaazi na wasiokua wakaazi wanaoishi kisheria wenye umri wa miaka 18 na kuendelea kwa ajili ya kuondokana na malalamiko ya uchelewaji wa kupatikana kadi hizo kwa waliokua wameshafikia umri ambao kila siku wanaongezeka.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala mbele ya Baraza lako Tukufu. Pia naomba niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hasa kwa kunichagua kuwa Mbunge kupitia Baraza la Wawakilishi, Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano. Aidha nawaomba Waheshimiwa Wajumbe

waichambue, waijadili, waiboreshe na mwishowe waipitishe bajeti hii kupitia mafungu yake yote pamoja na *programme* zake ili wizara iweze kuendelea na utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza kwa kunisikiliza. Kwa niaba ya Kamati yangu naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, kwanza sina budi nitoe shukurani kwa Waheshimiwa wote kwa utulivu wenu na uchangiaji wenu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri kujibu maswali vizuri lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa kwa uwasilishaji wa hotuba yake vizuri, hotuba ambayo kuwa imejaa kila kitu. Lakini pia nimshukukuru vile vile Mwenyekiti wa Kamati naye kwa kuwasilisha maoni ya kamati yake, nashukuru sana.

Kabla sijasitisha kikao cha Baraza hili kuna tangazo kwa Wajumbe. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mnaalikwa ufunguzi wa Ijitmai ya Kimataifa itakayofanyika leo tarehe 3/6/2016 baada ya sala ya Ijumaa Kidoti, Waheshimiwa tunaalikwa na tunaomba watakaopata nafasi wahudhurie.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya tangazo hilo kwa vile muda umemaliza na hatuwezi kuendelea na kuchangia sasa hivi naomba nisitishe Baraza hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 5.47 Mchana Baraza liliakhirishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshmiwa Wajumbe kabla sijamwita mchangiaji wetu wa mwanzo napenda nitoe tangazo. Kuna kadi hizi ambazo mtapewa baadae, lakini zina kosa kidogo la tarehe. Hizi kadi shughuli yenyewe iko kesho, mualika ni Mhe. Rais lakini zimeandikwa tarehe 4 Agosti, lakini shughuli iko kesho jioni tukimaliza semina. Ahsante.

Naomba sasa nimwite mchangiaji wetu wa mwanzo Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) akifuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na uwezo wake wa kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, kwa moyo wangu wa dhati kabisa namshukuru au nampongeza Mhe. Waziri kwa dhati, kwa kazi zake nzito na juu ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa katika mazingira mazuri na salama, tunapata usingizi usiku na mchana. Kwa sababu wizara hii ni wizara tunayoitegemea kwa hali na mali kwa mambo mengi sana.

Mhe. Spika, mimi katika michango yangu nitachangia mambo manne au matano kwa ufupi sana. Kwanza nampongeza Mhe. Rais kwa uwezo wake aliopewa na Katiba kwa kuwateua Wakuu wa Mikoa wapya na wale wengine wanaoendelea, na ninaamini kwa kazi zao nzuri walizozifanya walikotokea wakiungana na wa zamani watafanya kazi kwa moyo safi na kwa uadilifu mkubwa, tunawategemea kwa uwezo wao waendelee hivyo.

Pia Mhe. Rais kwa uwezo wake aliopewa na Katiba kwa kuwateua Wakuu wa Wilaya wapya kwa wilaya mbali mbali. Hilo pia ni jambo zuri, kwa sababu tunataka twende na kazi ya maendeleo na katika mwelekeo wetu kuna msemo, "hapa kazi tu". Kwa hivyo, naamini hii ni changamoto kwa watendaji hawa wapya kuwa watafanya kazi kwa moyo wao wote.

Mhe. Spika, pia niendelee kwa Makamanda wetu wa vikosi. Makamanda wa Vikosi vyote vya SMZ pamoja na wapiganaji wetu wote hawa inafaa tuwapongeze kwa ujasiri wao, tuwapongeze kwa uzalendo wao, tuwapongeze kwa kazi zao nzito wanazozifanya.

Mwisho kabla sijaingia katika michango ya moja kwa moja kuna Waheshimiwa Madiwani wetu. Tarehe 20 Machi, 2016 ulifanyika Uchaguzi Mkuu wa marudio, na kwa bahati nzuri Waheshimiwa Wawakilishi na Madiwani wetu tulichaguliwa siku moja, lakini na mimi kwa upande mwengine jimbo langu la Kijitoupele pia siku hiyo ilikuwa ni historia ya Tanzania kwa kukamilisha uchaguzi wa Mbunge wa Jimbo la Kijitoupele, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha.Tuko pamoja tunafanya kazi zetu kwa maendeleo ya wananchi wetu na nchi yetu kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nitamuomba sana Mhe. Waziri suala la madiwani wetu hadi leo bado hawajapata uongozi wa kuongozana katika manispaa zao na halmashauri.

Namuomba sana Mhe. Waziri akija hapa atupe maelezo ili madiwani wenyewe wajielewe.

Pili wananchi wanaowategemea katika wadi zao pia waelewe hawa watu wako katika ngazi gani na mwelekeo gani ili kukamilisha taratibu hizo za kufanya kazi kwa mujibu wa Katiba na sheria zetu. Namuomba Mhe. Waziri Waheshimiwa Madiwani ni chachu ya maendeleo katika wadi zetu, naamini Mwakilishi au Mbunge hana uwezo wa moja kwa moja kufanya kazi zake bila ya kushirikiana na madiwani wetu. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri hili aje atupe maelezo, tuhakikishe kwamba watu wetu hawa wako vipi na wanaendelea vipi na kazi zao siku hadi siku.

Mhe. Spika, suala jengine naipongeza sana serikali kutokana na uendeshaji mpya uliojitokeza katika nchi yetu. Kwanza katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi kuwa na manispaa tatu. Hili suala ni zuri na lina kila hadhi, kwa sababu wingi wa wananchi wanaoishi katika Mkoa wa Magharibi unatosheleza kwa wilaya zote tatu kuwa na manispaa. Kwa hivyo, nawapongeza katika Wilaya yangu ya Magharibi kuwa na manispaa ya Magharibi 'A' na Magharibi 'B', lakini pia katika mwelekeo wa utekelezaji mzuri ambao tunautegemea wautekeleze, na mimi nitatoa wito baadae niwape njia ya kukusanya mapato.

Kwanza kwa Wilaya ya Magharibi 'A'. Ukurasa wa 14 na 15 kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi katika Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Baraza la Manispaa Magharibi 'A' limepangiwa kukusanya jumla ya shilingi 500 milioni. Hii napongeza kwa dhati kabisa, na pia ningesema kidogo, kwa sababu bado kuna mianya mingi inaweza kuachwa hapo tukakosa pesa hizo, lakini waongeze nguvu zipindukie pesa hizo, shilingi 500 milioni kwa Wilaya ya Magharibi 'A' mimi naona kidogo. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri hiyo rai nitayoitoa hapa kwa Waheshimiwa madiwani wataohusika baadae wafanye kazi ya ziada kupata mapato hayo.

Kwa upande wa Magharibi 'B', kwa mwaka wa fedha 2016/2017 wamepangiwa ukusanyaji wa mapato katika manispaa yetu bilioni moja. Napongeza, na bilioni moja hii kama nitatoa rai inaweza kuongezeka. Kwa mfano, ukusanyaji wa mapato katika baadhi ya maeneo kuna mianya tumeiachia. Kuna viwanda vidogo vidogo vingi sana mapato hayakusanywi.

Sasa hivi katika nchi yetu kuna wajasiriamali wengi wanajiendesha wenyewe katika viwanda vidogo vidogo. Viwanda vidogo vidogo vina pesa kuliko hivyo vikubwa, wanaotengeneza milango ya ma-*grill* wengi sana. Mimi nawapongeza sana kwa juhudi yao hiyo, lakini wengi ukitembelea katika kudadisi leseni

hawana. Kwa hivyo, niziombe manispaa zetu kupitia Waheshimiwa Madiwani wetu katika maeneo yao humu waendelee kutafuta ukweli ulivyo, ili fedha zipatikane kwa maendeleo ya manispaa zetu pamoja na wananchi wetu.

Mhe Spika, uzoefu uliokuwepo na ndivyo ilivyo fedha hizi zikipatikana zinasaidia katika majimbo yetu. Kwa mfano, nitamuomba Mhe. Waziri baadae. Katika majimbo haya kuna maeneo mbali mbali yana matatizo mengi; ukosefu wa barabara za ndani, manispaa au halmashauri huwa ni kazi yao. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri pamoja na juhudi hiyo lakini naomba waongeze bidii ili tupate fedha hizo kwa kusaidia maendeleo ya maeneo yetu katika majimbo yetu.

Mhe. Spika, mimi katika Jimbo langu la Kijitoupele kuna maeneo mengi yana adha ya usafiri, na usafiri huu unatokana na kushindwa kupitika kwa barabara za ndani, lakini kwa bahati nzuri Magharibi nimezungumza mapema ina watu wengi kuliko wilaya nyengine na mikoa yote katika Zanzibar hii Unguja na Pemba. Kwa mfano, barabara yangu ya Mshelishelini mpaka mwisho ukizunguka mpaka Taveta ni barabara muhimu sana, wananchi wanapata shida usafiri mgumu. Nimuombe sana Mhe. Waziri kupitia manispaa yetu hizi barabara zitiwe fusi, zikitiwa fusi wananchi watapata raha na usafiri wa uhakika, ili kunusuru mambo yao na biashara zao hata kama kuna mzazi au mgonjwa atapata nafuu ya usafiri.

Jengine kuna watu katika Baraza wananambia Mhe. Shihata huko Kwarara Madina kuna nini? Maana sina siku nisiyouliza swali Kwarara Madina. Mhe. Spika, nilipokwenda kuomba ridhaa mimi, Mbunge na Diwani wetu tulipata kero ya mwanzo kwa wananchi wetu mambo mawili kwa matatu makubwa.

Kwanza barabara hawana, Madina walikuwa wanatumia barabara kwa gari la ng'ombe, ni hatari. Akiweko mzazi, mgonjwa, mtu tu hajiwezi hafiki maana daladala huko haziendi kabisa mpaka leo. Lakini kama Mwakilishi wa wananchi wa jimbo hilo nitawaomba madereva kuanzia muda wowote tutaokutana mimi na wao sasa hivi wafike Madina kwa njia yoyote, kwa sababu barabara inapitika, tumeipiga *grader* na Mhe. Mbunge inapitika haina wasi wasi.

Mhe. Spika, jengine niiombe serikali pia kupitia Manispaa yetu tumeanza kuweka fusi katika maeneo yale yenye mashimo makubwa, tumepiga *grader* gari zinapita za aina zote, lakini kama hatukuweka fusi basi huko mbele tutashindwa safari baada ya kutokea mvua.

Tumeanza mimi na Mhe. Mbunge tunaendelea vizuri, na tunaiomba manispaa yetu baadae tuungane nayo katika utekelezaji wa barabara hii kutoka Kwarara Meli Tano mpaka Madina.

Mhe. Spika: Dakika mbili zimebaki Mheshimiwa.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Spika, dakika mbili zangu za mwisho nawapongeza kama nilivyotangulia kusema vikosi vyetu vya SMZ kwa kazi nzuri wanayofanya, lakini namuomba Mhe. Waziri kuna wito ulitoka kwa Mhe. Rais na naamini haujasahaulika na unapoahidi huwa ni deni. Sisemi kwamba limesahaulika, limo, kwa sababu serikali imetangaza kima cha mishahara kwa hivyo na kwa vikosi vyetu nawaombea sana askari wetu waongezwe, lakini wakiongezwa pesa wazipate. Kwa sababu tunaambiwa katika maelezo ya hapa na pale kuna baadhi ya viongozi wajanja huwa wanawakata makato ambayo hayaeleweki.

Nimuombe Mhe. Waziri hili akilitaka mimi na yeye tu naweza kumpa taarifa hiyo kwa kuzingatia kwamba vijana wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu, kile wanachokipata wapewe ili waendeleze maisha yao.

Bahati nzuri mimi nilikuwa askari lakini nilikuwa najua kazi yangu moja tu, mimi mwanajeshi, kutembea kwangu mwanajeshi. Kwa hivyo na yeye askari kazi yake moja tu kulinda nchi yetu na mambo mengine yanayostahiki. Kwa hivyo, kile alichopangiwa akikipata kitamuendesha katika maisha yake.

Mhe. Spika, baada ya hayo, kwa kuwa muda mdogo, nasema tu kwamba naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja, mimi na wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii lakini kabla ya kuendelea ningeomba kutoa hoja ya kutenga kanuni kando, kanuni ya 58(6). Hii kwa kweli Wajumbe tuliombwa dakika 15 kujadili kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tupu, sio wizara nyengine yoyote.

Kwa maelezo zaidi tulielezwa kwamba, hoja ya kutenga kando Kanuni ya 58(6) Mhe. Mwanasheria Mkuu huyo.

"Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndiye mwenye hoja hapa iliyoko mbele..."

Hii tuliikubali kwa sababu ya Mhe. Balozi tu Ofisi yake ya Makamu wa Pili aliomba. Dakika 15 Mhe. Spika, mimi hazinitoshi nataka angalau 30 au 40 kama za mwanzo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa hoja yako Spika haikubali, tulivyotengua ile kanuni ilikuwa kwa bajeti nzima haikuwa kwa bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ni bajeti nzima. Tumefanya hivyo ili watu wengi zaidi waweze kuchangia Mheshimiwa, kwa hiyo nakuomba usiupoteze muda wako bora nenda kwenye mchango tu moja kwa moja usiende huko.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, nakubaliana na mawazo yako mazuri lakini kutokana na hizi wizara ni muhimu sana.

Mhe. Spika: Mheshimiwa kiti hubishani nacho, endelea kuchangia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante naheshimu kiti. Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima kila siku na kunijaalia kuweza kufika kwa salama.

Vile vile niwapongeze viongozi wote wa Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kutuletea hotuba yao nzuri, lakini kwa kuwa sisi Wawakilishi tuna maoni na michango yetu. Mimi kabla ya kuanza mchango ningeomba sana tuwasifu upande fulani, kwa sababu tunao viongozi Makamishna wa Vikosi wanajitahidi kufanya kazi nzuri.

Vile vile kwa ujumla nawapongeza sana Makamishna wa vikosi vyote kwa kufanya kazi nzuri sana, nampongeza sana Meya wa Mji wetu wa Zanzibar nzima kwa kufanya kazi nzuri sana na watendaji wetu wote.

Mhe. Spika, kwa kuwa hakuna muda na hoja nilizokuwanazo sijui hata nianze ipi kwa sababu zote naona zina umuhimu, isipokuwa nitaanza na ajira. Ajira ni kitu muhimu, na kwenye uamuzi wa ajira nahisi watu wengi sana nje wanalalamika na wanahisi kama wanatengwa au wanabaguliwa labda kwa sehemu waliyotokea au kwa njia yoyote ile. Sasa mimi ningeomba nimuulize Mhe. Waziri atapokuja aje anijibu kwenye suala la ajira, ndani ya miaka mitano hii katoa ajira ngapi kwenye vikosi vyake Unguja na Pemba.

Vile vile ningekwenda kwenye suala la mapato. Kwa kweli upande wa Kaskazini mwaka 2014/2015 Makadirio ya Mapato yalikuwa shilingi 295 milioni, Matumizi ya Kawaida shilingi 150 milioni na Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo ni shilingi 136 milioni. Hii kwa upande wa Kaskazini. Lakini

cha kushangaza kwamba kazi zilizofanyika mimi sizioni, na katika kusoma nimeona wameandika wamefanya maendeleo Kaskazini lakini maendeleo yenyewe wamenunua gari, wametengeneza Ofisi ya Halmashauri, wamesema pia wamesaidia Miradi ya Maendeleo ya Wananchi na wametoa posho la nguo za madiwani. Lakini mimi nina maswali yangu ningeomba kumuuliza Mhe. Waziri, gari hii ilinunuliwa shilingi ngapi, matengenezo ya Ofisi ya Halmashauri zilitumika shilingi ngapi, vile vile ningetaka kujua katika haya maendeleo yaliyozungumzwa waliyofanyiwa wananchi ni yepi na wamepewa wapi na wapi.

Mhe. Spika, pia ningependa kujua hiki kima wanachopewa madiwani cha posho yao ya nguo; wanapewa shilingi milioni moja, elfu kumi au laki tano? Ningependa kujua vile vile ili nikaridhika na majibu yake.

Mhe. Spika, kwa kweli madiwani wanasema wenyewe wananing'inia hawajijui wako dunia gani, wanasema kabisa wako tafrani kweli kweli. Madiwani wapo tu sasa hivi hawajui baba yao nani mama yao nani, hawajui hata waanze wapi. Mimi mwenyewe madiwani wangu wapo tu utafikiri mayatima.

Mhe. Spika, ningeomba sana tuje tupate ufafanuzi mzuri wa madiwani kwa nini mpaka hii leo hatua hazijachukuliwa ambazo wanatakiwa wapewe za kuanza kazi pamoja na wale ambao wanatakiwa kuteuliwa wateuliwe na kutafutwa wenyeviti.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia sehemu ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kaskazini, imeshazungumzwa tayari ni wizara hapo kwa niaba yake. Ningeomba Mhe. Waziri angekuja kunihakikishia.

Mimi wakati nafunga kampeni zangu za Chama changu cha Mapinduzi Mhe. Babla kwa umaarufu, alikuja na akajinadi kwenye soko la Kinyasini akasema kwamba Halmashauri yake na mpaka Waziri anajua na pesa zimeshatengwa za kujengwa soko la ghorofa. Sasa ningeomba kumuuliza Mhe. Waziri hii kauli ya mwenyewe Babla au amemtuma au Halmashauri imemtuna, na kama hajatumwa alizungumza kwa mambo yake mwenyewe binafsi ya kufurahisha watu.

Basi Mhe. Spika, huyu mtu moja kwa moja hafai kuwa Mwenyekiti wala hafai kuwa katika kazi kama zile, kwa sababu atakuwa anazungumza uongo kama kazungumza yeye. Kama kazungumza ukweli basi nitamuomba Mhe. Waziri anambie lini soko lile la Kinyasini aliloliahidi Mhe. Mwenyekiti wake kwa niaba yake lini litajengwa. hilo swali langu jengine.

Mhe. Spika, vile vile ningeenda kutoa mchango wangu kidogo tu wa vikosi. Kwa kweli kuna Vikosi vya KMKM, JKU, Zima Moto, Mafunzo na Vikosi vya KVZ. Ningependa kutoa mchango hivi vikosi vizuri sana. Kwa kweli hasa upande wa KMKM, KMKM wanahitaji vifaa vizuri katika kwenda kusimamia magendo.

Ningependa kujua Mhe. Waziri hawa KMKM kawapatia vifaa gani vya kuzuia magendo au boti za aina gani wanazo, wanazo ngapi na zina nguvu gani za kukamata watu au zina *speed* gani zinaweza kutembea baharini.

Vile vile ningeomba kutoa maelezo kwa sababu kuna Vikosi najua kuwa Viongozi Wakuu wanakuwa hawana matatizo, mara nyingi wale wakuu kama Kamishna na wengine. Lakini watendaji wa chini baadhi yao sio wote, na baadhi ya sehemu huwa wana matatizo, yaani imefika hatua JKU au KVZ wale wanaopita doria huwa wao wanajifanya wakubwa kuliko Majeshi wenyewe wa JWTZ.

Mhe. Spika, nitatoa mfano mdogo tu hivi sasa vikosi vile baadhi yao vinatolewa kwa makundi vinapita baadhi ya maeneo mjini na sehemu nyenginezo, badala ya kufanya kazi waliyopewa ya kulinda ya kutafuta wahalifu wanabaki kusimamisha vespa na gari, na cha kushangaza zaidi wanafika mpaka kuwapiga bambasachi watu wakiwa wako sehemu mbaya, wanawanyang'anya simu na vitu vyengine.

Mimi nina ushahidi kamili nitatoa mfano mmoja tu kipindi cha nyuma mdogo wangu binafsi baba mmoja mama mmoja Msikiti wa Forodhani, na natoa hii kwa maana nataka niwaeleweshe viongozi wajue wale waliowapa kazi baadhi yao hawana utendaji waliowapa.

Hapo nitatoa mfamo mdogo tu walimsimamisha kwa sababu ya leseni na matokeo yake wakamvamia wakampiga na kesi iko Madema na simu wamemnyang'anya.

Baada ya mimi kwenda kule nikafuatilia wakageuza kibao wakasema kuna ushahidi wanataka kuangalia wamepigwa pichwa. Hata kama wamepigwa picha si wamefanya makosa ambayo hayatakiwi kwa nini kusiwepo ushahidi lakini naizungumza kwa ufupi huu natoa mfano mdogo tu. Vile vile ningeomba wafahamishwe zaidi, wachunguzwe, kwa sababu kazi waliyopewa ni kwenda kutafuta ulinzi sio kusimamisha vihonda au kukera watu au kuwanyang'anya watu vitu.

Mhe. Spika, inasikitisha sana wakubwa wao ni watu wazuri sana, wanawafundisha vizuri sana wanawagharamikia lakini na wao wanawatia ila. Na hili mimi nimesema lazima nitalizungumza niwajuilishe, kwa sababu naamini mambo mengine hawayajui.

Vile vile jana nakupa mfano mdogo tu nimekwenda *airport* mwenyewe juzi nimepita kwa miguu pale, wamenisimamisha wakanambia hii sehemu hairuhusiwi kutembea kwa miguu, nikawaambia bango linasema gari sijaona bango linalosema mtu hatembei kwa miguu. Kuna yule aliyenisimamisha wakaanza kuropokwa wengine pale wako kama wanne wamekaa kwenye mti, wanasema mgaragize huyo, mmwagie maji, kama mara tatu wakazungumza kauli ambazo sio za kinidhamu katika kazi.

Naomba sana Mhe. Waziri akae na vikosi tena na Waheshimiwa Makamishna wawaeleze vizuri nidhamu za kazi ni zipi hasa za Polisi.

Mhe. Spika, imefika hatua wamekuwa tena kuna baadhi ya mambo wanafanya mpaka yanakirihisha, huo nimetoa mfano ili wakawafahamishe zaidi, wafanye kazi inayostahiki sio kufanya kazi ya kunyanyasa watu na kuwaibia watu vitu. Sio wote, ni wale ambao wanatembea Mji Mkongwe ndio wanaofanya hivyo na hapo *airport*. Mengine ninayo lakini nayaacha kwa sababu muda mdogo sana.

Mhe. Spika, mimi chengine kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Mhe. Spika, nimekuta wizara hii inashughulika pia na mambo pia ya barabara kutia vifusi na mambo mengine. Mhe. Spika, mimi nahisi Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu tunayo, sasa nikaona na humu pia wanatengeneza barabara.
Lakini nitamuomba Mhe. Waziri aje anijibu wizara yake inahusika vipi na kutengeneza barabara wakati Wizara ya Mambo ya Miundombinu na Mawasiliano tunayo. Sijui inahusika vipi masuala haya, nakuta hapa kuna sehemu barabara ya Muembe Kisonge, Kikwajuni, Miti Ulaya yote imeshughulika na wizara hii. Sasa ningeomba anieleze kwa nini wizara yake pia inahusika na mambo ya kujenga barabara.

Mhe. Spika: Mheshimiwa Mjumbe una dakika mbili.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, ningekuomba sana dakika tano kama utaweza kunipatia.

Mhe. Spika, naingia kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti vile vile suala la *CCTV*. Mhe. Spika, suala la *CCTV camera* mimi nilikuwa silifahamu lakini kwa kusoma ndani nimeona kwamba hili suala la *CCTV camera* zimepangwa

ziwekwe Mji Mkongwe, Bandarini, Uwanja wa Ndege na baadhi ya njia kuu za maeneo ya Wilaya ya Mjini.

Mhe. Spika, hizi pesa bilioni kumi na nane za *camera* ni nyingi sana kwa *project* hii. Ningemuomba sana Mhe. Waziri aje anijibu maswali yangu yafuatayo kuhusiana na suala la *camera*.

Suala la kwaza kampuni gani ambayo wameipa kufunga hizi *camera*, zimekuja ngapi na hiyo iliyowapa kufunga hizo *camera* wamewapa kwa *grade* gani au wamewapa kwa *specification* gani. Kwa uzoefu gani hata wakawapa, hilo swali langu la kwanza.

Pili *project* yote hii ya kufunga *camera* nataka kujua *camera* ngapi ambazo zitafungwa ndani ya mji wote uliopangwa kufungwa *pieces* ngapi na za aina gani, nafikiri hilo swali langu la pili.

Swali langu la tatu ningeomba kujua vile vle hizi *camera* zina uwezo gani, zina *mega pixels* ngapi katika uchukuaji wake wa *camera* na zina *size* gani ndani yake kama inazunguka au ya kukaa tu hivi hivi, ningependa kujua vile vile.

Swali langu la nne ningeomba sana kumuuliza Mhe. Waziri vile vile aje anieleze kabla ya kuwapa tenda hii kampuni, kiasi gani cha fedha kimetumika kwenye kufanya utafiti kwa kuweka hii miundombinu ya *camera*, wamelipwa shilingi ngapi kwa kuweka hivi vifaa vya *camera*.

Swali langu la tano ningemuomba Mhe. Waziri aje anijibu hizi *camera* zilizofungwa ni za nchi gani; za China, Marekani, au Canada? Mimi maswali yangu ni hayo. Kwa sasa hivi ningemshauri vile vile aliomba bilioni kumi nafikiri kuna bilioni moja na milioni ishirini na nne zishatolewa.

Lakini kama sijapata maelezo au majibu ninayoyataka mimi, nikayafahamu, mimi kwa sasa hivi siungi mkono hoja nasubiri majibu yangu itakapokuja kifungu.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri katika ofisi hii.

Mhe. Spika, nitangulize kutoa shukurani kwa Mhe. Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba hii. Hotuba ambayo imepangika na alikuwa na ufasaha mzuri na alitumia muda mfupi, nimpongeze sana. Alikuja na *style* mpya.

Vile vile niwapongeze watendaji wake wote wakiowemo Makamishna wa vikosi. Nichukue fursa hii vile vile kuipongeza Kamati ambayo imewasilisha ripoti yao yenye kuhusiana na ofisi hii ambayo imewasilishwa na Mhe. Machano Othman Said.

Kwa kweli ripoti yao ilisheheni maoni, na kama laitani maoni yale yatachukuliwa na Mhe. Waziri basi utendaji katika bajeti utakuwa ni mzuri sana. Niipongeze sana Kamati inayohusika.

Vile vile niwapongeze Waheshimiwa wenzangu wote ambao wametoa michango yao mizuri katika kuifanya hotuba hii ya Mhe. Waziri kuwa bora zaidi. Nivipongeze vile vile vikosi vya SMZ katika wakati wote wa harakati za Kampeni na Uchaguzi Mkuu ule wa awali na ule wa marejeo katika kuweka amani na utulivu katika nchi yetu hii. Mhe. Spika, mimi katika hotuba hii nina mambo machache mno.

La kwanza nakuja katika Idara ya Uratibu wa Idara Maalum. Mhe. Spika katika kitabu hichi cha bajeti kimetuonesha kwamba katika idara hii mwaka 2015/2016 iliidhinishiwa wastani wa shilingi milioni hamsini na tatu laki nane thamanini na tatu. Lakini ilikadiriwa kutumia shilingi laki nane na thamanini na tatu.

La kusikitisha sana Mhe. Spika, kwamba idara hii iliingiziwa shilingi milioni tatu laki tano tisini na tatu tu ambayo ni wastani wa asilimia nane. Hii inasikitisha sana, mimi sijawahi kuona bajeti zote duniani kuona kwamba Idara au Taasisi inayohusika imetengewa pesa halafu ikapata asilimia nane ya matumizi. Ukizingatia kwamba idara hii ndiyo inayoratibu, vikosi vyote vya SMZ vinaratibiwa hapa, hizi ni pesa kidogo sana.

Ni pesa kidogo lakini ukitizama katika taasisi nyengine pesa zilizotumika ni wastani wa asilimia 73 na wengine wana 118. Hii inasikitisha na naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja aitolee maelezo kwa nini idara hii ilipata asilimia nane katika matumizi yake. Inasikitisha sana zitaendaje kazi haziwezi kwenda hii ni idara ambayo inaratibu. Hawa wote wanategemea uratibu kutoka katika idara hii.

Mhe. Spika, nije sasa katika suala la ajira kwa vijana. Mhe. Spika, afisi hii ni afisi ambayo ina vikosi ikiwemo JKU. Vijana wanaingia JKU kwa mujibu wa sheria ili kujenga taifa, lakini vile vile kwa kupitia Serikali ya Muungano vijana wa Zanzibar wanapata fursa ya kwenda JKT. Vijana hawa baada ya kumaliza muda wao na ikiwa hawakupata ajira wanarudi mitaani.

Mhe. Spika, zinapotokezea ajira zinahusiana na Mambo ya Ulinzi tatizo linalokuja ni malalamiko matupu kwa sababu vijana wale ambao wamepitia makambini na ambao tayari wameshafundishwa mambo ya ulinzi unakuta hawapati fursa hizi, na baada yake wanachukuliwa vijana wengine ambao ni watu wa kulea tu majumbani ambao hawajapitia katika vikosi hivyo.

Na hivi sasa Mhe. Spika, wasi wasi mkubwa sana upo kwa vijana ambao tumeshawapa *training* za uaskari na hivi sasa kuna vikosi vya *Al-shabab*, vya *Islamic State* vinawatafuta sana vijana hawa ambao tayari wameshapikwa wao wanaenda kuwafinyanga tu kidogo. Kwa hiyo, niishauri sana serikali zinapotokezea ajira zinazohusiana na ulinzi basi vijana hawa waliomaliza JKT na waliomaliza JKU wapewe kipaumbele sana kuliko wale ambao tunawachukua tu majumbani kutokana na nafasi zetu au kutokana na ushemegi na urafiki.

Mhe. Spika, niendelee sasa katika Afisi ya Usajili wa Kadi za Utambulisho. Afisi hii Mhe. Spika, ina wajibu wa kusajili na kuwapatia vitambulisho Wazanzibari Wakaazi na wasio wakaazi wanaoishi kisheria wenye umri wa miaka 18.

Imeeleza ripoti kwamba kwa mwaka 2015/2016 Afisi hii imesajili Wazanzibari Wakaazi 8691, lakini hakuna *data* inayoonesha wale ambao wasiokuwa wakaazi wanaoishi kisheria. Ningependa sana tupate *data* hiyo ili kuweza kuwajua wao walikuwa ni wangapi. Vile vile katika hili hawa watu wanaosajiliwa ambao sio Wazanzibari wanaoishi hapa kunakuwa na vigezo gani vya kuweza mpaka kuwapatia vitambulisho vyetu vya Mzanzibari.

Mhe. Spika, nije sasa suala la makaazi ya askari wetu hawa wa vikosi vya SMZ. Mhe. Spika, ni aibu makaazi ya askari wetu kwa kweli hayaridhishi, nyumba nyingi sana ni mbovu hususan vikosi hivi vya Magareza au tunaita Chuo cha Mafunzo. Unapotembelea katika maeneo yao basi hizi nyumba ni aibu kukaliwa na askari, yaani hata wale wafungwa basi huwa wanawacheka askari wao jinsi wanavyoishi. Utakuta familia moja inaishi katika chumba kimoja mtu na mke wake na watoto humo humo halafu nyumba yenyewe hairidhishi.

Mhe. Spika, nimuombe sana Waziri kwa sababu katika bajeti hii sikuona kama kuna eneo ambalo linaonesha kwamba kutakuwa na ukarabati au ujenzi wa nyumba mpya za maaskari hawa, askari hawa wanafanya kazi ngumu, kwa hiyo lazima tuweze kuthamini kazi zao. Nimuombe sana, halafu tukizingatia kwamba kikosi cha Mafunzo kina kitengo cha ujenzi kwa nini kisitumike katika kuona kwamba tunaziboresha nyumba zao.

Mhe. Spika, katika idara hii hii ya Mafunzo au Vyuo vya Mafunzo miongoni mwa malengo na majuku ya Vyuo vya Mafunzo ni kuweza kurekebisha tabia za wale ambao wameingia pale kwa makosa mbali mbali. Na inaelezwa kwamba mule wanafundishwa kazi mbali mbali za amali lakini vile vile na mwendo mzuri.

Mimi ni mjasiriamali huwa natoa mafunzo katika masuala haya ya ufundi, na vijana wanapotoka pale huwa nafanya *follow up* kuweza kuona yale waliyojifunza wanatumia vipi.

Labda ningependa tu kujua ufafanuzi, kwamba hawa vijana wetu waliofanya makosa mbali mbali wanaoingia katika Vyuo vya Mafunzo wakishatoka pale chuo au uongozi huwa una utaratibu gani wa kufuatilia mienendo yao kama inaweza kurekebishika au vile vile zile kazi za amali ambazo wamewafundisha huko walikokwenda wanazitumia, kwa sababu lazima uweze kufanya ufatiliaji na tathmini hatimaye ndio utajua kwamba kazi wanayofanya inatekelezeka vizuri, na hiyo ndio ambayo itatuhakikishia sisi kwamba vijana wanaopita Vyuo vya Mafunzo kwa makosa mbali mbali wanarekebishika na wanaweza kufuata yale mafundisho ambayo wamepewa.

Mhe. Spika, nije sasa katika suala zima la Mstahiki Meya. Mstahiki Meya ni mtu mkubwa sana. Katika nchi mbali mbali duniani Mstahiki Meya ni mtu muhimu sana. Lakini la kusikitisha sana Mstahiki Meya wetu, watu au Mawaziri huwa wanagawana magari mazuri mazuri lakini Mstahiki Meya wetu gari yake haiendani na hadhi ya Ustahiki Meya.

Wakati mwengine hata katika misafara mikubwa basi kama si ile bendera basi utaweza kusema labda kachapia tu msafara. Ningependa sana tumtizame sana Mstahiki Meya hususan tayari tunaingia katika masuala mapya haya ya kuwa na Mameya nafikiri watakuwa zaidi ya mmoja. Kwa hivyo, tuliangalie sana na tumtizame sana Mstahiki Meya wetu ili aendane na hadhi ili alau anapoenda duniani akikutana na Mameya wenziwe basi ajisikie kwamba na yeye ni Meya katika nchi hii.

Mhe. Spika, mimi sina mengi sana ya kusema, hayo machache yanatosha lakini nina imani sana kwamba yanaweza kusaidia katika hotuba hii. Nimshukuru sana Mhe. Haji Omar Kheri kwa uwasilishaji lakini vile vile niushukuru utawala mzima wa Afisi hii kwa kuweza kuwasilisha hotuba hii.

Nitamke rasmi kwamba mimi pamoja na michango hiyo basi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi. Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said akifuatiwa na Mhe. Hidaya Ali Makame na Mhe. Salum Ali Haji ajiandae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Spika. Nilikuwa na ombi kidogo Mhe. Spika, zile dakika tano zako ninaziomba kama inawezekana.

Mhe. Spika: Hapana Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika. Mimi Mhe. Spika, nilikuwa ninahitaji kama saa moja. Kwa hivyo itabidi niende kwa haraka.(*Makofi*)

Sasa nitamuomba Mhe. Waziri na watendaji wake washike kalamu zao ziwe mikononi mwao ili ninachowauliza tusije tukagongana katika mafungu. Nitahitaji majibu mazuri ili tusije tukashikana huko mwisho. (*Makofi*)

Nianze kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu Mhe. Spika, kwa kuwashukuru wote na kuwapongeza wote ambao waliochaguliwa humu ndani pamoja na kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Mapinduzi. Lakini nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri leo asubuhi na amezungumza kwa utaalamu na yeye ni mtaalamu na mzoefu, na sisi tunamuona kama *senior*.

Niwapongeze Wakuu wa Mikoa wote waliochaguliwa hivi karibuni na niseme tu kwa Mhe. Waziri kwamba Wakuu wa Mikoa waliochaguliwa hivi sasa, kwa Kiingereza wanasema hii ni *Dream Team*. Yaani hawa ni watu ambao ni mahodari kwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini ni jembe, ana uzoefu, hodari na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi Ndugu Ayoub ni hodari, mtiifu. Kijana mwenzetu na ninaamini atasaidia mukiwa pamoja na daktari wetu Mkuu wa Mkoa wa Kusini Dkt. Idrissa, kwa kweli wote hawa safi kabisa.

Nimpongeze na Mkuu wetu wa Wilaya ya Kati Mhe. Sukwa kuletewa jembe, ninawaaminia akinamama. Huyu ni mfano. (*Makofi*)

Sasa nianze kwenda kwenye hoja zangu. Mhe. Spika, jambo la kwanza nitaanza na suala la Mji wa Zanzibar, ninataka kujua katika huu mpango mzima. Je, utakuwa katika mfumo wa *Metropolitan City* ambapo hili eneo Mhe. Waziri anazungumzia itakuwa inafanya kazi kuhudumia na hizi manispaa au inakwenda kwa mfumo gani.

Suala langu la pili ni kuhusiana na JKU. Nilitaka kujua hawa JKU kwa kweli ni watu muhimu sana na wanaweza wakafanya mambo ya maana makubwa sana katika nchi yetu kwa kuweza kutusaidia. Sasa nilikuwa na wazo moja labda Mhe. Waziri anaweza akalifikiria na akalichukua kwa mfano kuna eneo hili la Karakana hapa Mbweni. Ninatambua kwamba magari mengi ya serikali sasa hivi yanatengenezwa upande wa Toyota. Lakini hapa hapa Chuo chetu sisi cha Elimu cha Karume ambapo kipo chini ya Wizara ya Elimu na hili eneo la Karakana (Matrekta) lipo chini ya Wizara ya Mawasiliano.

Sasa kama kuna uwezekano eneo la Karakana pakajengwa na *garage* ya kisasa ambapo hawa JKU wakatumika kuchukua hawa vijana wanafunzi wanaomaliza Chuo cha Karume, ili kufanya kazi ikawa *garage* ya maana. Lakini pia katika masuala ya *mechanical engineering, electrical engineering, refrigeration* na *marine service.* Yote tunaunganisha sehemu tatu lakini Karakana kuna eneo sasa hivi limekuwa ni tupu. Yaani ukiliona, unaona kama vile ni binadamu kama amekufa anatembea. (*Makofi*)

Sasa naona nafasi tuitumie. Lakini pia nilikuwa ninataka kujua kwenye Chuo cha Mafunzo ni utaratibu gani unaotumika kwa hawa wafungwa kwenye kuwaendeleza katika maeneo tofauti, pale wanapotoka kwa sababu hiki Chuo sasa hivi kinaendelea kinachukua *remandees,* sijui kama hawa *juveniles* wanapelekwa wapi, hawa vijana lakini pia wale wanaofika ambao wanafika kati ya miaka ishirini na ishirini na tano wana makosa wanapelekwa wapi. Kama wanapelekwa Mafunzo, nina taarifa zaidi kuhusu Chuo cha Mafunzo za kina.

Kuhusiana na Zimamoto. Hilo litakuwa ni la nne. Nilikuwa ninashauri pia kwa upande wa Zimamoto. Kwanza *number* yao ya 114 ambayo ni *number* ya uokozi, haijulikani. Mhe. Waziri achukue juhudi kuhakikisha kwamba wananchi wote wa Zanzibar wanaitambua hii number.

Pia, ni utaratibu gani unaotumika kuwaunganisha upande wa Zimamoto pamoja na Idara ya Maafa.

Pia nilitaka kujua wakati wa *Mv. Spice Islander* ilipozama wawekezaji wengi walijitokeza kwenda kusaidia pamoja na maafa mengi yanapotokezea wakati wa ajali za moto zinapotokezea kwenye maeneo tofauti. Ni utaratibu gani ambao ulikuwa unatumia Zimamoto kuwashirikisha jamii kwa ujumla katika kusaidia. Pia ninataka kujua ndani ya Zimamoto je, kuna mfanyakazi yeyote anayetoka katika eneo la Mji Mkongwe. Kwa sababu kunapotokea dharura wanakuwa hawazijui njia. Nimeshuhudia mimi mwenyewe. (*Makofi*)

Kwa upande wa Manispaa. Taka nyingi zinazotumika kupelekwa katika majaani; Kwanza ninataka kujua wale madereva wanaoendesha yale magari, wanaendesha kwa kasi sana. Wametumwa wafanye hivyo au wanafanya makusudi. Lakini je, magari yao yale yana *insurance* kwa sababu bei zake ni kubwa sana.

Lakini hapa nilitaka kujua suala la taka, hili litakuwa ni la sita. Taka zote zinazotupwa sasa hivi hapa Zanzibar, hatuchagui baina ya vigae, betri, uchafu wote unaingizwa kwa pamoja na unachomwa moto. Hizi taka ni nyingi sana pamoja na *oil* chafu. Hizi zinawezekana zikaishi kwa miaka ya mbele, zikashuka chini kwenye *water table* kwa sababu mvua zinanyesha na Zanzibar ni kisiwa ambacho ni *coral.* Ni mpango gani ambao wizara yake imejipanga kuhakikisha kuwa maji katika vizazi vijavyo yatakuwa yapo salama. Kwa sababu sisi tunakaa hapa tunachoma moto taka juu lakini zinashuka chini, zinaelekea kwenye *water table*. Kwa hivyo ninahitaji maelezo ya kina sana katika eneo hili. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia ninamshauri kama inawezekana aangalie kwa mfano Mbeya kuna jaa linaonesha ambapo Serikali pamoja na mradi wa *World Bank*. Je, ana taarifa nalo na amechukua watu wake kwenda kujifunza kule. Pia nilikuwa kujua katika mpango mzima wa *ZUSP* ambao ni wa *World Bank* katika mipango yote kama mfano wa ukuta ule wa Mji Mkongwe, ninafikiria kuondoa maji Mnazi Mmoja na mambo mengine. Lakini pia katika hizi nguzo za umeme, ni mkakati gani wa kibiashara Baraza la Mji na Manispaa zake zimejipanga kuhakikisha kwamba zitakuwa endelevu na hayo matangazo tutakayoyapata ni kiasi gani na hizi fedha zitakwenda wapi. (*Makofi*)

Suala la Daladala na vituo. Hili jambo linanikera sana. Madaladala yanasimama maeneo yoyote ya mjini. Imekuwa ni hatari kwa wananchi, wanapata tabu, watoto wachanga kila maeneo. Mvua juzi zimenyesha wananchi wameathirika

vibaya sana. Ni mpango gani ambao wizara yake inachukuwa inayohusu vituo vya daladala hasa katika kituo cha Daladala cha mjini na maeneo yote. Lakini ninataka kujua katika mwaka, ijapokuwa haitowezekana. Je, ana mpango gani wa kuhakikisha kwamba kutakuwa na vituo vya Daladala Unguja na Pemba kote. Kama hatojenga vibanda vya Daladala ambavyo vitakuwa vina vivuli na mvua. Je, ataweza kuweka japo *sign* kwamba wananchi na daldala waadilifu wanasimama hapa. (*Makofi*)

Pia nataka kujua kuhusu soko la Saateni; maendeleo yake, mapato yake na mpango gani unaotarajiwa pale kuhusu miaka ya mbele na faida gani zinapatikana. Kwa sababu pakinyesha mvua panaonekana yaani ni eneo lisiloridhisha.

Pia ninataka kujua masuala ya Halmashauri ya *double licenses. Licenses* ni eneo ambalo watu wanepewa lenseni ili ku-*monitor*, ku-*facilitate*, utaratibu gani mfanyabiashara atakwenda nao kwenye maisha, kama biashara ya duka. Lakini maduka mengi yaliopo katika Halmashauri zote wananchi wetu ni maskini, wanatozwa sana leseni za kila aina. Ninataka kujua kwa mfano hata Mji Mkongwe duka ambalo linauzwa vinyago, anakatishwa leseni na Kamisheni ya Utalii lakini pia wanalipa leseni kwa Manispaa. Kama hili limeondoka lakini bado kuna utaratibu wa leseni za maduka. Ninataka kujua leseni zote ambazo maduka wanazipata je, zinalingana uhalisia wa biashara zao.

Suala jengine ni kuhusu masoko. Nilimuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo suala la soko akasema kwamba tayari amejipanga na michoro ipo. Na masoko ambayo nilizungumza mimi ilikuwa ni Kaebona Unguja Ukuu, Dunga Mitini pamoja na Kivunge Mahonda. Kwa vile Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo amesema ramani zipo, hivyo ninataka kujua ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kati kuhusiana na soko la Unguja Ukuu Kaebona pamoja na Dunga Mitini, tuweze kupata taarifa zaidi kutoka Wizara yake.

Pia katika eneo la Kaebona, lile ni eneo la jeshi. Mbali ya kutaka kujengwa soko la kawaida. Tunataka tujenge soko kubwa ambalo litakuwa soko la kisasa na litawaunganisha watu wa Kusini yote; Paje, Michamvi, Jambiani, Makunduchi, Unguja Ukuu, Uzi, Unguja Ukuu Kaepwani na maeneo yote yale, iwe ni *centre* ya huduma kwa Mkoa wa Kusini kuweza kupeleka huduma kutoka mjini kuwasogezea wananchi wetu wa Mkoa wa Kusini. (*Makofi*)

Pia kwenye hotuba yake amezungumzia suala la *CCTV*. Kwenye ukurasa wa 12, kwenye bajeti kuu aliposoma Wizara ya Fedha na Mipango ameomba

Waziri bilioni kumi na nane ambazo zilikuwa zimetengwa katika suala zima la *CCTV*. Katika ukurasa wa 12 nimegundua kwamba kuna bilioni kumi ziliidhinishwa hadi mwaka jana mwaka wa fedha wa 2015/2016. Tayari ametiliwa bilioni nne, milioni mia moja na ishirini na nne, laki mbili na elfu tano sawa sawa na asilimia 41. (*Makofi*)

Sasa hivi fedha zilizotoka mwaka jana kwenda mwaka huu na hizi kuna tofauti gani. Mhe. Spika, ninazo taarifa pia kwamba Kampuni ya *ZITE* ilifunga kamera kumi mwaka jana au mwaka juzi. Kuna kamera mia tatu na kumi na tano zilitaka kufungwa maeneo mbali mbali na hizi zilikuwa ni msaada. Sasa je, kama hizi taarifa ni sahihi baina ya kamera hizi na hizi alizoomba mwaka jana maeneo tofauti, kuna tofauti gani.

Pia nilitaka kujua suala moja muhimu kwani mimi nakwenda kusimamia katika suala la haki. Kwa bahati nzuri au mbaya katika Wizara yake pia anasimamia suala zima la usajili na masuala ya vitambulisho. Kwa kweli hii ni taasisi muhimu sana. Katika mwaka wa fedha wa 2015/2016 bajeti aliyotiliwa ni *almost forty three percent*. Hii hatari kwa sababu Ofisi hii ni muhimu. Wananchi wote hawawezi kupata maisha yao yote bila ya kuwa na vitambulisho vya Mzanzibari. Wanahitaji kwenda benki kufungua akaunti, wakitaka kununua ardhi wanahitaji kadi. Yaani kama huna kadi hii ni balaa.

Kwa hivyo, lazima Ofisi hii na taasisi nzima ya Usajili tuwe makini sana. Kwa hivyo ninaamini hizi fedha zilizoidhinishwa hazitatosha. Sasa nilikuwa ninataka kujua hapa pana mpango gani maalum wa kuweza kuwasaidia hawa wawe wanakwenda vizuri. Mwenzangu amegusia suala zima la Meya. Meya kila kukicha hadhi yake inashuka. Ninataka kujua Meya wetu huyu amejenga mahusiano na nchi ngapi katika miaka iliyopita na Meya ameweza kutembelea nchi ngapi. (*Makofi*)

Ninakumbuka baba yangu mimi alikuwa Mkurugenzi wa Manispaa na tulijenga mahusiano na Serikali ya Ujerumani. Sasa kama ni Meya; huyu leo hadhi yake inashuka na hizi nchi zilizokuwa na miji ambayo amejenga mahusiano nayo kwa pamoja. Je, haya mahusiano bado yapo. Na Meya kama alivyosema Mhe. Mwakilishi hapo alipochangia, ninakumbuka alipokuwa Marehemu Mtoro Reheni, enzi za Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, alikuwa huyu mtu ni muhimu sana. Na leo hadhi yake Meya inazidi kushuka. Ni kitu gani kinachopelekea kushuka huku. (*Makofi*)

Pia ninataka kuzungumzia suala la *public toilets*. Watu, wanajisaidia kila eneo, hasa wanaume. Ni hatua gani za kisheria zitachukuliwa na kwa nini serikali

mpaka leo haina mpango wa kujenga *public toilets* hasa mijini. Na katika mpango huo mzima naomba kuelewa katika Mikoa ambayo sasa hivi tayari wageni wanakwenda wengi ya *spice tours*, maeneo ya Kusini wanapopita. Ni maeneo gani ndani ya Halmashauri umeweza kujenga *public toilets* kwa sabbu *public toilets* ni ajira. Unamuweka mtu anasimamia vyoo, anasafisha mchana na jioni. Ninaamini hapa tunapoteza mapato makubwa sana.

Pia nilitaka kuzungumzia suala la Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kati. Mhe. Spika, Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kati ni katika Halmashauri moja muhimu sana kama Halmashauri zote. Hii Mhe. Spika, kwa sababu tayari Mhe. Rais alipokuja amezungumza katika mji mpya unaokuja kwenye Mji wa Tunguu. Ninataka kujua Halmashauri yake inajipanga vipi katika mpango mzima huko mbele tunakoelekea.

Mhe. Spika, ninataka kuzungumzia sasa suala la taka. Kwa kweli mengi nimeshataja na ninatumai Mhe.Waziri ameandika, sasa kidogo ninarudi nyuma. Sasa sijasema suala la taka ninataka masuala ya fedha. Kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuna Halmashauri zake ambazo zimetajwa hazijapata ile *certificate* ya namba moja kwamba kuna kasoro.

Mimi ninakubaliana hapa pana changamoto nyingi na ninamuonea huruma sana Mhe. Lakini ninataka Mhe. Waziri akazane sana mapato mengi sana katika Wizara yake. Atafute mfumo ambao utaweza kumsaidia, ambao katika miaka ya mbele fedha hizi, nina dakika ngapi Mhe. Spika...

Mhe. Spika: Una dakika mbili.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana. Katika mfumo mzima lazima awe na mpango maalum. Kwa mfano Baraza la Mji lazima wawe *innovative*, waje na mawazo ya kisasa, mawazo ya kimjini. Baraza la Manispaa linafanya kazi kwenye Mji Mkongwe wenye urithi lakini pia ni mji ambao umechanganyika damu, madhehebu, kabila na fikra tofauti. Kwa hivyo tunataka kujua miaka ya mbele Baraza la Mji atalifanyaje liwe Baraza la Mji, kama ilivyo Manispaa yetu katika Afrika Mashariki na Kati. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja asilimia 98. Nitamuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja masuala yangu yote anijibu ili tusije tukabanana katika vifungu, tukatesana kama jana tukakaa masaa marefu.

Ahsante sana Mhe. Spika, ninakushukuru, naunga mkono hoja asilimia tisini na nane, mbili kidogo nitazizuia mpaka nitakapopata maelezo kwenye masuala yangu.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said. Sasa naomba nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame atafutiwa na Mhe. Ali Salum Haji na Mhe. Nassor Salum Ali ajiandae.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara ya Maalum za SMZ.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuweza kufika hapa na leo tukiwa katika hali ya uzima na afya. Pia naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa uwezo wa kuweza kulifikisha hili na kuweza kulifanyia kazi katika siku hii ya leo. Lakini pia nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii nzuri ambayo inatosha kama itafanyiwa kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, nikija kwenye mada. Nianze kwenye Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM). Mhe. Spika, kwenye hotuba yake hii kaeleza kwamba Kikosi hiki ch KMKM kina majukumu ya kulinda usalama wa bahari na kuzuia njia zote zinazoingiza magendo. Lakini hapa hapa ningependa kumuuliza Mhe. Waziri. Je, kikosi hichi kina kazi ya kuzuia tu haya magendo kuingia, na sio kutoka? Mhe. Spika, ningeomba kwa nafasi ya upendeleo ungeiona Nungwi zaidi kwenye kazi hii ya kuingiza magendo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Nungwi tuna bahari kubwa na inafahamika Zanzibar nzima hii. Lakini Nungwi hatuna bandari ambayo inafahamika Zanzibar hii. Nungwi tuna soko ambalo linafahamika Zanzibar nzima hii. Lakini soko lile la Nungwi ndilo linalotumika kama ni bandari. Bandari hiyo ndiyo ambayo kunafanyika vitu ambavyo vipo kinyume na sheria zetu ambazo tumezitunga.

Mhe. Spika, kwenye Kijiji cha Nungwi, ongezeko kubwa sana la uingizaji wa magendo asilimia hamsini na tano mpaka sabini ninaweza kusema linafanyika katika Kijiji cha Nungwi. Mhe. Spika, Nungwi ipo karibu sana na Tanga na Nungwi ipo karibu sana na Pemba. Lakini maingiliano haya yanafanyika hasa zaidi kwa kutoka Tanga kuja Nungwi. Kwa sababu mtu anaweza akatoka labda sehemu nje ya mji wetu au nje ya Zanzibar akapitia Tanga, akaingia Nungwi

yeye kama ni Mtanga. Na akaingiza vitu, ana uhakika kwamba pale hakuna mtu wa kumzuia wala hakuna mtu wa kumuuliza. (*Makofi*)

Nungwi tuna Kikosi cha KMKM pale Mnarani ambacho kinafanya kazi vizuri na tunakishukuru kwa kazi hizo ambazo inazifanya.

Kama utaamini Mhe. Spika, Kikosi cha KMKM kipo Mnarani, kinaweza kikazunguka kikafika mpaka sokoni, lakini ufukwe wa Nungwi ni mkubwa na ni mpana na tunajua kwamba umezunguka Nungwi nzima. Nikisema Nungwi nzima ninamaanisha Jimbo zima la Nungwi. (*Makofi*)

Tukiangalia kwamba watu hawa wa Kikosi hichi cha KMKM hawawezi kumuona mtu aliyeingia Nungwi kupitia njia sokoni, upande mwengine wa Nungwi lakini yupo katika Nungwi ile ile. Sasa tunajiunga. Je, hichi kikosi kipo kwa ajili ya kutusaidia au kipo kwa ajili ya kutubomoa. Kama kipo kwa ajili ya kutusaidia basi tunaomba wananchi wa Nungwi tusaidiwe, tena tusaidiwe sana kwa hili la uingizaji wa magendo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nikija katika suala jengine kuhusu hichi hichi Kikosi cha KMKM. Mhe. Spika, katika miaka mitatu au minne iliyopita kulitokea ajali kubwa sana, kama tunaikumbuka ya *MV. Spice Islander*, ilizama katika bahari ya Nungwi.

Mhe. Spika, wana kijiji wa Nungwi ndio waliofanyakazi ya uokozi naweza nikasema hivyo, kabla ya mtu yeyote. Kama kungekuwa na kile chuo pale cha mafunzo ya uzamiaji na uokozi kilichokaribu na Nungwi basi tungeweza kufanikiwa katika suala hili mapema zaidi kuliko mtu aliye mjini au aliye Kusini Unguja. Kwa sababu kama taarifa tulizipata mapema, kwani mawasiliano yalikuwepo na watu tangu wako katika bahari ya Tumbatu wameanza kufanya mawasiliano na watu walioko Nungwi. Kwa hivyo, watu wakawa wanajua chochote kinachoendelea kule baharini mpaka meli ile inazama watu taarifa zote mitaani wanazo, lakini kilichoshindikana kwamba pale Nungwi hivi vitu havipo. Hakuna vitendea kazi vya aina yoyote kiufupi.

Mhe. Spika, hakuna boti pale, hakuna wafanyakazi ambao wanahusika na hilo suala na kama zingekuwepo hizi mapema basi tuna uhakika kwamba tungeweza kuokoa, japokuwa tumeweza na tumefanikiwa vizuri tunashukuru kwa hilo. Kwa sababu mpaka leo kwa kila aliyekuja aliona jitihada iliyofanyika kwa wana kijiji wa Nungwi. Tunaomba Mhe. Waziri katika bajeti yako hii ulitaja hapa idadi ya pesa ambazo zitatumika kwenye mikoa. Nakuomba Mhe. Waziri kwamba jengo hili la mafunzo ya vikosi hivi vya uzamiaji na uokozi katika Wilaya yetu ya Kaskazini A, basi lije lisimame Nungwi, kwa sababu

sisemi Mkoa naweza kusema Wilaya na liwepo jengo hili. Kwa sababu tunajua kwamba Nungwi ndio kwenye bahari kubwa.

Mhe. Spika, nikiangalia kwenye suala jengine, nakuja kwenye suala la vitambulisho. Mhe. Spika, katika suala hili tunaona mlolongo na msongamano na mazonge yaliyokuwepo kwenye wilaya na mikoa kuhusu vitambulisho. Mhe. Waziri ningekuomba suala hili. Tunajua kwamba mtu ili apate kile kitambulisho cha Uzanzibari atimie umri uliopangwa. Hata kama mtu kapitiliza au hajafikia kwa muda wa siku moja tu au mwezi mmoja tu basi hawezi kupata hiki kipande, lakini ungekuwepo utaratibu kwa hawa watumishi ambao wanashughulikia hili suala, kwamba kila utakapofika mwaka wanajua kwamba lazima kuna vijana ambao tayari watakuwa wanatimiza ule umri.

Kwa hivyo, wafanye kupita kule kwenye zile sehemu, tusiseme kama kwenye Shehia, tuseme pale pale wilayani tu. Wangetenga siku ambayo wangefanya ile kazi kwa upana zaidi ili waweze kuwasaidia wale vijana, kwa sababu utamkuta kijana labda tayari kakaribia kwenye mitihani yake anataka kile kipande tayari awe nacho, lakini usumbufu ambao unapatikana ni mkubwa na huchukua muda kupata kile kipande. Kwa hivyo, tungeomba Mhe. Waziri na hili ulione tena kwa mara nyengine zaidi ili vijana wetu waweze kupata wepesi wa kupata hivi vitambulisho.

Mhe. Spika, nikimalizia mchango wangu nije kwenye suala la Halmashauri. Suala hili Mhe. Waziri kwenye Wilaya yetu ya Kaskazini A naweza kusema, hasa kwenye Jimbo langu la Nungwi, kwa sababu ndiko kwenye majivuno na majidai ya kila kitu. Katika Wilaya nzima Jimbo la Nungwi ndio kila kitu, na Wenyeviti wa Halmashauri ndiko wanakojivunia, lakini tunafanyiwa mambo ambayo hayaingii akilini. Tunafanyiwa visa ambavyo hata aliyekuwa binaadamu hasa wa kweli na Muislamu hawezi kuvifanya.

Wakuu wa Halmashauri Mhe. Spika, tungekuomba Mhe. Waangaliwe na wawe na usimamizi mkubwa, kwa sababu tukiangalia Nungwi ndio sehemu ambayo inaipa pato kubwa sana nchi yetu hii ya Zanzibar katika masuala ya utalii. Lakini Mhe. Waziri kama utawauliza hao wahusika wa hayo mahoteli na kila kitu kule Nungwi hivyo visa wanavyovipata kwa kupitia Halmashauri naweza kusema vya mjusi kafiri labda. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri Halmashauri mpya ambazo zitapatikana hivi karibuni, hawa wenyeviti wawekewe mkakati mkubwa sana juu ya suala la kula rushwa na kula mali za umma pasipo na sheria na bila ya kujijua wao ni nani. Kwa sababu inavyoonesha kama wakishapewa hivi vyeo hawajui vyeo vyao ni nini na vipi

wavitumie. Kwa hivyo wao wanaingia pale kwa maslahi yao na sio kwa maslahi ya wananchi.

Mhe. Waziri nakuomba uliangalie hili na uwaangalie watu wenyewe, kwa sababu ukimuangalia mtu usoni huwezi ukamjua visa vyake na vitendo vyake. Lakini anapokaa siku mbili tu kwenye uongozi utamjua huyu yukoje na anafanya nini. Usimuonee mtu haya wala usimuone mtu kama huyu labda ni ndugu yangu, udugu usiuangalie, uangalie kazi, wanafanya sivyo halafu lawama zinakuja kwa serikali na serikali ambayo haihusiki wala haina habari.

Mhe. Spika, inafika hatua Mhe. Rais ambaye hana kosa wala hajui kitu kinachoendelea yeye ndiye anaingia kwenye majukumu ya mtu ambaye hata hajui kazi yake ni ipi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningekuomba suala hili uliangalie kwa njia zote na ulifanyie kazi vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa ukamilifu na kwa kupitia wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja hususan vijana. Tuna hakika kwamba tutapewa kipaumbele katika hotuba hii sisi wananchi vijana, asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana kwa mchango wako Mhe. Hidaya Ali Makame. Sasa naomba nimwite Mhe. Ali Salum Haji Kirova, akifuatiwa na Nassor Salim Ali na Mhe. Suleiman Saharani Said ajiandae.

Mhe. Ali Salum Haji (Kirova): Nakushukuru Mhe. Spika, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Lakini kabla sijaanza lolote nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Azza Wajalla, kwa kuweza kunijaalia afya njema na uhai na kuweza kusimama katika hadhara hii ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, mimi sina michango mingi sana natarajia kwamba dakika zako 15 nitajitahidi kwenda nazo sambamba na ikiwezekana nisizimalize. Lakini kabla ya kutoa mchango wangu wa aina yoyote katika wizara hii ya Idara Maalum na Vikosi vya SMZ, ningependa nitowe mkono wa pole kwa familia ya ndugu yetu Ahmed Rashid Ahmed maarufu wanamwita 'Joe'. Huyu ni mgombea wa muda mrefu alikuwa mgombea makini katika uhai wake na alikuwa mwana harakati mzuri sana, amefariki leo asubuhi na majira haya ya Alaasiri umekwenda kulazwa mwili wake pale maeneo ya Kiembesamaki. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, amsamehe makosa yake na awape matumaini familia yake.

La pili, ambalo nataka nimalizie katika salamu zangu na nakuomba uniridhie sana, nataka kuwapa salamu wana CCM wa Zanzibar Unguja na Pemba, kama tunavyofahamu kwamba kwa bahati nzuri Wawakilishi wa CCM walioweza kunipa ridhaa ya kuwa kiongozi wao katika shughuli hizi za Baraza. Mhe. Spika, salamu zangu kwa wana CCM ni kuwaomba watulie na propaganda zinazoelezwa katika nchi yetu, ambazo aliyekuwa mgombea Urais Seif Sharif Hamad kupita maeneo mbali mbali na kujitangazia kuwa yeye ni Rais.

Mhe. Spika, nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa katiba na ndio maana nikawaambia watulie. Kwa nini nikawaambia wananchi watulie, kwa sababu ukifungua cha katiba ya Zanzibar ya 1984, ukurasa wa 16 ibara ya 26(1), inasema;

"Kutakuwa na Rais wa Zanzibar ambaye atakuwa Mkuu wa nchi ya Zanzibar, Kiongozi Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi"

Lakini katika ukurasa wa 23 Mhe. Spika, inasema;

"Iwapo mgombea ametangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwamba amechaguliwa kuwa Rais kwa mujibu wa kifungu hiki, basi hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kumchunguza kuchaguliwa kwake" *(Makofi)*

Katiba ndio muongozo. Kwa hivyo, haya maneno maneno ambayo wamekuwa watu wakiyasema, naomba wayachukulie mithili ya mgonjwa wa akili ambaye nilikutananaye *mental*. Mhe. Spika, jimbo langu na *mental* ni mpaka tu bainaya Jang'ombe na Kwahani zamani, sasa mule ndani tumechimba kisima. Kuna siku wakati tumo kwenye harakati za kutengeneza kisima kile, alisimama mwendawazimu akawa anagombana na wenzake huko pembeni, akawa anawaambia leo sikubali jengo langu hili mpaka niliuze. Sasa watu wakashangaa, yule mgonjwa kapelekwa *mental* kwa sababu ya kutibiwa kwa akili zake pungufu, lakini anapiga kelele kwamba lile ni jengo lake na anataka aliuze. Sasa wale wagonjwa wenzake wakawa wanaulizana, vipi huyu. Kuna mmoja akamzungushia mkono sikioni kwamba hamna, lakini kumbe na yeye mwenyewe ni mgonjwa. Sasa imekuwa CUF, Seif mgonjwa na wafuasi wake wote wagonjwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi namwambia, kama kweli mwanamme na anathubutu kwamba kweli anachokitangaza ndicho kilicho. Hebu siku moja ile gari yake aondoshe ile SMZ, halafu abandike hiyo Adamu na Hawa kama atafika angalau

maili moja, watu hawajamfanyia kazi. Mhe. Spika, tuwachane na propaganda zao, tuendelee kuijenga nchi yetu na tuendelee kufanya maendeleo ya nchi yetu. Naamini kwamba vyombo vinavyohusika vitafanyakazi yake pale ambapo mtu yeyote atakwenda kinyume na katiba ya nchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa nataka nije katika michango yangu, wenzangu wamezungumza, lakini na mimi najaribu kukazia tu katika suala zima la Waheshimiwa Madiwani na nimuombe sana Mhe. Waziri. Tunajua kuna *misunderstanding* ya sheria kitu ambacho kinampa mikwamo, lakini ajitahidi kadiri ya uwezo wake hili suala kuweza kulifanyia kazi ili Waheshimiwa Madiwani waweze kuapa kwa haraka.

Kwa sababu tatizo la Waheshimiwa Madiwani kutokuapa linatugharimu sisi wawakilishi, maana yake inabidi tufanye kazi mbili. Tufanyekazi za Serikali Kuu, lakini pia inabidi tufanyekazi zao za Serikali za Mitaa, kwa sababu madiwani hawako madarakani. Pia tunafika pahala kuwazoofisha. Mwanadamu yeyote anapofanya jambo lolote, basi hufanya jambo kwa matumaini.

Mhe. Spika, wenzetu hawa waligombea kwa matumaini kuwa viongozi ili baadae wafanyekazi za maendeleo, lakini pia wapate riziki za kuendeshea maisha yao. Madiwani wetu wamekuwa wakiteseka na kudhalilika, jambo ambalo kweli ukiliangalia hatufikii pahala na halileti mantiki nzuri.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri afanye jitihada ili hili suala *In sha Allah Biidhinillah Taallah* aweze kulimaliza kwa haraka, ili wenzetu hawa waweze kufanyakazi na tuweze kushirikiana nao kwa pamoja. Kwa sababu hizi ni taasisi mbali mbali zimegawanywa ili kuweza kujenga nguvu ya pamoja baina ya wawakilishi, wabunge na madiwani. Sasa ikiwa eneo moja tayari linafanyakazi na eneo moja halifanyikazi na hawajijui watafanyakazi lini, inakuwa ni hatari na zaidi ni kwamba tunasikia kwamba walikwisha kuapa lakini viapo vyenyewe wakaambiwa batili. Sasa imekuwa kama watoto yatima ambao hawajijui wako wapi.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nataka kulizungumzia ni suala la *parking* katika mandhari yetu ya Zanzibar. Mimi nitazungumzia tofauti zaidi na wenzangu. Wajumbe wenzangu walizungumzia maegesho mbali mbali. Lakini nataka niseme kwamba Manispaa ilianzisha utamaduni mzuri wa kuongeza vyanzo vya mapato kwa kuweka *parking* katika maeneo mbali mbali. Lakini lazima tukiri pamoja na jitihada zao za kuweka *parking* katika mji wetu bado hazijatosheleza.

Mhe. Spika, mimi nataka nitowe mfano wa maeneo ya Malindi Bandarini. Mhe. Spika, inawezekana tukafanya jambo zuri, lakini ikaleta chuki baina ya taasisi na madereva. Eneo la Malindi Mhe. Spika, sasa hivi tunatumia *one way*, hii njia ya kuingia *round about* Malindi kwenda bandarini imefungwa. Sasa magari yanayokwenda kupokea wageni bandarini ndani hayaruhusiwi kuingia, na lile eneo lote wanakuwa wanatumia eneo la pembezoni kuweka magari ili kusubiri watu wao watoke bandarini.

Mhe. Spika, nadiriki kusema kwamba watu wanateswa sana na kile kitengo chetu cha ulinzi shirikishi cha Malindi, maana yake huchukui hata dakika moja. Ukisema unataka kumtizama mgeni wako tu kama ametoka ama hajatoka basi gari imepigwa mnyororo. Sasa tunauliza, sisi hatukatai kulipa kodi, lakini tuoneshwe ni maeneo gani ya kutoka bandarini unaweza kuweka gari yako ikaweza kulipiwa kodi.

Mhe. Spika, lazima tujifunze kwa wenzetu wa Tanzania Bara. Kuna maeneo ya njia kubwa ni kweli huwezi kuegesha gari pembezoni, lakini kwa maeneo ya njia ndogo ndogo za ndani kama bandarini na maeneo mengine, basi magari yanaweza kuwekwa pembeni, kunakuwa na watu ambao wanaongoza namna ya kuegesha magari kwa sababu wanajua magari yale hayachukui muda, ni kiasi cha abiria kushuka na kuondoka. Wangekuwa wanatumia utaratibu huo basi hata hizo Manispaa zingeweza kuongeza kodi. Lakini imekua sasa hivi hawa walinzi shirikishi wamegeuka kama *Askari Traffic*, wanabaki sehemu wanasubiri ufanye kosa ndipo wahukumu, hawakai kumsaidia mtu kumuongoza wapi uegeshe gari yako.

Kwa hivyo, hili limekuwa ni tatizo, maana yake ingekuwa tunaoneshwa usiweke gari hapa, lakini kibao kimekuelekeza weka pahala fulani, lakini pahala pa kuweka hapana, ukisimama imekuwa maudhi.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri, tunataka kuongeza kodi, basi tuweke utaratibu mzuri wa kuegesha magari yetu katika eneo lile. Eneo wanalotumia watu wengi sana bandarini ni eneo la hoteli ambalo liko nyuma ya bandari upande ilipokuwepo ofisi ya zamani ya Mkuu wa Wilaya. Lile eneo dogo, magari yanajaa mengi inakua tabu sana.

Mhe. Spika, jengina ambalo nataka kulizungumzia ni suala la Chuo cha Mafunzo kwa ndugu zetu ambao wanahukumiwa katika Chuo chetu cha Mafunzo kwenye maeneo mbali mbali. Mhe. Spika, vyuo hivi au kwa jina jengine watu wanaita Magereza, kwa muda mrefu yalikua makazi yake sio mazuri katika sehemu ya kulalia. Lakini naishukuru serikali kwamba waliamua

kutumia jitihada ya kupeleka masponji ya badala ya kulala kwenye vile vigodoro au vishuka shuka. Watu wale wanaohukumiwa sasa hivi wanalala kwenye magodoro.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atafute namna mbadala kwa sababu godoro ambalo linawekwa chini, kwa sababu hakuna vitanda linakua linachukua muda mfupi kuweza kuharibika, na matokeo yake wanaigharimu serikali kila baada ya muda mfupi kununua magodoro mengine.

Sasa mimi nahisi tungetumia njia ya busara, kwamba sasa hivi tuondokane katika masuala ya kuweka magodoro chini, ili kujitia hasara za mara kwa mara na tuweze kuwatengenezea wenzetu vitanda ili magodoro yale yawekwe kwenye vitanda badala ya kuwekwa sakafuni.

Mhe. Spika, sio kwamba nalisema hili nawapenda sana wahalifu. Lile gereza halina mtu, Mwenyezi Mungu atunusuru, anaweza akaingia mtu yeyote na mazingira anahitaji yawe mazuri. Cha msingi na ndio maana serikali yetu ikaamua kuita Chuo cha Mafunzo. Tunawapeleka watu kule baada ya kutenda makosa wakajifunze na wajirekebishe ili wakitoka basi wawe watu ambao wameelimika na yale mambo ambayo wameyafanya.

Katika eneo hilo hilo la Chuo cha Mafunzo Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri anisaidie, kwa bahati nilikua Mjumbe wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Baraza lililopita. Mwenyekiti wangu alikuwa Mwenyekiti wa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu Mhe. Hamza Hassan Juma, tulitembelea maeneo mengi sana. Kwa kweli katika maeneo ambayo mimi nataka niyapongeze sana ni eneo la Chuo cha Mafunzo, kwa namna wanavyojitahidi kuzalisha chakula wenyewe na vyengine wakaweza kuuza. Kwa kweli jitihada zao ni kubwa sana, ni lazima nimpongeze Kamishna kwa jitihada ambazo wanatumia.

Kwa bahati tulifanya ubunifu mkubwa sana katika Chuo cha Mafunzo, kuweza kujenga gereza au chuo cha kisasa ambacho kitakwenda na wakati tuliokuanao. Kuweza kuweka viwanda ili wanafunzi watakapokua katika gereza basi wawe na maeneo mbali mbali ya kujifunza na kujitosheleza kabisa.

Pia Mhe. Spika, kuwawekea uwanja wa mpira, wale ni binadamu wanapokua ndani basi angalau waweze kufanya mazowezi mbali mbali. Nataka kujua kwa sababu chuo kile kilileta mjadala mkubwa sana katika vikao vilivyopita. Mjadala wake ulikuwa inaonekana kwamba Chuo cha Mafunzo bajeti yao haitoshelezi kuweza kujenga lile gereza. Serikali ikaji-*commit* kujenga lile

gereza, lakini kukawa kuna *partition* mbili. *Partition* moja serikali iliji- *commit* kulitengeneza, lakini *partition* ya pili tuliwaachilia wenyewe watu wa Chuo cha Mafunzo kujenga eneo la watoto. Kwa sababu inaonekana bado tuna matatizo ya vyuo vyetu vimechanganyishwa baina ya watoto na watu wazima, baada ya wanafunzo watoto kuwaelimisha, imeonekana walikuwa wanaharibika kwa sababu wanakaa na watu sugu. Nataka kujua gereza lile limefikia wapi kwa upande wa lile kubwa la Serikali lakini na lile dogo ambalo tulitegemea la kukaa watoto wadogo ambao hawajatimiza umri wa miaka 18, nalo limefikia wapi.

Mhe. Spika, maeneo mengine ambayo nataka kujaribu kuyaelezea na kupata ufafanuzi, hili nataka nimuombe Mhe. Waziri na kupitia Manispaa, kwa bahati karibuni nchi yetu ilipata mafuriko ya mvua, tunasema tu mvua kubwa maji mengi, lakini nataka nimwambie kwamba baadhi ya maeneo sisi wenyewe tumechangia. Kwa sababu serikali inatumia nguvu za kujenga mitaro, sasa hivi kuna mtaro wa ZUSP lakini huko nyuma jimbo langu lilibahatika kupata mtaro kupitia Benki ya Ujerumani, mtaro ule ni mkubwa umetoka Kwahani umepita Kariakoo, umepita Miembeni, umeelekea baharini. Lakini cha kusikitisha Mhe. Spika…..

Mhe. Spika: Dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Nakushukuru Mhe. Spika, la kusikitisha mtaro ule tangu unatengenezwa huwa haujasafishwa na unachukua mchanga mwingi, sasa ile *level* iliyokuweko mwanzo kama kulikuwa kuna kima zaidi ya futi tatu ule mtaro wenyewe sasa hivi una kina labda cha futi moja na nusu. mchanga ni mwingi. Hatuoni jitihada za Manispaa kuusafisha hatma yake mvua zinaponyesha maji yanakuwa yanapita kwa *speed* ndogo.

Mhe. Spika, jengine nitazungumza kwa haraka haraka anielezwe Serikali itafanya jitihada gani kuondosha bughudha za wafanya biashara katika barabara. Nimejaribu kuziainisha barabara ya Muzamili kwenye jumba la Treni kuelekea sokoni, barabara ya Vikokotoni Skuli kuelekea Afisi kuu na barabara ya Suma kuelekea Mlandege; watu hawana raha ya kutumia njia hizi bughudha imekuwa kubwa. Serikali inatumia gharama kubwa kujenga barabara, inasikitisha zaidi barabara hii ya Afisi Kuu imejengwa karibuni kwa gharama nyingi lakini baada ya kutumia watu wenye huduma za magari, imekuwa wanafanyabiashara ukikanyaga mzigo wa watu wanakuwa wakali wao kutaka kumpiga dereva, wakati dereva ndio mwenye haki ya kutumia ile barabara.

Mhe. Waziri, jitahidi nataka unipe maelezo ya lini tatizo lile litaweza kuondoka ili wenye haki ya kutumia barabara wakatumia barabara yao.

Jengine Mhe. Spika, nataka la kumalizia la mwisho kama nilivyokuahidi kwamba nitakwenda juu ya dakika zangu kumi na tano, naomba Mhe. Waziri anisaidie kunieleza katika mambo ambayo nilijifunza katika hatua nilizopita, tulipata kutembelea mradi wa Misri na JKU Bambi, mradi ule ulileta mjadala tukafika pahala tukazuia fungu na ilikuwa Serikali ikitoa kama sikosei milioni 40. Nilitaka kujua tu ule mradi umefikia hatua gani upo au umeondoka, na kama haupo basi nini tufanye. Lakini kama unaendelea Serikali kupitia JKU imefaidika nini na mradi ule.

Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa dhati kabisa na sina tatizo na Wizara sio hii tu lakini Wizara zote. Lengo letu ni kujenga na kukosoa na kupata maelezo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani nakushukuru sana. (Makofi)

Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira): Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, na mimi kwanza nimpongeze mnadhimu wangu wa Chama cha Mapinduzi Mhe. Ali Salum kwa mchango wake mzuri na umetupa dira zaidi ya muongozo katika michango yetu.

Mhe. Spika, aidha nimpongeze sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi wake wa Wakuu wa Mikoa wapya, wakuu wa Wilaya, vile vile niwapongeze Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wa kisiwa cha Pemba kwa kazi nzuri wanayoifanya mbali na changamoto za kisiasa wanazozipata na kuleta maendeleo katika nchi yetu kwa Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo pia nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye malengo mazuri, yenye mipango mizuri ya kujenga na kuleta maendeleo kwa nchi yetu. Mhe. Spika, nije kwenye Idara maalum, vikosi vyetu vya SMZ nichukue fursa hii pia kuwapongeza sana Makamanda wetu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kulinda na kuleta amani katika nchi yetu, wanafanyakazi nzuri. Hawa ni wajibu wetu kuwapongeza kwa kudumisha amani na kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vile vile Mheshimiwa katika kitabu hiki katika malengo makuu katika kuimarisha uwezo na kuutendea kiutendaji Idara maalum ya kuimarisha mfumo

wa uwezo wa upatikanaji wa huduma imeelezwa katika kitabu chake hiki. Aidha kukuza ushirikiano na vyombo vya ulinzi na usalama vya nje na ndani ya nchi. Vikosi vyetu hivi alikuja akazungumza Mhe. Shamsi hapa kuhusiana na hali halisi ya vikosi vyetu hususan kikosi cha Mafunzo, hali halisi ambayo ipo katika maeneo yale ya makaazi yao, bahati nzuri Chuo cha Mafunzo kiko katika jimbo langu la Kikwajuni nakijua vizuri naielewa vizuri na hali halisi naifahamu.

Kweli haiko katika hali nzuri mimi nimuunge mkono Mhe. Shamsi katika maelezo yake na nimuombe Mhe. Waziri tuwaangalie kwa jicho la huruma, vikosi vyetu hivi hususan kikosi cha Mafunzo. Kutokana na hali halisi ilivyo sio hapa tu Makao Makuu, lakini hasa katika maeneo mengine mbali mbali ambayo wanaishi askari wetu.

Vile vile katika vikosi vyengine vya KMKM, JKU Mhe. Waziri nimuombe sana na Serikali yangu au Serikali yetu chini ya jemedari Dkt. Ali Mohammed Shein kuviangalia na nimpongeze Mhe. Rais kwa kuweza kuangalia kuwapandisha mishahara na kuwa na malengo ya kuweka mishahara sawa sawa na vikosi vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haya ni mapenzi makubwa kwa Rais wetu na Serikali yetu. Lakini huduma hizi lazima ziangaliwe, ili kuangalia maslahi na majengo ambayo vinakaa vikosi vyetu.

Mhe. Spika, nije Baraza la Manispaa waswahili wanasema mwenye haki mpeni Mhe. Mkurugenzi wa Manispaa mpya ambaye Mhe. Rais amemteua miezi michache iliyopita, amelifanya Baraza la Manispaa kuwa linang'ara anafanya kazi nzuri haki yake tumpe. Mimi nina imani kwamba Mhe. Meya amefarijika sana kupata Mkurugenzi huyu. Mimi ni shuhuda hata nikimpigia simu saa 12 za asubuhi, kuna tatizo hasa katika kipindi kile cha janga na mripuko au wakati ule wa mvua yalipotokea matatizo ya mvua na mripuko ule wa maradhi ya kipindupindu, asubuhi nikimpigia anakuja tunashirikiana pamoja katika kusaidia wananchi kutatua matatizo yao.

Mhe. Spika, Baraza la Manispaa limeanza kufanya kazi nzuri ya kuimarisha hali ya usafi katika mji wetu na kuweza kujenga na kuimarisha bustani, vile vile katika maelezo ambayo yapo katika kitabu cha utekelezaji kimeeleza hapa kuendeleza maeneo ya wazi, bustani pamoja na ukarabati na michirizi. Ujenzi wa njia za waendao kwa miguu ujenzi ule ambao unaendelea katika jumba namba 7, mimi nipongeze sana Baraza la Manispaa kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Niwaombe na nimuombe Mhe. Waziri kwamba kazi ile iwe ni endelevu katika maeneo yote ya mjini hususan katika jumba namba 1, jumba namba 9 jumba namba 3 na maeneo mengine ya mjini, kwa sababu Mheshimiwa wakati tunapofanya kazi zile nzuri wananchi wetu watakuwa wanapita kwa miguu bila ya kupata ajali au bila ya kuwa na matatizo yoyote katika shughuli zao za kimaendeleo. Kwa hivyo niwapongeze na kuwaomba kuendeleza miradi ile ambayo kwa kweli umeleta sura mpya katika mji wetu wa Zanzibar.

Suala hili la bustani sote tunatembea katika miji mbali mbali tunaona miji ya wenzetu hali halisi inapendeza, nimesema hapa kwamba sura imeanza kubadilika, lakini nimuombe Mhe. Waziri kama ambavyo Serikali ina mipango ya kufanyia ukarabati jengo lile la treni pale Darajani ni eneo ambalo linahitajika, pia kufanyiwa kazi kwa haraka na Mhe. Waziri akija atwambie kwamba ule ujenzi unaanza lini na mipango gani itakuwa inaendelea nje ya jumba lile, ili kuweza kujenga bustani nzuri. Angalau wananchi wanapokuja au wageni wanapokuja basi waangalie katika mazingira yaliyo mazuri.

Mhe. Spika, nije katika suala zima la barabara za ndani, niipongeze Wizara husika kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuanza vizuri katika kujenga barabara za ndani, lakini Mhe. Spika, katika Jimbo la Kikwajuni ambalo ni jimbo lenye historia, jimbo ambalo la zamani na mji wa zamani mji ambao unanuka asumini nzuri, bahati nzuri Mhe. Meya analijua vizuri jimbo la Kikwajuni.

Kuna barabara ambayo inatokea jumba namba 10 Kisima Majongoo kuteremka bondeni Msikiti Makuti Mheshimiwa, barabara ile kwa kweli iko katika hali mbaya na barabara ile inatumiwa na wananchi walio wengi. Barabara ile ni muhimu sana kwa wananchi wetu. Mheshimiwa laiti kama utafanya ziara katika barabara ile nadhani utaweza kukatisha safari yako njiani. Barabara imejaa mashimo, barabara haipitiki na barabara ile ni muhimu hasa ukizingatia kwamba Kikwajuni ni mji wa zamani, hata hao watalii wanapokuja lazima wafike Kikwajuni waone asumini za Kikwajuni. Sasa sio vizuri kuoana kwamba Kikwajuni inanukia asumini nzuri, lakini barabara ile ni mbovu ukiunganisha na barabara ya jumba namba 7 nyuma.

Mheshimiwa pale Mkurugenzi anapafahamu vizuri sana tumeshakwenda mimi na yeye kuangalia hali halisi ya maeneo yale hata kama sio katika bajeti hii, lakini bajeti ijayo basi ziingizwe katika kuzifanyia ukarabati barabara zile. Niipongeze Wizara kwa kuweza kujenga barabara ya Msikiti wa Shehe Nassor kuelekea Maisara, lakini vile vile kujengwa kwa haraka.

Mhe. Spika, kuna barabara ambayo inatoka Baraste Kipande kuja kwa Biziredi, barabara ile ni ya zamani na mimi nina imani Mhe. Spika, barabara ile unaijua kutoka Baraste Kipande kuja Biziredi. Ni barabara ambayo huwa inatoa huduma kubwa sana wakati inapotokea matatizo katika barabara nyengine.

Kwa hivyo niombe kwa heshima na taadhima nimuombe Mhe. Waziri kuiingiza katika bajeti ya 2017/2018 ili barabara ile nayo iweze kujengwa. Nilipiga kelele katika kipindi kilichopita wakati niko katika jimbo la Rahaleo kwa barabara ya Mitiulaya, nimshukuru sana na nimpongeze sana Mhe. Waziri na niipongeze sana Serikali kwa ujenzi wa barabara ile na leo wananchi wanafurahia sana matunda ya Serikali yao na haya ndio matunda ambayo wananchi wanayataka.

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya mengi, Zanzibar imebadilika, inang'ara. Jana Mheshimiwa Suleiman Sarhani kazungumzia hapa suala la barabara ya Msingini kwenda Chachani ambayo iko sawa sawa na barabara hii ya Kisimamajongoo kuja Kikwajuni, na mimi nina imani kwa Serikali yetu hii tuliyonayo kwa kasi ambazo imeanza barabara hizi zitajengwa. Zanzibar itang'ara, Kikwajuni itang'ara, Chake Chake itang'ara Fundo itang'ara.

Mhe. Spika, nataka nilizungumze hili halipo katika Wizara hii lakini nataka nizungumze kutokana na maendeleo ambayo yanafanywa na Serikali yetu. Siku moja nilifanya ziara kisiwani Pemba chini ya Mwenyekiti wangu Mhe. Hamza Hassan Juma (kamanda), tukafika pale Konde Mjini, sasa kukawa na mahali pameandikwa *New Singapore* lakini sisi tukapata jibu kutokana na uzuri wa barabara ambayo imejengwa kutoka Konde/Wete.

Kwa hivyo mimi nina imani katika kipindi cha miaka mitano tuliyonayo kutokana na kasi ya Serikali yetu, kutokana na kasi za viongozi wetu, kutokana na kasi ya Waziri wetu huyu, mimi nina imani barabara zote za majimbo yote, barabara za ndani ifikapo 2020 tutakuja kusema Serikali yetu imefanya hili. Na ni vyema Mhe. Waziri basi ukafanya ziara katika majimbo yetu ili tukakuonesha hayo maeneo, ukaja Kikwajuni nikakuonesha. Ukenda Chake Chake Msingini kwa Mhe. Suleimani atakuonesha, ukenda kwa Mhe. Hamza ili tukaona hali halisi ya mahitaji ya wananchi wetu katika barabara hizi za ndani.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakia mbili.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, kwa kumalizia muda wangu mnadhimu wangu kasema na mimi msaidizi wake ni wajibu wangu na mimi kusema

kwamba naunga mkono yale aliyosema; amani na utulivu tulionao ni lazima Serikali yetu iunge mkono na kuunga mkono vikosi vyetu hivi, ili kufanya kazi na kulinda amani yetu.

Tunaelekea katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, mengi yamesemwa, mengi yanafanywa sote ni Wazanzibari, sote ni Watanzania na sote ni ndugu. Nimuombe sana Mhe. Waziri kukaa pamoja na vikosi vyetu kupanga mikakati ya ulinzi na usalama kwa sababu hapa kumejaa Wakuu wa Mikoa ambao ni Wajumbe wa Kamati za Ulinzi na Usalama. Wakuu wa Wilaya, Makamanda kuhakikisha katika kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani hatutaki kusikia choko choko, wananchi waislamu wafunge kwa amani na utulivu. Tudumishe, tuendeleze amani yetu tuliyonayo kwa faida yetu sisi na kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mheshimiwa tusibabaike wala tusihangaike, wala tusishurutishwe na viongozi ambao hawaitakii amani nchi hii. Sote ni Wazanzibari nakusudia kusema sote ni ndugu, Mpemba kamuowa Muunguja, Muunguja kamuoa Mpemba. Sote ni ndugu tudumishe amani yetu tupendane tujenge nchi yetu kwa maslahi yetu sisi.

Baada ya kusema maneno haya naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii adhimu tena ndio pahala pake maana yake mimi ndio mwenye mji wa Chake Chake. Mhe. Spika, mengi yameshasemwa sana kuhusu habari ya barabara ya Msingini kwa hivyo nitalisemea zaidi, lakini awali ya yote na mimi napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, nimshukuru na Mtume wake Muhammad (SAW), nawashukuru na watu wa Jimbo la Chake Chake walionipigia kura na hata wasionipigia kura, tutakwenda pamoja kuendeleza nchi yetu.

Mhe. Spika, pia nikishukuru Chama cha Mapinduzi pamoja na watendaji wake, pia niwashukuru Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, Maafisa Tawala waliokuwa tunakwenda nyumba kwa nyumba kumuombea Dkt. Ali Mohammed Shein na mimi mwenyewe walikuwa wananiombea kura. Lakini Mheshimiwa kabla sijaendelea na yote kwa muongozo wako tu nimemuona Mkuu wa Mkoa wangu ambaye ndio katika jumla walionisaidia basi kwa heshima yako asimame hapo hapo atoe mkono pale juu, kwa sababu nimefurahi

sana. Mheshimiwa naomba umwite mwenyewe Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mhe. Mwanajuma Majid Abdalla. Nakushukuru sana mheshimiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa jengine kabla sijaendelea kuchangia hotuba, mimi nakubaliana na wapenzi wangu wote waliomo kwenye Baraza sijui kwa umahiri wangu au kwa kila kitu huwa wananita majina tofauti tofauti.

Nilikuwa natoa ufafanuzi zaidi Mheshimiwa mimi nalikubali jina ambalo Chake-Chake wananiita jina maarufu ni Sele Manga, hilo nalikubali bado, nalikubali jina jengine wananiita Meya eti kwa kulitetea Jimbo la Chake-Chake sana pia nalikubali sana.

Pia wananiita Naibu Waziri wa Wanawake kwa kuwatetea wanawake nalikubali nitakuwa wa Castico, lakini wengine akina Mhe. Nadir na wengine akina Mhe. Diwani huwa wananiita jembe. Mheshimiwa neno hili silitaki mimi, kwa sababu mimi sitiwi mpini. Jina la jembe mimi silitaki wasiniite, waniite Meya, hili nalitaka nalisema wazi wasinite jembe atakayekubali kuitwa na akubali mwenyewe mimi sitaki kuitwa jembe. Mheshimiwa naendelea.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze vyama vyengine vilivyokuwa vimeshiriki ambapo wenzetu wengine wamo humu. Mimi kila siku nilikuwa nasema kwamba vyama sio vya upinzani, ni vyama vya ushindani na waliomo humu ndani ni waliojiwekea kwamba wao ni vyama vya ushindani si upinzani. Kwa hivyo, mheshimiwa tunakwenda nao vizuri sana.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye hotuba moja kwa moja, kweli mheshimiwa Chake-Chake, ni mji nambari mbili ambao kwa kweli namwambia Mhe. Waziri autizame kwa jicho la kipekee. Mhe. Spika, Mji Mkongwe tayari umeshajengeka, umeshapata heshima kubwa, lakini Mji wa Chake-Chake namthibitishia na kumwambia katika Pemba nzima ndio mji unaoweza kumpatia mapato na ndio mji wa kistaarabu kuliko miji yote kwa Pemba.

Mhe. Spika, mji huu hapo mwanzo na haiba yake kama unavyoiona kwa sababu tunasema miji ambayo ina majengo makongwe ndio miji ambayo zamani ilikuwa ya kistaarabu zaidi, kwa sababu wenzetu kabila hizi za Kihindi na Kiarabu ndio walivyozivamia kibiashara. Lakini Mheshimiwa mji wa Chake-Chake kwanza uko *centre* pia jinsi ulivyovamiwa katika biashara, namuhakikishia mheshimiwa mapato zaidi atayapata pale.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme leo asubuhi Naibu Waziri wa Miundombinu kidogo alinipunguza kasi katika barabara zangu mbili. Barabara ambayo inatoka katika hospitali ya Chake-Chake kupitia Qatar kuja kuungana na barabara kubwa inayokwenda Tibirinzi, na barabara ya Msingini ambayo mpaka mheshimiwa Mhe. Nassor pia hapa ameitaja. Mheshimiwa amenivunja nguvu kwa sababu ameniahidi na mimi nataka niwahakikishie watu wa Jimbo la Chake-Chake na watu wote wa Zanzibar kwamba haraka iwezekanavyo, hii barabara ya Qatar mpaka mkandarasi tayari ameshapatikana na wakati wowote itaanza. Hilli amenithibitishia huyu bwana lakini na njia ya Msingini ananihakikishia kwamba itajengwa katika viwango vikubwa wakati wowote kuanzia sasa.

Ningeomba tuwe na subra watu wa Chake-Chake kwa maneno niliyopewa sina haja ya kumuwekea waziri vikwazo kwa njia hizi mbili. Isipokuwa tu nitamuomba waziri kwamba najua mimi sio peke yangu katika majimbo kuna wenzangu wengi kwenye hizi. Kuna njia kama tatu au nne ambazo nitazihitajia hata na mimi tuchangiane lakini tuzifanyie ukarabati mdogo, barabara inayotoka Madungu kuelekea Mgogoni, barabara inayotoka Chanjaani kuelekea Mpendae na barabara moja ambayo inatoka Madungu wanaenda Cossovo na barabara moja iko Kiziwani. Hizi barabara tutasaidiana kwa muongozo alionionesha tutazifikisha pahali pazuri angalau zipitike kwa kiwango cha aina yoyote. Hilo mheshimiwa nilikuwa nashukuru sana.

Mhe. Spika, nije katika mambo ya kukuza mji. Chake-Chake haina *stand* ya magari wala haina *stand* ya mabasi na mizigo. Mheshimiwa katika *stand* kubwa ambayo tunaitegemea, hii ishapelekwa karibu tunasema wimbo wa taifa, imeshazungushwa mabati mara tatu, nilisikia itawekwa Tibirizi haikuwa, itawekwa Michakaini haikuwa, sijui sasa iko wapi? Nataka tu utakapokuja hapa unieleze hii *stand* itajengwa wapi na lini? Mheshimiwa mji wa Chake-Chake hauendeki sasa hivi, kwa hilo moja nitaomba na lini itaanza hii *stand*, hilo moja ningeshauri sana Mheshimiwa.

Mhe. Spika, la pili ni kwamba mji wa Chake-Chake haiba yake imekosekana kabisa kwa sababu tumeingia katika mazingira mengine tofauti. Mheshimiwa siwakatai watu wanaoitwa wazungu wanaokuja kufanya tathmini zao hapa, lakini tutizame na mazingira. Kisiwa cha Pemba ni kidogo sana kama tunataka bahari basi twende Vitongoji upande wa Kusini hakuna nchi tena ni bahari tupu. Ukitoka pale wewe mpaka kiama huko hakuna tena kwengine.

Sasa bahari tunayo hapa upande wa Qatar chini kwenye soko kubwa la samaki la zamani kuanzia sasa hivi ofisi ambayo ni ya Makamu wa Pili wa Rais

ambapo palikuwa na gati hapo zamani kuelekea mpaka Ikulu, eneo lile lilikuwa kama ni *beach* ambayo inapendeza. Ilikuwa na maeneo mazuri halafu ilikuwa na usafi wa kuangalia mpaka Kisiwa cha Misali unakiona na ndio haiba hasa iliyofanya mpaka Ikulu kujengwa kule.

Leo mheshimiwa tumeingiwa na sababu za mikoko limeachwa lile eneo wakati ndugu zetu wa magereza walikuwa wakija kulisafisha, kwani kuna mchanga mzuri watoto walikuwa wanajifundisha kuogelea pale. Mambo yalikuwa pale lakini leo mtu akitaka aende Wesha, sijui aende pahali gani mji gani huo utakaofanyika vile. Kwa hivyo, ningeomba sana tufanye utaratibu wa Mji wa Chake-Chake, nakuomba mheshimiwa uje utuangalie kwa kina ule mji unaweza ukawa mji mzuri, tena naweza kusema hata hapo Mji Mkongwe. Lakini lazima uje ufanyiwe utafiti wa kina una uwezo wa kupata mapato mengi sana pale na mji pia ukaondokana na tatizo la *stand* ndogo ndogo kwa wanaofanya biashara. Pale pana eneo kubwa sana tulijaze itakuwa sisi si wa kwanza.

Mhe. Spika, kuna nchi kama Holland wanajaza bahari, Dubai hapo imejazwa bahari hivyo wanapata mapato kwa kupitia maeneo haya nchi hawana tena, lakini leo sisi tunaingiza bahari kusogeza mbele kwa nini na sisi tusijaze na sisi tukaongeza upeo wa mambo hayo. Ningekushauri sana mheshimiwa pamoja na kwamba unaijua Chake-Chake, tuje tufatane mguu kwa mguu nikuoneshe vyakutusaidia.

Mhe. Spika, naendelea kusema kwa sababu muda mdogo lakini nakuomba dakika tano lazima unipe.

Mhe. Spika, pia nataka niseme na *stand* kongwe kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa soko la Chake-Chake la mboga ulivyolifanyia ukarabati, hili lazima nalo nikusifu kwa sababu umelijenga vizuri, la kisasa umetia na ukuta wake, linaendelea na ndani yake kuna *stand* ya asili.

Mhe. Spika, *stand* ile ilikuwa na mipango ya kutobolewa mlango mwengine maana ina mlango mmoja kama chupa, gari zikiingia hazitoki tena, akibana mlango waliomo ndani wote hawatoki. Kuna nyumba tumeziacha mpaka baadhi ya nyumba zimejengwa. Hivyo ningeshauri pia uje ututembelee ikiwezekana kuna nyumba kama moja tuje tufanye mitikasi ya kuiondoa halafu tuweze kupita angalau kuungana na Qatar. Kwa hivyo, gari inaweza ikatokea katika maeneo inayotokea ikashusha pale *stand* ikenda ika-*park* kule Qatar ni mji mzuri utapangika. Ningeshauri mheshimiwa tutakuja kuangalia na tuwapate wataalamu pamoja na mambo hayo.

Kwa hivyo, hayo nilikuwa nataka nikwambie kutokana na mwelekeo mzuri ambao kwa kweli nimeufurahia.

Mhe. Spika, jengine sisi pale Chake-Chake ndio *centre,* ndio pahala wenzetu wakitaka *drip* wanakuja kuchukua wakapeleka mashamba, mambo ya kisiasa haya lakini na vyama vyetu hivi vikitaka mikutano vinafanya Tibirizi, vyengine vinafanya Gombani. Mhe. Spika, mikutano hii ya vyama iondoke pale Tibirizi itafute Pujini, itafute nje ya mji. Mheshimiwa siku ya kufanya mkutano pale mji mzima askari wanapata tabu, matatizo yanajitokeza kwa nini, hapa tumeondoa Malindi tumeweka Kibandamaiti. Sasa tuondoe pale mjini kwani ile ni njia ya Ikulu, Rais yuko kule anashindwa hata kupita pakiwa na mkutano hasa viongozi wakubwa. Hawa viongozi wadogo wadogo hii mitaa mitaa hawa waache kila mmoja atafanya mkutano wake, lakini viongozi wakubwa mjini tuondoe matatizo Mheshimiwa. Hilo mimi nashauri ikiwezekana liwe linazingatiwa.

Mhe. Spika, jengine Chake-Chake maofisi karibu asilimia 80 yako Chake-Chake, mimi nataka nikwambia hata kama sio wizara zako lakini maofisi mengine naweza kusema hata ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya bado hadhi zake hazipo. Hiyo ya Mkuu wa Wilaya nimesikia inatengenezwa lile jengo kongwe la kizamani mpaka leo sijaona mimi umuhimu wake, wala sijaona limetengenezwa vipi.

Bado Mkuu wa Wilaya anakaa kwenye kibanda ukifika uiname ndio upite. Kwa hiyo, hili ningeomba ulichukue kwa kina na Mkuu wa Mkoa bado ingawa ana jengo amejengewa lakini bado hadhi yake hasa kama Mkuu wa Mkoa bado, lakini si haba halipo. Kwa hivyo, hilo ningeshauri pia.

Mhe. Spika, pia niseme watu wa Zimamoto kwa pale Chake-Chake. Watu wa Zimamoto wana eneo Chake-Chake ni kweli bado serikali haijakuwa na uwezo, lakini walikuwa na eneo kubwa sana la kuweza kukaa pale njia ya Pujini. Mheshimiwa wametia uzio kijisehemu magari yao wanaingiza humo siku watakayokuja kuwa na magari, hivi sasa pana vijumba vitatu vinne pale Chanjaani wangefanya utaratibu kabisa wa kulichukua lile eneo ili wakaondoka kabisa na tatizo hilo, nyumba zenyewe bado hazijakuwa na hadhi kubwa ni kulipana ukamwambia ondoka wakapiga uzio kabla mambo hayajawa. Mheshimiwa watakuja kuwa na magari waje waweke chini ya nyumba za watu ije iwe balaa, *fire* ni kitu kikubwa haina gari ndogo hii, magari yake yote ni makubwa na yenye matenki yana yanafasi kubwa ya kuweka pale. Hilo

ningeshauri Mheshimiwa ulifanyie kazi kabla mambo hayajaharibika pale Chanjaani.

Mhe. Spika, pia hapa Qatar watu wamekuja kwenye mambo ya masoko, lakini hili tutalizungumza sana na Mkurugenzi atakayekuwepo pale au Meya baada ya kuingia pale. Mheshimiwa pale watu wanauza samaki chini, wanauza vitu vyengine chini, mvua inanyesha na samaki wako chini, haipendezi.

Kama tunawahitaji wale watu tuwajengee mabao, tuwajengee banda tujue vya kufanya na wako barabarani, tufanye kila jitihada pale pana msingi tu ufukiwe, pasogezwe vizuri, mji wa Chake-Chake ukipangika ni mzuri. Kwa hiyo, hilo nilikuwa nalisemea sana maana yake na nafasi yenyewe mheshimiwa aliyonipa ni ndogo.

Mhe. Spika, jengine nataka niseme kwamba humu nimeangalia angalia nikaja nikaona taarifa moja ambayo hii ni ya utumishi iko katika ukurasa wa 17…

Mhe. Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Haina shida Mheshimiwa.

Mhe. Spika, hawa watumishi ambao kwa kweli nimeona katika malipo yao, hii kamati ya utumishi wa vikosi nimeona baadhi ya vikosi vingi au katika sehemu nyingi tumelipwa asilimia 99 wengine, asilimia 80. Hii kamati pamoja na kusoma nimeona wamefanya vikao karibu vitano, imelipwa asilimia 6 kwa mwaka mzima ambapo mimi naweza kuwasifu watu hawa ni wazalendo sana wanajitahidi lakini tusiwafanye hivyo itakuwa hawawezi kufanya asilimia 6 ni asilimia ndogo mno. Kwa hiyo, ungefanya maarifa zaidi tukaweza kuwafanyia maelekezo.

Mhe. Spika, nizungumze neno la mwisho ili nisichukue nafasi zaidi. Mimi nataka nizungumze na watu wa Magereza hawa wenzetu wa Chuo cha Mafunzo. Mimi nazungumza tena dhana ile ile ya Chuo cha Mafunzo ibakie isiwe Magereza hata kama inajuulikana ndio hilo. Ningeshauri sana tunapiga vita sana ukimwi, tunapiga vita madawa ya kulevya lakini bado nazungumzia suala la baba au mama aliyefungwa. Bado nawaomba watu wa Magereza pamoja na kwamba wao ndio wenye nafasi kubwa wasiwe na vikwazo vikubwa kumkabidhi baba au mama kule gerezani kumpa nafasi akazungumza nae japo kwa ulinzi, lakini wampe nafasi hata kwa mwezi aweze kukaa na mama na watoto kwa sababu mambo ya kule magerezani yanakuwa mashaka.

Mhe. Spika, bado nina mengi lakini sitaki nivunje kanuni, kwa asilimia mia moja naunga mkono hoja. Nashukuru Mheshimiwa.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi ya kuchangia machache kwenye hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.

Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote. Niwapongeze Wakuu wa Mikoa wa Pemba Kaskazini na Kusini Pemba pamoja na Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tawala wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Kusini Pemba.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa ni mdogo sana kwa sababu nimesema nichangie ili niweze kusaidia na niweze kutoa ufafanuzi mdogo.

Mhe. Spika, niende kwenye Wilaya ya Micheweni; Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ni Halmashauri ambayo mwaka 2014/2015 iliongeza mapato mengi, lakini kabla yalipokatwa majimbo kwa kweli mapato yatapungua sana. Mhe. Spika, naiomba wizara kwa kushirikiana na serikali kwa sababu Wilaya ya Micheweni ni Wilaya ambayo ina umasikini mkubwa iweze kutizamwa kwa jicho la huruma kwenye vipaumbele vya serikali.

Mhe. Spika, nikiendelea hapa hapa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni niwapongeze kwa kuweza kushirikiana na wananchi kujenga soko la Micheweni Chamboni na soko la Jimbo la Wingwi na Skuli Simai, pamoja na skuli nyengine ambazo ziko Wilaya ya Micheweni maeneo ya Tumbi.

Mhe. Spika, nikiendelea niende kwenye Kikosi cha KVZ. Mhe. Waziri KVZ Micheweni mwaka 2000 walikuwa wana ofisi yao kwenye jengo la soko ambalo lilijengwa tangu awamu ya Mhe. Rais Amani Abeid Karume. Mhe. Waziri soko lile lilisusiwa lakini pia soko lile sasa hivi ni bovu na halikuwahi kuhamiwa na wananchi wa Jimbo la Micheweni. Mhe. Waziri nakuomba sana uangalie kwa jicho la huruma, kwa sababu kama unavyojua Micheweni sasa hivi imekuwa na tunategemea kutakuwa na malengo makuu ya mwaka 2016/2017, tuna matarajio makubwa kwenye maeneo ya utalii tutakuwa tuna viwanda na maeneo mengine ambayo mji wetu ule utazidi kukuwa.

Sasa nakuomba Mhe. Waziri tukiangalia kwenye Wilaya ile tuna masoko ambayo ni madogo madogo mahitaji yake ni madogo sana. Tukijengewa soko lile watu wa Micheweni Chamboni na Shumba ya Mjini watakuwa kituo chao ni lile soko lililopo pale Micheweni nyuma ya Ofisi ya Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Waziri kwa kweli nakuomba sana ili uweze kuiona Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwanza kwa kuweza kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya Micheweni.

Mhe. Spika, imeelezwa hapa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kama kuna ujenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, nakumbuka Halmashauri ya Micheweni kwenye ofisi yake ile ina upungufu mkubwa sana, na kama tunavyojua mapato ya Wilaya ya Micheweni ni madogo sana kwenye Halmashauri yake. Nakuomba sana Mhe. Waziri uweze kuwaongezea kwenye fungu ili waweze kupata vifaa vya ofisini na ukuta uliopo pale wakuzungumzishia ofisi ile haujafikia malengo na mahitaji yake. Mhe. Waziri nakuomba sana uweze kuisaidia Halmshauri hii kwa hali na mali.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele niende kwenye Kikosi cha KVZ. Mwaka 2005 kulikuwa na kiwanja kimepimwa kwa Ofisi ya KVZ Micheweni, Mheshimiwa lakini ofisi ile haijafika hatua yoyote Mhe. Waziri, nakuomba sana utakapokuja kutoa majumuisho uweze kunieleza, ni sababu gani ambazo ofisi ile haijafikia malengo na vijana wetu wale wa KVZ na wao Micheweni waweze kupata ofisi yao.

Mhe. Spika, kama tunavyojuwa Mhe. Waziri, tukirudi nyuma, tuna matumaini makubwa na *Rest House* yetu ya Micheweni itajengwa mwaka 2016/2017 na tuna matarajio makubwa kama walinzi wetu watakua ni wale wale vijana wetu ambao ni wa KVZ. Mhe. Waziri, suali hili nakuomba sana ulichukuwe na uweze kulifanyia kazi kwa mahitaji yetu ya Serikali.

Mhe. Spika, niende kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Wete. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na nimpongeze Mhe. Rais kwa kuweza kutujengea soko Wilaya ya Wete na kwa kweli tumefarajika sana ingawaje kuna upinzani mkubwa lakini upinzaji hautushughulishi na Mwenyezi Mungu akitujaalia tutakwenda mbele hatua baada ya hatua.

Mhe. Spika, niende kwenye SACCOS. Mheshimiwa kwenye hotuba yako umeelezea kuhusu SACCOS, tunajuwa kwamba vikosi vyetu ni vikosi ambavyo vina mashirikiano na wananchi, vina malengo makuu kwa wananchi na kama sisi wanawake tuna SACCOS zetu lakini tunategemea Halmashauri. Mheshimiwa, Halmashauri ya Micheweni kama nilivyokwambia mapato yake ni madogo sana kwa sababu Wilaya ya Micheweni ni Wilaya ndogo sana kiugavi, lakini nakuomba sana Mheshimiwa kwenye malengo yako uangalie kwenye SACCOS za wanawake za Wilaya ya Micheweni, ili na wanawake hawa walioko Wilaya ya Micheweni nao waweze kufaidika na SACCOS hizi.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele niende kwenye Kikosi cha Zima Moto. Kwanza niwashukuru sana na niwashukuru kwa kuweza kusaidia pahala popote pale panapotokea majanga ya moto wana mashirikiano na wananchi na wakaweza kutoa huduma ile bila ya kujali huyu ni nani na huyu ni nani. Kwasababu ya kusema hivyo, mwaka 2015 Mhe. Waziri, ulitokea moto msitu wa Shumba Viamboni kwa kushirikiana na kikosi hichi moto ule waliouzima kwa kushirikiana na wananchi na wakafika hatua ambayo ni nzuri sana. Mhe. Waziri, nakupongeza sana pamoja na watendaji wako wote.

Mhe. Spika, niende kwenye Jeshi la Polisi. Mheshimiwa naipongeza sana Serikali kwa mashirikiano ya pamoja na Jeshi la Polisi kwenye harakati zetu za uchaguzi wa 2015 hadi kufikia uchaguzi wa tarehe 20 kwa mashirikiano ya pamoja bega kwa bega na kuweza kutulinda juu ya kuwa kulikuwa na kasoro ndogo ndogo lakini hakuna binaadamu mkamilifu anaeweza kuyatengeneza yote; lakini ninakuomba sana Mhe. Waziri, kikosi hichi cha Polisi wawe na mashirikiano na wananchi, watakapokuwa na mashirikiano na wananchi wataweza kufikia malengo ya Serikali na malengo ya wananchi bila ya kunun'gunika kusema kwamba hawasaidiwi kitu chochote.

Mhe. Spika, kwa kuendelea niende kwenye bajeti hii imeelezwa kwenye bandari bubu. Nirudi kwenye Wilaya yangu ya Micheweni, Jimbo la Micheweni. Mheshimiwa kwenye Jimbo la Micheweni kuna bandari bubu nyingi sana, Mheshimiwa kuna bandari ya Shumba Mjini, kuna bandari ya Kiuyu Maziwa ya Ng'ombe, kuna bandari ya Maziwa ya ng'ombe na kuna bandari nyengine zilizoko maeneo ya Micheweni lakini sehemu za ndani bandari ya Kisiwani. Mheshimwiwa nakuomba sana kwa heshima na taadhima, wananchi wa Jimbo la Micheweni nakuomba sana ili kuweza kuwawekea ulinzi kwenye bandari bubu. Kwasababu ya kusema hivyo Mhe. Waziri, bandari hizo zimeambatana na Mombasa, zimeambatana na nchi nyengine. ni bandari ambayo Wakenya wanaingia wala hawana khofu na wa nchi nyengine wanaingia wala hawana khofu, tutakapokuwa na ulinzi kwa kweli tutafikia malengo.

Mhe. Waziri, kama tunavyokuwa juzi tu kuchelewa jana wenzetu wa Tanga wamepata msiba mkubwa sana. Mheshimiwa na sisi kwenye Serikali yetu na usimamizi wako Mhe. Waziri, uweze kuweka ulinzi wa kutosha kwenye maeneo hayo.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele kuhusu... narudia tena nyuma kuhusu mapato ambayo yanaingia na uchimbaji wa matofali na uchimbaji wa mawe. Mhe. Waziri, uweze kuelimisha wafanyakazi wa Halmashauri, ili kusimamia mapato

ya uchimbaji wa matofali Micheweni na uchimbaji wa mawe. Kwasababu maeneo mengi sasa hivi Mhe. Waziri, yameharibiwa kwa uchimbaji wa matofali na mawe. Na kama unavyojuwa Mhe. Waziri, Micheweni unaijua na hali halisi ya Micheweni unaiona imo machoni mwako na kama wananchi wetu wa Micheweni unavyowajua wanataka taaluma ya kutosha, ili kuweza kutoa mapato siku hadi ili Halmashauri ile izidi kuendelea kutekeleza majukumu yake ya miradi mbali mbali ya kusaidia wananchi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru sana, namshukuru na Mhe. Waziri, kwa hotuba yake hii na mimi naiunga mkono, Mhe. Waziri, nataka nikwambie sina la kukupinga isipokuwa nakupongeza sana kwa bajeti hii iliyokuwa ina ufasaha na utulivu mkubwa uliioonesha wakati wa kuwasilisha bajeti hii naunga mkono hotuba hii mia kwa mia. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana, na mimi awali ya yote nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuweza kukutana jioni hii tukiwa salama. Lakini pia nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi hii niweze kusema machache katika Wizara hii.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri na ambayo ameiwasilisha kwetu kwa ujasiri mkubwa, maana yake ameisoma vizuri na kwa utaalamu zaidi.

Mhe. Spika, pia nianze na kumpongeza Mhe. Rais, kwa uteuzi alioufanya hivi karibuni kwa kuwateuwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na hasa niseme Mkuu wa Wilaya yule ambaye ninamfahamu zaidi na ninampa pongezi kama yuko hapa Barazani azidi kunisikia Mhe. Marina. Kwa kweli mama huyu namuelewa utendaji wake wa kazi ni hodari na ni mchapa kazi inshallah Mwenyezi Mungu amsaidie katika majukumu yake haya mapya na wale wenzake wote ambao wamejaaliwa kupata uteuzi huu Mungu awasaidie katika kazi zao ili waendelee vizuri.

Mhe. Spika, nianze na mimi mchango wangu katika Tume Utumishi ya Idara Maalum. Mheshimiwa kwanza mimi nataka kujua ile ahadi ya Mhe. Rais ambayo aliitoa katika kampeni zake katika kuongezea maslahi Makamanda wetu ili na wao walingane na wenzao wa SMT, kama alivyoahidi Mhe. Rais nilitaka kujua tu ahadi hii itatekelezwa lini ili na wao waweze kuwa katika furaha ya kuongezewa posho hilo.

Mhe. Spika, lakini pia nimuombe tena Mhe. Waziri, kuangalia kwa jicho la huruma kabisa wale askari wetu ambao wao wanakabiliana na uokozi yaapotokea maafa. Mheshimiwa hawa ni watu muhimu sana na wanafanyakazi kubwa sana ya ku-*risk* maisha yao ni lazima na wao tuwaangalie kwa jicho la huruma, kama watapewa basi na wao waongezewe zaidi kutokana na uzito ule wa kazi yao. Lakini pia kuangalia kuwapatia vifaa vile muhimu ambavyo vinatakiwa katika kazi zao zile za uokozi ili waweze kufanya kazi zao hizo kwa uhakika.

Mhe. Spika, niende katika Jeshi la Kujenga Uchumi. Mhe. Spika, katika Jeshi hili niseme kwanza nawapongeza sana, kwanza navipongeza sana vikosi vyetu vyote vya ulinzi ambavyo vilituonyesha juhudi kubwa kabisa wakati wa uchaguzi waliweza kutulinda na tukajihakikishia kuwa tupo salama na mpaka muda huu tunaendelea na usalama wetu tunawapongeza sana na Mwenyezi Mungu awazidishie kila la kheri.

Mhe. Spika, Kikosi hichi cha Kujenga Uchumi kwa kweli ni kikosi ambacho kinafanya kazi kubwa ya uzalishaji mali na kama kilivyojieleza hapa kwamba kinatoa mafunzo kwa vijana ya uzalishaji wa kilimo, mifugo na uvuvi na mafunzo ya amali. Mimi nilitaka kujua tu Mheshimiwa kwa kuwa wana kazi na ni muhimu na ni zenye kuongeza kipato, je wanavyo vifaa vya kutosha katika uzalishaji mali huu. Kwasababu ukenda katika kazi za amali lazima wawe na vitu ambavyo wanavitumia vinawasaidia kuongeza ujuzi hao vijana, lakini pia kama ni uvuvi basi wawe na boti ambazo wanakwenda katika huo uvuvi ili waweze kufanya kazi zao hizo vizuri. Kwa hivyo Mheshimiwa utakapokuja utatueleza je, wanazo zana hizo kwa ahili ya kazi hizi kwasababu tunajua wanafanya kazi kubwa na wanaisaidia sana nchi yao.

Mhe. Spika, pia niende katika hichi Chuo cha Mafunzo ambacho kinaonekana kuna programu ya urekebishaji wa wanafunzi. Nilitaka kujua ni mafunzo gani ambayo wanapatiwa ili wanapotoka pale tukaona kweli vijana wetu hawa wamebadilika kweli tabia na sasa wanaweza kujitegemea, kwa kufanya shughuli zao ambazo zitawaingizia kipato na wataondokana na yale yote ambayo yanawasababisha kuingia kule Gerezani.

Mhe. Spika, nije katika Kikosi hiki cha KMKM, kwa kweli nacho nakipongeza kinafanya juhudi kubwa kabisa. Mheshimiwa lakini askari hawa wanajituma lakini wako katika mazingira magumu ya kuwa na vitendea kazi hasa ukijua sskari hawa mara nyingi wanaitumia bahari kwa kweli kupambana na hawa wanaoshughulika na magendo.

Sasa Mheshimiwa kulikuwa kunatakiwa kuwe na boti ambazo ziwasaidie wao katika doria zao ili waweze kuwafikia hao, tena hizo boti ziwe za kisasa kwasababu na hawa wanaofanya shughuli hizo na wa wao wanayo maboti yao ziwe za kisasa ili waweze kupambana nao katika kuwafukuza katika harakati hizo.

Mhe. Spika, mimi nimekaa pale Mkokotoni na nilikuwa niko karibu nao sana, nilikuwa nawaona wanavyohangaika pale wanapoona boti zinatokea huko washazijua kama zile kweli zinahusika na magendo, lakini wao wanazunguka hapa ama hawana mafuta ama mashine yao mbovu hawana uhakika wa usafiri.

Mheshimiwa naomba sana hawa askari wa KMKM hasa walioko katika kituo cha Mkokotoni kwa sababu nasema hivi kwasababu pale Mkokotoni ni karibu na Nungwi, Mhe. Hidaya nilimsikia alivyochangia kwa kusisitiza kuwa na chombo muhimu katika eneo lile Mheshimiwa ni muhimu sana kwa sababu ni sehemu ambayo ina mkondo mkubwa na mara yanapojitokeza maafa wanashindwa wenzetu hawa kukimbilia; kwa hiyo ni muhimu pale kuwa na boti kubwa ya kisasa ambapo hivi juzi nadhani wiki moja au mbili zilizopita walikwenda kuwaokoa watu karibu ya Pangani huko. Sasa ni muhimu katika kikosi kile cha pale kuwa na boti ya uhakika ambayo itaweza kuharakisha pale linapotokea jambo kama lile la maafa.

Mhe. Spika, lakini pia nimsisitize Mhe. Waziri, uingizwaji wa magendo unasababishwa sana na hizi bandari bubu ambazo wenzangu wameziznguzmzia. Bandari hizi bubu kama askari hawa ndio bado hawana boti hizi za kuzungukia katika hivyo vibandari wakagunduwa vitu hivyo vinavyoshushwa basi bado itakuwa tatizo na ndiyo hayo mapato yataendelea kuvunja ili kuikosesha Serikali. Lazima tudhibiti bandari bubu ili wakashushe katika bandari zinazohitajika Serikali iweze kupata mapato yake kama kawaida. Mhe. Spika, pia mimi nimuombe Mhe. Waziri pale anapofanya uwajiri wa vijana wetu katika vikosi. Wenzangu wamelizungumza hili lakini kwa kuwa ni changamoto kubwa kwetu naomba na mimi niliendeleze.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri anapofanya ule uwajili wa kuwaajiri vijana wetu. Ni kweli kuna malalamiko makubwa vijana wetu wanatulalamikia kwamba wanaajiriwa vijana ambao wako nje, wao wako pale wanasota kwa muda wote kambini lakini ikifika ajira wao hawaonekani hawachukuliwi wanachukuliwa watu ambao wako nje ya kambi. Hili ni tatizo na wanatusikitikia sana, tunaomba Mheshimiwa wale waliokwenda pale kupiga kambi na wenzao na kupata mafunzo mbali mbali tunaomba Serikali izingatie kuwapa kipa umbele wale kwanza halafu baadae kuwaangalia wengine kama

kutakuwa kuna mahitaji, ni vijana ambao wanajituma na wana moyo wa kizalendo kusema kweli, kwa sababu bado hawajakata tamaa.

Mhe. Spika, naomba tuwafikirie sana na pia mimi naomba kama tunawaambia kuingia katika makambi hivi kwamba lazima vijana wapite makambini ndio tuwaajiri basi tuwape pia hasa ile ni wanatakiwa wa gani au wawe na kiwango gani cha elimu, ili kupunguza ile watu wanakwenda halafu wakifika wanaambiwa wewe huajiriki tena, wewe huna sifa za kuajiriwa. Sasa ni muhimu tunapowaambia kama waingie makambini basi pia tuwaeleze kwamba ni lazima unapokwenda kujenga taifa pale kambini basi uwe na sifa moja mbili tatu, ili inapotokea ile nafasi mtu huyu aweze kuajirika bila ya matatizo.

Mhe. Spika, pia mimi nilitaka kujua kwa sababu muda mwingi tulikuwa na kilio cha nyumba za askari wetu wanamoishi. Kwa kweli kipindi hicho nyuma zilikuwa zinaonekana chakavu sana hazina kiwango kulingana na wao askari wetu wanaoishi pale. Sasa naomba Mheshimiwa au nilitaja kujua je kuna marekebisho yoyote ambayo yamefanyika katika nyumba hizi wanazoishi au bado na kama bado naomba sana Mhe. Waziri, kulizingatia hili lazima askari wetu jambo ambalo wametuonesha lazima na sisi tuweze kurejesha imani kwao lazima tuwaweke katika makazi mazuri, waweze na wao kuwa na mvuto kama wale askari wengine wawe na hadhi kama walivyo wenzao.

Mhe. Spika, kwa kweli na mimi nilitaka nichangia kidogo katika bajeti hii. Kwa hiyo na mimi niseme baada ya maneno hayo machache naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kunipa uhai na afya njema. Pia shukurani zangu ziende kwako wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Niendelee kuchangia katika hotuba hii ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri, kwa hotuba yake hii iliyo nzuri ambayo kuwa inamuelekeo mzuri pindipo akipatiwa hizi fedha alizoomba na naomba apewe pesa hizi ambazo kuwa ameziomba aweze kutekeleza majukumu yake.

Nawapongeza na watendaji ambao wamemsaidia kazi hii na wanaendelea kumsaidia kazi hii Mhe. Waziri. Lakini pia pongezi kwa Wakuu wa Mikoa wapya na Wakuu wa Wilaya wapya ambao kuwa wameteuliwa karibuni nawapongeza sana, nawatakiwa kila la kheri katika nafasi zao hizo mpya walizopewa katika kusukuma gurudumu la maendeleo.

Mhe. Spika, lakini nina ombi kwa wale Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambao kuwa nafasi zao zimechukuliwa na hawa wapya, waendelee kuwa na busara. Nawaomba sana wawe na busara na hekima na waweke milango wazi kwa wenzao ambao wameshika nafasi ambazo walikuwanazo waweze kuchoma hekima na busara katika pale ambapo watakuwa wamekwazwa katika shughuli zao.

Mhe. Spika, naaza kuchangia katika sehemu zangu kwa kutanguliza maneno yasemayo kwamba: "Tukuza kilicho chako mpaka usahau cha mwenzako". Mhe. Spika, tuna vikosi, vikosi vyetu hivi ndio rasilimali zetu lazima tuvitunze na navipongeza sana kwa kazi zao nzuri wanazozifanya kwa kutekeleza majukumu yao ya ulinzi pamoja na uzalishaji mali. Wanaisaidia sana serikali yao na bado hawajachoka. Kwa hivyo, ni lazima tuweze kuwapongeza kwa dhati kabisa na kuwapa kila nafasi ambazo zinastahiki.

Mhe. Spika, niende katika masuala ya vizazi na vifo na vitambulisho. Nawapongeza idara hii kwani ni idara muhimu na idara maalum na napongeza serikali kuweka pamoja baina ya vizazi, vifo na vitambulisho. Ofisi hizi zilikuwa mbali mbali lakini sasa ziko pamoja. Lakini nimuombe sana waziri atakapofika kule kuitembelea Ofisi ya Vizazi na Vifo iliyoko Wilaya ya Wete aifanye iwe bora zaidi, kwani ofisi hii bado ina changamoto nyingi sana mazingira yake hayafanani kabisa. Ofisi muhimu lakini ukifika wakati mwengine nawaonea huruma wale watendaji wa kule, wanaweza kutafuta kitu kwa muda mwingi wakati mwengine hakipati kulingana na mazingira yalivyo, iboreshwe au ifanywe iwe bora zaidi ofisi hii.

Mhe. Spika, niendelee kuwasifu viongozi hawa kwa kuchukua juhudi ya kuwasomesha wafanyakazi, wameweza kuwafundisha wafanyakazi 229 wanawake na wanaume. Hii ni hatua nzuri kwa wizara hii kuwaendeleza wafanyakazi.

Niendelee katika kuchangia kwa upande wa usajili wa vizazi na vifo. Pale ambapo wamesajili vizazi vipatavyo 39,359 nawapongeza, vifo 286, ndoa 125 na talaka 16; hizi talaka nazichukia siwapongezi kwa Unguja na Pemba ni 16. Lakini namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anambia ni mkakati gani aliyouweka kwa ajili ya wananchi kuwaelimisha kusajili hivi vizazi na vifo pamoja na ndoa na talaka. Kwa sababu ninavyoona kwa uzoefu wangu sehemu hizi bado hazijakuwa na muamko vizuri. Niwashukuru kwa upande wa vizazi tayari vinaendelea vizuri lakini vifo havisajiliwi, talaka hazisajiliwi, ndoa ni chache sana nazo ni kitu muhimu sana katika takwimu za nchi.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja ni mkakati gani ambao ameweka katika kuona anawapatia elimu wananchi walioko vijijini, ili na wao waweze kujisajili pale yanapotokezea.

Mhe. Spika, niende katika kuchangia Ofisi ya Mdhamini Pemba na Mkuu wa Mkoa wa Kusini. Ofisi ya Mdhamini Pemba hadi hivi sasa inatumia majengo ya kupanga, lakini pia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa sioni kwamba ina hadhi ya kuwa ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, inakuwa kama ni nyumba ya mtu binafsi tu. Namuomba sana Mhe. Waziri afanye mpango wa makusudi kushirikiana na serikali, Wizara ya Fedha na Mipango kuweza kuweka mpango wa kujenga ofisi za kisasa, tukiweza kupata jengo moja kama pale pa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa eneo lile litaweza kuchukua nafasi kubwa na ofisi nyingi zitakuwepo pale tutaepukana na fedha yetu kuipeleka kwengine badala ya kuihifadhi tukaweza kufanya shughuli nyengine za kuendesha serikali yetu.

Mhe. Spika, niende katika Mkoa wa Kaskazini Pemba. Katika hotuba hii Mhe. Waziri ameonesha humu katika hotuba hii kwamba Mkoa wa Kaskazini Pemba umeonesha jumla ya shilingi 86,792,000 kwa miradi ya maendeleo aliyopanga kwa mwaka 2016/2017. Namuomba atakapokuja anambie ni mipango gani ambayo ameipanga kuwa ni miradi gani katika kipindi hiki ataweza kuitekeleza kwa fedha hizi, naomba sana alieleze Baraza hili.

Mhe. Spika, tuondoke twende kwenye Madiwani. Mimi naungana katika masuala ya madiwani wetu tuliowachagua. Madiwani wamechaguliwa sambamba na sisi tulivyochaguliwa, lakini madiwani hawa hadi leo kila siku tunapata simu hizi na hizi vipi huko, kama wananisikia na hivi sasa watajua kwamba kweli naufikisha ujumbe wao. Madiwani hawa ni wenzetu na wanatusaidia, tunasema hawa ni askari wa miguu ambao watatusaidia sisi wawakilishi hapa tukiwa katika shughuli za kuendelea kuleta maendeleo katika majimbo kama tulivyoahidi wakati wa kampeni. Nawaombea sana watu hawa. Lakini pia kuna kilio zaidi katika madiwani Wilaya yangu ya Wete, wakisikia wenzao baadhi ya wilaya wameanza kupata maposho katika wilaya yangu hawajapata posho wana kilio hicho kwa nini wenzao wameanza kupata posho, lakini katika Wilaya ya Wete hasa Jimbo la Mgogoni hawajapata chochote. Naomba Mhe. Waziri hili alifuatilie aone ukweli uko wapi.

Mhe. Spika, naomba nichangie kwa upande wa vikosi vyengine kama KMKM, vikosi kwa ujumla wake. Kama nilivyosema tutunze kilicho chetu Mhe. Spika, vikosi vyetu vinajitahidi kufanya kazi vizuri lakini kuna manung'uniko ambayo yanafaa kuangaliwa tokea mwanzo, tulipoanza Baraza hili tunapiga kelele

kufanywa maslahi yao kuwa mazuri kama vile mishahara lakini naongeza kwenye maposho.

Hawa wanapatiwa posho za chakula lakini ni ndogo sana hasa ukizingatia wenzao kule Tanzania Baraza wanavyojaliwa na serikali yao na wao pia wanataka waangaliwe. Posho la shilingi 70,000 ni ndogo sana naomba liangaliwe vizuri pamoja na kwamba serikali imeshaweka bajeti yake lakini itafute namna, kama si mwaka huu lakini serikali ijue kwamba posho ni dogo sana la chakula.

Sambamba na KMKM katika vikosi hivi nina jambo moja nalishauri sana, KMKM ni kikosi chetu cha kuzuwia magendo na magendo haya yako baharini na nchi kavu, lakini sijui hawa KMKM wote wanajua kuogelea na kuzamia. Ni imani yangu kwamba aliyeko juu kuna siku ataambiwa ingia kwenye chombo wende ukalinde baharini. Je, yule atakuwa anashindana jiwe kwa kuzama kama hataanza kupewa mafunzo. Kwa hivyo, wapewe mafunzo ya kuogelea na kuzamia kama wanavyopewa mafunzo mengine ya silaha na ulinzi, lakini mafunzo hayo iwe ni mafunzo ya lazima nashauri sana hilo.

Mhe. Spika, iendelee kwa upande wa Kikosi cha JKU, kikosi ambacho najivunia kuwa na mimi ni muanzilishi wa JKU. Nimekuja mwaka 1977 ikiwa mimi niko kambi za vijana tukaipokea kule Upenja, nimeweza kuhenyeka nayo mpaka leo nambari yangu ninayo. Kwa hivyo, hawa JKU nawapongeza kwa kazi zao ni watu mahiri sana na wanajituma sana kwa uzalishaji lakini wanahitaji msukumo wa ziada. Kikosi hichi ambacho kinafanya uzalishaji wa mazao mbali mbali ikishirikiana kama vile Chuo cha Mafunzo no vile vile wanajitahidi katika uzalishaji wa mali. Ni vyema pale ambapo tunaona jitihada kama hii tusiiachie, tunapiga kelele kwa habari ya chakula nchini lakini wenzetu hawa wamo katika jitihada hii, ni vyema tuwaangalie. Wamezalisha mazao mbali mbali kama vile mpunga, mahindi na mboga mboga.

Kilimo cha mboga mboga wamejitahidi sana na wanaendelea. Kwa hivyo, tuwape nguvu watu hawa tuondokane na yale mazao ambayo tunaweza kuzalisha hapa tuyazalishe, yale masoko tuliyosema tutajenga kule kwenye sehemu mbali mbali za mikoa yetu yatumike. Katika kambi zetu hizi tukiziimarisha vizuri kwenye maeneo kama haya ambapo mboga mboga ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu yataweza kusaidia mapato katika vikosi vyetu wataweza kupata baadhi ya huduma ambazo ziko nje ya bajeti yao, lakini pia wataendelea kuchagia mapato. Kwa sababu nao ni wadau wazuri wa kuchangia mapato tunawashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Spika, niendelee kuchangia kuhusu suala la kuvunjwa kwa Halmashauri. Kutokana na mabadiliko yaliyopatikana sasa hivi ya kuanzishwa Mabaraza ya Miji kuongezeka imepelekea halmashauri nyengine kuvunjwa. Mimi sipingi hili Mhe. Spika, lakini hebu tuangalie lile lengo la zamani kuanzishwa hizi Serikali za Mitaa, kuanzishwa hizi halmashauri halitapotea? Kulianzisha suala hili serikali kwa sababu ya kutoa huduma karibu lakini leo kama tutazichukua halmashauri zote tuzipeleke kwenye Mabaraza tuziweke mijini kule vijijini zitaweza kufanya kazi vipi, ukizingatia halmashauri hizi zimejitahidi kujenga majengo yao makubwa yenye gharama kubwa sana peza za walipa kodi hizo zimekwenda hapo, leo tukisema ofisi ile haiko tena nini tumepanga katika kuyatumia majengo hayo?

Kwa mfano, ukiangalia Halmashauri ya Wilaya ya Wete lipo jengo zuri la kisasa lenye gharama kubwa sana, jengo lile kama tutaondoka ofisi ile pale sijui tuna mpango gani. Nimuombe Mhe. Waziri majengo kama yale kama limefanikiwa suala hili la kuweka Halmashauri kuwekwa kwenye Baraza basi angalau tuendelee kulitumia iwe ni sehemu ya Baraza kwa kutoa huduma sehemu kama hizo. Watu wameshazowea kwenda pale leo ukamwambie mpaka aende Wete, kwa kweli ni usumbufu. Kwa hivyo, nashauri sana ofisi zile hata kama ni Micheweni maana nasikia Micheweni bado hawajaweza kuwekwa Mabaraza, lakini pale Wete ambapo yameshawekwa basi tuweze kulitumia jengo lile. Huo ni ushauri wangu.

Mhe. Spika: Mheshimiwa una dakika moja.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri aangalie sehemu za mapato. Mapato machimboni yanapotea pamoja na kwenye madiko. Halmashauri sidhani kwamba sasa hivi wanafanya kazi katika madiko na yale machimbo vizuri kwa kuweza kukusanya mapato. Hizi ni sehemu ambazo mapato yamo lakini naona yanavuja tuangalie vizuri sana.

Mwisho naomba Waziri wa Fedha aweze kuwaingizia fedha zao zote walizoomba bila ya kupungua na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Spika, kwa heshima yako nashukuru kupata nafasi hii. Wahenga wamesema, naomba kunukuu: "Ng'ombe akianguka malishoni hujikokota na zizini kusaidiwa". Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri asiwe na wasiwasi nimeikubali hotuba hii ya bajeti kwa asilimia mia moja kabla sijazungumza chochote. Nimeikubali kwa sababu amezungumza pande zote za Unguja na Pemba katika kuleta maendeleo ya watu. Kwanza

Mhe. Waziri afahamu yeye ndiye waziri wetu wa watu katika nchi hii ya Zanzibar. Katika maelezo yake amezungumza maendeleo na kuzungumza hadi Barabara za Mwanakwerekwe za ndani kwamba ataziweka lami ahsante sana.

Mhe. Spika, mimi nataka kuzungumzia uanzishwaji wa Manispaa hizi mbili, Wilaya ya Magharibi 'A' na "B'. Mheshimiwa ili programu ya uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zifanye vizuri, basi kuna mambo tunayahitaji, lazima kuwe na eneo la kijografia eneo ambalo tayari lipo, lakini pia tunahitaji kuwa na chombo cha *council* au halmashauri zinazoundwa na pande mbili. Wawakilishi wa wananchi ambao ni madiwani na watendaji wa kisekta wa halmashauri hapa nina wasi wasi. Madiwani wetu mpaka sasa hivi kama walivyozungumza wenzangu hawajijui wako wapi, wana *hang*. Juu hawako, chini hawako la kwanza, lakini hilo sina tatizo najua mambo yatarekebishwa.

Tatizo langu jengine lakini ambalo ni kubwa hawa watendaji wa sekta nina wasi wasi nao, sizungumzii Magharibi tu nazungumzia karibu Unguja na Pemba. Je, tunao *qualified person* wa vitengo hivi labda kunakuwa na Idara ya Ujenzi, barabara, elimu, tunao watu hawa na hivi ndivyo vigezo vimoja vya kuanzisha Manispaa.

Pia kuwe na majukumu yaliyopambanuliwa yepi ya Serikali Kuu, yepi ya Halmashauri. Je, tumejitayarisha na mambo hayo? Wasi wasi wangu kwamba mambo mengi yatakuwa kwenye Serikali Kuu na yakishakuwa huko maana yake Manispaa watakuwa wanangojea kulishwa hawatakuwa na maamuzi. Sasa huo ni wasiwasi wangu. Vile vile kuwa na vyanzo vya mapato vya ndani au nje je, vipo.

Mhe. Spika, ukitaka tena kuanzisha Manispaa ambayo pia nina wasiwasi kuna vitu kama hospitali sijui kama Magharibi 'A' na 'B' tunayo, tuwe na maji ya kutosha, tuwe na *recreation* (sehemu za michezo) na vitu vyengine. Hivi ni vigezo vya kuwa na manispaa. Sasa Mhe. Waziri akina labda atufahamishe kwa sababu tunataka kuona Manispaa nzuri.

Mhe. Spika, kubwa zaidi sijui kuna kigezo gani ama nani anateuwa Mkurugenzi wa hii Manispaa, utanisamehe Mhe. Spika, kwa sababu wakurugenzi ambao wapo sasa hivi walikuwa wanaitwa makatibu sasa, wanaitwa wakurugenzi. Sasa wasi wasi wangu wakurugenzi hawa wa Manispaa mpya wasije wakawa kama wale wapigaji wa Benbati, wale wazee wana vioo vikubwa sana lakini baada ya nyimbo kwisha wanaambukia mlenda kwa sembe. Kwa maana ninayozungumzia mimi ni mshahara wao. Sasa hivi wote utawakuta wanalalamikia mishahara lakini wanaitwa wakurugenzi.

Jengine katika mambo ya Manispaa, hili nina ushahidi kwa sababu niliwahi kushiriki, vigezo hivi kama havijatimizwa basi tunaweza kukosa hata misaada kutoka kwenye taasisi nyengine ambazo zinahesabu kuwa tuna Manispaa. Kwa hivyo, naomba katika hili tukae tusiamue tu moja kwa moja tukasema tuna Manispaa Magharibi 'A' na Magharibi 'B', je tunazo hizi sifa? Mhe. Waziri akija anaweza akatusaidia kidogo.

Mhe. Spika, lakini jengine Mhe. Waziri nimesema kwamba yeye ndiye waziri wetu kwa watu wote, kuna mawaziri wengine samahani wa misitu, wa viwanda, lakini yeye wa watu. Kuna kitu *local government reform* ningependa tu akija atujuilishe labda zimefikia wapi, iko vipi, tumekwama wapi. Kwa sababu sasa hivi ni muda mrefu wananchi hatujajua tunakwenda wapi na *reforms* na muda ushapita na sheria ishawekwa saini.

Mhe. Spika, jambo la tatu nakuja kwenye usafi na hasa kwenye jimbo langu la Mwanakwerekwe, nashukuru. Naishukuru Halmashauri, na nawashukuru watendaji wake, lakini bado tujitahidi. Sina uhakika kama ni watendaji ama ukorofi wa wafanyabishara, lakini bado 25% haijakuwa *implemented*. Kwa hivyo, nashukuru kwamba angalau tumefikiwa 25% binaadamu anaweza akakaa, binaadamu anaweza akasema kwamba hapa kuna taasisi ya serikali.

Mhe. Spika, tunakwenda kwenye Manispaa. Mhe. Spika, ukiwa mfanyakazi wa Baraza la Manispaa basi unaweza kuwa meneja muda wowote. Labda mnaweza mkanishangaa. Nina maana hii na hapa nawaomba Manispaa wawasomeshe watu wao hasa kwenye mambo ya *financial aspect.* Unaweza ukamkuta mtu anaongoza Soko kama Mwanakwerekwe, soko ambalo linatoa karibu shilingi 40 milioni kwa mwezi, wamemchukuwa mtu ambae alikuwa anakata miti wakamuweka meneja, wakamuondosha yule wakamchukuwa mwengine ambaye kazi yake kufagia au Mkuu wa Majaa wakamuweka meneja, wakachukuwa mtu mwengine kutoka sehemu ambayo haifahamiki, hiyo ndiyo tabia ya Manispaa. Matokeo yake sasa kinachopatikana hakifahamiki. Anayekata risiti anafanya anavyotaka yeye kwa sababu utawala wenyewe unakuwa hauna uisimamizi bora.

Kwa hivyo, nawaomba Manispaa katika vifungu vyao watafute watu wawapele kwenye taasisi hata kama kwa mwezi mmoja wasomee mambo ya pesa, lakini tuwe na watu ambao wanafahamika. Manispaa karibu itakuwa jiji sasa kama unamchukuwa mtu mchimbaji wa mchanga unamuweka meneja. Unamchukuwa Mkuu wa Vikosi unamuweka meneja nadhani Mhe. Waziri hii tuirekebishe kidogo.

Halafu kuna tuhuma, maana yake sina uhakika, wanasema kwamba kuna baadhi ya askari hasa KVZ wamekwenda kwenye mafunzo wako wengine wamepewa vyeo wengine hawakupewa. Sasa namuomba Mhe. Waziri hili tuinamishe vichwa vyetu, nimesema tuhuma sina uhakika.

Jengine hapa watu wataanza kunicheka kwa sababu ya hivyo tena, lakini hizi *CCTV* za wizara mimi nashukuru sana kwamba sasa hivi zipo zinatizama matatizo ya mji, lakini hata sisi huku pembeni ya mji nadhani tuna matatizo makubwa zaidi kuliko hata mjini. Kwa sababu mjini ukimfukuza mtu utampata barabara ipo, mwakupita mumo, taa zimo, *ok* na sisi taa zipo. Lakini mimi ningeomba angalau japo kuwa mbili akatusaidia katika shilingi 18 milioni akatuwekea sokoni. Sokoni kuna vitendo vyote tunavyovijua vinafanywa mjini, lakini pia ingetusaidia sisi tungeweka huku barabarani tunakofukuza watu wale wanaouza bila ya mpango. Basi tukawa hatuna kazi ya kufukuza, usiku ukifika tunachukuwa sura zao tu, nadhani ingetusaidia.

Mhe. Spika, nakuja na shukurani na ombi. Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kitabu chake kunihakikishia kwamba na Mwanakwerekwe wanasikia barabara yetu ya Msumbiji, Mwanakwerekwe na Makaburini itajengwa kwa lami. Lakini pia Mhe. Waziri kuna barabara ya kutoka Magogoni kwa Mabata kwenda Kinuni. Kinuni wakati mwengine mpaka Mwera, naomba sana hata kama hatutafanikiwa kwa lami basi iwe kwa angalau kifusi cha *quality*. Namuomba sana Mheshimiwa na ikiwezekana basi akipata siku angalau apande kwa Mabata aende Kinuni ateremke chini. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Abdalla Ali Kombo sasa naomba nimuite mchangiaji wa mwisho Mhe. Mohammed Mgaza Jecha.

Mhe. Mohammed Mgaza Jecha: Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Oh! Samahani Mheshimiwa utachangia mtu wa mwanzo Jumatatu nimesahau muda umeshakwisha. (*Makofi*)

Mhe. Mohammed Mgaza Jecha: Haya ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda umeshamalizika wachangiaji bado wapo nitapenda ajifahamu huyo mmoja tu kwa sababu nilikuwa nimeshamgaia nafasi ya kuchangia. Lakini wachangiaji bado wengi sana na hoja hii tunaihitimisha asubuhi ya siku ya Jumatatu kwa sababu mchana tutakuwa tunaanza kusikiliza hoja nyengine.

Kwa hiyo, ningewashauri watu ambao watakuwa hawajafikiwa basi wachangie kwa maandishi. Kwa sababu walioomba ni wengi sana pamoja na kwamba muda tumeubana. Waheshimiwa Wajumbe baada ya maelezo hayo naomba sasa niakhirishe shughuli za Baraza mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa. 1.45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi Jumatatu tarehe 06/06/2016 Saa 3.00 Asubuhi)